# Nipashe

Jumatatu Juni 10, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579940

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Wakurugenzi wapingwa tena kusimamia uchaguzi madiwani

UKURASA 2




UKURASA 13

# Vigogo TRA waingia mikononi Takukuru

**WAANZA** kuhojiwa baada ya JPM kutaka wachukuliwe hatua kwa tuhuma za rushwa...

*Endelea uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**MELI MPYA KUNUFAISHA WAKAZI KANDA YA ZIWA**

WANANCHI wa Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera na mikoa ya jirani inayozunguka Ziwa Victoria, wanatarajia kunufaika na meli mpya ...

UKURASA WA 3

**MSAKO MKALI WAPIGA RAMLI CHONGANISHI**

JESHI la Polisi Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, limetangaza kufanya msako mkali kila kata, kijiji na vitongoji dhidi ya waganga wa tiba asili wanaoendelea kukaidi ...



Wafanyabiashara wadogo wa Mwenge wilayani Kinondoni jijini Dar es Salaam wakiyaimarisha mabanda yao jana, baada ya kuhamishiwa eneo la Coca-Cola kupisha upanuzi wa Barabara ya Ali Hassan Mwinyi kutoka Mwenge-Morocco. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

## KIGOGO POLISI AFA KWA KUJINYONGA

UK 3

**RIPOTI MAALUM**

## Tamu, chungu bajeti serikali awamu ya 5

UK. 4

**MICHEZO** VITA YA KUCHEZA AFCON YAPAMBA MOTO STARS UK.31

MAONI, KATUNI UK.6

# Vigogo TRA waingia mikononi Takukuru

Na Romana Mallya

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) inawashikilia maofisa kadhaa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ukiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli dhidi ya tukio la watumishi hao kudaiwa kumnyang'anya mfanyabiashara bidhaa zake kwa muda wa miaka mitatu.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo Ijumaa Ikulu katika mkutano kati yake na wafanyabiashara baada ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kueleza mbele yake kuwa kuna watumishi wa TRA walihusika katika tukio la kumnyang'anya mfanyabiashara bidhaa zake kwa muda wa miaka mitatu.

Baada ya maelezo hayo, Rais Magufuli alimwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Kamishna wa Polisi, Diwani Athuman, awakamate maofisa hao na kuwaweka ndani kisha kuwafikisha mahakamani, huku TRA ikitakiwa kuwasimamisha kazi wakati kesi ikiendelea.

Akizungumza na Nipashe jana Kamishna wa Polisi, Athuman, alisema baada ya agizo walilopewa na Rais Magufuli kuhusiana na tukio hilo, utekelezaji wake ulianza mara moja.

"Rais Magufuli alitoa maagizo Takukuru kuhusu maofisa wa TRA waliohusika kwenye tukio la rushwa dhidi ya mfanyabiashara, maagizo ya Rais yalianza kushughulikiwa siku ile ile kwa sasa tunaendelea nayo.

"Hivi karibuni tutatoa taarifa yake...tumeanza uchunguzi wake na wapo baadhi ya watu tunao tayari... kwa sasa naweza kusema hivyo," Kamishna wa Polisi Athuman aliiambia Nipashe.

**KAULI YA TRA**

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, alipoulizwa kuhusu utekelezaji wa agizo la Rais Magufuli alisema watayatekeleza.

"Ni kweli tulipokea maagizo ya Rais Magufuli. Tutayatekeleza, si unajua baada ya kutolewa maagizo TRA kumefanyika mabadiliko na leo (jana) siyo siku ya kazi hadi kesho (leo), nitakuwa kwenye nafasi

INAENDELEA UK. 8



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na mkewe Mary (kulia), wakimjulia hali Mama Maria Nyerere anayepatiwa matibabu jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: OWM**

# JPM atajwa kubadili mfumo wa uongozi

Na Beatice Moses

RAIS John Magufuli ametajwa kubadili mfumo wa uongozi kwa kuhakikisha hawakai ofisini, badala yake wanawafuata wananchi, wanawasikiliza na kutembelea miradi ili kupata ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, aliyabainisha hayo juzi katika uzinduzi wa ofisi za walimu wa Shule ya Msingi Vijibweni, Kigamboni, zilizojengwa kwa ufadhili wa kampuni ya CRJE (East Africa) Limited ya China.

Alisema Rais Magufuli amekuwa akiwaza maendeleo ya wananchi kila siku, hivyo viongozi aliowateua wanapomwangusha anaumia, kwa kuwa nia yake ni kufanya kazi.

"Moja ya kazi kubwa tulizopewa si kukaa ofisini, yaani umkute mkuu wa mkoa au wa wilaya yuko ofisini kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa anafanya nini? Kwani amekuwa 'secretary' (katibu muhtasi)? Tunatakiwa kufuatilia miradi inavyokwenda na kuwafuata na kuwasiliza wananchi," alisema Makonda.

INAENDELEA UK. 8

# Wakurugenzi wapingwa tena kusimamia uchaguzi madiwani

Na Enock Charles

KADA wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Bob Wangwe, amesema anakusudia kufungua kesi mpya ya kupinga wakurugenzi wa halmashauri nchini kusimamia uchaguzi wa madiwani.

Akizungumza jana na gazeti hili, Bob Wangwe alisema hukumu iliyotolewa Mei 10, mwaka huu na Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam, haikuwazuia wakurugenzi hao kusimamia uchaguzi huo.

Alisema hiyo inatokana na ukweli kuwa uchaguzi wa madiwani unasimamiwa na sheria ya uchaguzi wa serikali za mitaa, huku uchaguzi wa rais na wabunge ukisimamiwa na Sheria ya Taifa ya Uchaguzi.

"Sioni ni wapi Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) inashindwa kutumia mamlaka yake kuteua wasimamizi 'impartial' (huru) tofauti na hawa wakurugenzi. Ipo haja ya kurudi mahakamani," alisema Wangwe.

Juni 2, mwaka huu, vyama nane vya upinzani nchini vilitoa tamko la kutoshiriki uchaguzi mdogo wa madiwani katika kata 32 unaotarajiwa kufanyika Jumamosi kwa kile walichodai kuwa Nec imepuuza hukumu ya Mahakama.

Hukumu ya Mahakam Kuu iliyotolewa Mei 10, mwaka huu na jopo la majaji watatu, Dk. Atuganile Ngwala, Dk. Benhajj Masoud na Firmin Matogolo, ilibatilisha kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Uchaguzi kinachoipa Mamlaka NEC kuteua wakurugenzi wa miji, majiji na manispaa kuwa wasimamizi wa uchaguzi na kifungu cha 7(3) kinachoipa NEC mamlaka ya kuteua mtumishi yeyote wa umma kuwa msimamizi wa uchaguzi.

Mahakama hiyo ilisema kuwa vifungu hivyo ni kinyume cha Katiba kwa kuwa wakurugenzi ni wateule wa Rais na si waajiriwa wa NEC, hivyo kuifanya tume hiyo kutokuwa huru.

Hivi karibuni, aliyekuwa Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Fatma Karume, alisema kuna sheria mbili zinazosimamia uchaguzi wa rais na wabunge na pia ipo sheria inayosimamia uchaguzi wa serikali za mitaa. "Uamuzi wa Mahakama Kuu umelenga uchaguzi wa rais na wabunge kwa sababu huchaguliwa chini ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, hawa wengine wanachaguliwa chini ya sheria ya uchaguzi ya serikali za mitaa, ambayo haijapigwa marufuku," alisema Fatma ambaye pia ni wakili wa kujitegemea.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Athuman Kihamia, alinukuliwa akisema kuwa uchaguzi huo haujaenda kinyume cha hukumu ya Mahakama kwa kuwa unasimamiwa na sheria tofauti na ile iliyofanyiwa maamuzi.

"Tume inaheshimu maamuzi ya Mahakama Kuu na inawahakikishia haijagusa au kuathiri sehemu ya vifungu ambavyo Mahakama Kuu imevitolea hukumu," alisema Dk. Kihamia. Uchaguzi wa madiwani unasimamiwa na sheria ya uchaguzi sura ya 292 ya mwaka 2015, ambayo imeeleza taratibu na namna madiwani wanavyochaguliwa ikiwamo mamlaka zinazosimamia uchaguzi huo.


PHARMACEUTICAL SOCIETY OF TANZANIA (PST)
PST OFFICE: P.O. BOX 55666, DAR-ES-SALAAM, TANZANIA
Tel.: +255 753800918 Email: info@pst.or.tz

**TAARIFA KWA UMMA**

Chama cha Wafamasia Tanzania (PST) kwa kushirikiana na wanachama shiriki wa Umoja wa Wanawake katika Taaluma ya Famasi (TAWOPHA), Jumuiya ya Wanafunzi wa Kada ya Famasi (TAPSA) na wanataaluma wote kwa udhamini wa Baraza la Famasi (PC) tutaadhimisha Wiki ya Famasi nchini kuanzia 11 hadi 16 Juni, 2019 nchini kote. Kauli Mbiu ya mwaka huu ni **"MFAMASIA WAKO NI ZAIDI YA UTOAJI WA DAWA".**

*Ewe Mwananchi Mshirikishe Mfamasia kwa Masuala yote Yanayohusu Dawa na Afya yako.*

Katika maandhimisho hayo, shughuli mbalimbali zitafanyika ikiwa ni pamoja na; kuhamasisha umma kupitia njia mbalimbali kuhusu masuala yanayohusu afya kwa ujumla na matumizi sahihi ya dawa. Sambamba na uhamasishaji huo, zoezi la utoaji wa dawa za minyoo litafanyika katika mashule na jamii zinazotuzunguka katika vitongoji vya Jiji la Dar es Salaam hususani maeneo ya; -

- **Mlimani City – Mwenge;**
- **Kibo Complex – Tegeta; na**
- **Kiwanja cha Mwembe Yanga – Temeke.**

PST inawaomba wafamasia wote nchini washiriki katika uhamasishaji kwenye maeneo yao ya kazi kama sehemu ya maadhimisho haya. Vilevile, naomba wananchi wote tujumuike katika maadhimisho ya **"WIKI YA FAMASI 2019"** ili muweze kuelewa haki zenu za msingi kuhusu matumizi sahihi ya dawa na huduma za kitaalamu.

**Issa S. Hango**
**Rais wa Chama cha Wafamasia Tanzania.**

215265902

## HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (wa pili kulia) akimwangalia kobe ambaye anakadiriwa kuwa na miaka 100, huku akipewa maelezo na Ofisa Wanyamapori wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Proches Rongoma, alipotembelea bustani ya wanyamapori katika maonesho ya Biashara na Utalii mkoani Tanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msako mkali wapiga ramli chonganishi

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

JESHI la Polisi Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, limetangaza kufanya msako mkali kila kata, kijiji na vitongoji dhidi ya waganga wa tiba asili wanaoendelea kukaidi maelekezo ya kuacha ramli chonganishi.

Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Igunga, Ally Mkalipa, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki mbele ya madiwani katika kikao maalum cha Baraza la Madiwani wa wilaya hiyo. Alisema baadhi ya waganga wa tiba asili wanaoendelea kupingana na agizo la serikali kwa watu wanaokwenda kutibiwa kwao, hivyo kusababisha kuendelea kwa mauaji kutokana na kuamini maneno wanayoambiwa na waganga hao. Kwa mujibu wa Mkalipa, hivi karibuni mkazi wa Kata ya Ntobo, alimuua mke wake baada ya kwenda kwa mganga wa tiba asili akiwa mgonjwa na kuambiwa amelogwa na mke wake. Alisema mtu huyo aliporudi nyumbani aliamua kumuua kwa kumkata mapanga.

Alisema kutokana na hali hiyo, Jeshi la Polisi litawaita waganga wote wa tiba asili, ili waeleze sababu zinazowafanya kuendelea kupiga ramli chonganishi wakati serikali ilipiga marufuku.

Mkalipa alisema wataendelea na msako kwa kata, vijiji, vitongoji hadi nyumba kwa nyumba na watakaomatwa wote watafikishwa mahakamani kwa mujibu wa sheria.

Aidha, aliwataka madiwani hao kuendelea kutoa elimu kwa wananchi katika maeneo yao, ili waweze kuacha tabia ya kupiga ramli chonganishi ambayo imekuwa ikipoteza maisha ya wananchi wasiyokuwa na hatia.

Baadhi ya madiwani waliohudhuria katika baraza hilo maalum, Njeli Miley wa Viti Maalumu ( CCM) Kata ya Sungwizi, Rukia Mwakibinga, Viti Maalumu (CCM) Kata ya Igunga, Emmanuel Samson, Diwani wa Ntobo na Charles Bomani wa Igunga (CCM) waliahidi kwenda kutoa elimu katika maeneo yao ili waganga hao waache tabia hiyo.

# Kigogo wa polisi afa kwa kujinyonga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mafunzo na Mapambo wa Jeshi la Polisi Makao Makuu ya Dar es Salaam, Azizi Juma, anadaiwa kufariki dunia kwa kujinyonga.

Azizi ambaye aliwahi kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, alikutwa ameshafariki dunia akiwa amening'inia katika mti wa mlimau uliopo nyumbani kwake eneo la Kijichi.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo, Kamanda wa Polisi Zanzibar, Muhammed Hassan Haji, alisema chanzo cha kifo hicho hakijajulikana.

"Alikutwa amefariki dunia akiwa ananing'inia katika kitanzi kilichofungwa katika mti wa mlimau uliopo nyumbani kwake Kijichi," alisema.

Alisema kifo chake ni pigo na pengo kubwa kwa Jeshi la Polisi.

Aliitaka familia ya marehemu kuwa na moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu cha msiba.

Juma alizaliwa mwaka 1960 huko Michakaeni kijijini kwao kisiwani Pemba.

Alizikwa jana jioni katika makaburi ya Mwanakwerekwe mjini Zanzibar.

# Meli mpya kunufaisha Kanda ya Ziwa

**Na Mary Geofrey,** BUKOBA

WANANCHI wa Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera na mikoa ya jirani inayozunguka Ziwa Victoria, wanatarajia kunufaika na meli mpya itakayokuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo.

Mbali na meli hiyo mpya, meli nyingine ya MV. Victoria inafanyiwa marekebisho na itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200 hadi 4,000 na tani za mizigo 200 na kurahisisha usafiri kwa wakazi hao.

Kaimu Meneja wa Bandari za Ziwa Victoria, Geofrey Lwesya, aliyasema hayo kwa waandishi wa habari juzi walipotembelea bandari hiyo ili kuona miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA).

Alisema ujenzi wa meli hiyo unatarajiwa kukamilika Septemba mwakani na itasaidia kuongeza mapato katika bandari ya Bukoba ambayo licha ya kutokuwapo kwa meli za abiria, yamefika Sh. milioni 60 kwa mwezi kutoka Sh. milioni 29 miaka ya nyuma.

"Mwezi Septemba mwaka 2020, tunatarajia meli hii mpya itakuwa imekamilika ambayo itarahisisha usafiri kwa abiria na mizigo yao. Meli nyingine ya MV. Victoria nayo inaendelea na marekebisho ikikamilika itasaidia sana usafiri katika bandari hii na zote zitasaidia kuongeza mapato," alisema Lwesya.

Kwa mujibu wa meneja huyo, bandari hiyo inatekeleza miradi mbalimbali ikiwamo ukarabati wa jengo la abiria la kisasa na ujenzi wa ofisi inayogharimu Sh. milioni 143.8.

"Baadhi ya majengo muhimu yakiwamo majengo ya abiria, sehemu za kuhifadhia mizigo, vyoo vya kisasa, vibanda vya walinzi na zote vyenye ubora wa kisasa yapo katika hatua za mwisho na tumeboresha maeneo ya bandari yetu iendane na huduma zinazotolewa na bandari hiyo," alisema Lwesya.

Pia alisema mbali na boti ndogo zinazosafirisha abiria katika bandari hiyo, kuna meli ndogo maalumu zinazohifadhi ubaridi kwa ajili ya kubebea samaki kutoka visiwani na kupelekwa viwandani.

Aidha, alisema makusanyo katika bandari hayo yanatokana na wafanyabiashara wakubwa wanaotumia bandari hiyo ikiwamo wanaotoa bidhaa Uganda na Kiwanda cha Sukari cha Kagera (Kagera Sugar) ambaye ndiye mteja mkubwa.

Kwa upande wake Mkuu wa Bandari hiyo, Bulenga Ndaro, alisema meli ni usafiri muhimu unaotegemewa Bukoba, hivyo kusimama kwa huduma hiyo kumesababisha adha kwa watu wengi.

INAENDELEA UK. 8



# Chungu, tamu bajeti serikali awamu ya tano

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI ya awamu ya tano kwa kiasi kikubwa imefanikiwa kudhibiti mianya ya ufujaji wa fedha za umma na kutekeleza miradi muhimu.

Udhibiti huo umefanywa kwa mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuzuia safari holela za nje kwa watendaji wa serikali, kuahirisha sherehe za kitaifa zikiwamo za maadhimisho ya uhuru wa nchi na kuratibu vizuri taratibu za ununuzi wa umma.

Ufujaji wa fedha za umma pia umedhibitiwa kwa kuhakikisha unafanyika uhakiki kabla ya kuidhinisha malipo kwa watoa huduma na makandarasi wanaotekeleza miradi ya serikali.

Pia, uhakiki wa watumishi wa umma umeokoa fedha nyingi ambazo serikali ilikuwa inalipa kwa watumishi wasiokuwapo kazini, maarufu watumishi hewa, huku pia ikifanya marekebisho kwenye viwango vya mishahara ya 'vigogo' wa taasisi na mashirika ya umma.

Serikali ya awamu ya tano pia imeokoa mabilioni ya shilingi kutokana na uamuzi wake wa kuzichukua fedha za mashirika na taasisi za umma na kuziweka kwenye akaunti maalum iliyoko Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Kwa kuchukua uamuzi huo, serikali imeokoa mabilioni yaliyokuwa yanatumiwa na watendaji wa mashirika na taasisi hizo kuwekeza katika miradi isiyozalisha faida, huku wakijilipa mamilioni ya shilingi kupitia posho za vikao walivyokuwa wanavifanya katika miji mikubwa barani Ulaya na Amerika.

Mabilioni yaliyookolewa, yametumika kutekeleza miradi muhimu ikiwamo ya ujenzi wa madaraja, barabara za juu kwenye makutano ya barabara kuu jijini Dar es Salaam na Daraja la Furahisha jijini Mwanza, ukarabati wa shule kongwe zote nchini pamoja na zilizoharibiwa na tetemeko la ardhi Kanda ya Ziwa.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango

Serikali pia imefanikiwa kujenga mamia ya vituo vya afya na hospitali za wilaya nchini, huku ikitoa mabilioni kila mwezi kugharamia mpango wa kutoa elimu bila malipo kuanzia darasa la awali hadi kidato cha nne kwenye shule zake.

Aidha, serikali ya awamu ya tano imeanza utekelezaji wa mradi wa uzalishaji wa umeme kwenye Mto Rufiji, maarufu Stiegler's Gorge, ingawa uamuzi huo unapingwa vikali na wakosoaji wa serikali.

Takwimu za makusanyo zinazotolewa na Mamlaka ya Mapato (TRA), zinaonyesha serikali ya awamu ya tano imefanikiwa kuongeza makusanyo kwa wastani Sh. bilioni 450 kwa mwezi.

Takwimu hizo zinaonyesha kuwa serikali ya awamu ya tano imeongeza makusanyo kutoka wastani wa Sh. bilioni 850 kabla ya Novemba 2015 hadi kufikia Sh. trilioni 1.3 kila mwezi.

Hata hivyo, pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano kuimarisha makusanyo ya nchi kwa kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato, bado kuna utekelezaji usioridhisha wa baadhi ya miradi ya maendeleo inayoidhinishwa na Bunge.

Wakati makadirio ya bajeti ya nne ya serikali ya awamu ya tano yakitarajiwa kusomwa bungeni jijini Dodoma Alhamisi, bado takwimu zinaonyesha kuna utekelezaji duni wa bajeti ya maendeleo licha ya makusanyo ya ndani kuwa makubwa.

Hali hiyo inatokana na kile kilichoelezwa na serikali kwamba kiwango kikubwa cha makusanyo kinatumika kulipa Deni la Taifa na mishahara ya watumishi wa umma.

Taarifa zilizowasilishwa bungeni wakati wa Bunge la Bajeti, zinaonyesha utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa miaka yote mitatu, yaani kuanzia 2016/17 uliokuwa wa bajeti ya kwanza ya serikali ya awamu ya tano hadi 2018/19, umekuwa chini ya asilimia 50 karibu kwa wizara zote, huku baadhi ya wizara zikiwa hazijapewa hata senti moja.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ilieleza bungeni wakati wa Bunge la Bajeti mwaka jana kuwa, kati ya mafungu yote 47 ya wizara mbalimbali yaliyostahili kupata fedha za maendeleo mwaka wa fedha 2017/18, ni mafungu 16 tu yaliyokuwa yamepata fedha kwa zaidi ya asilimia 50 hadi Machi 31, 2018.

Kamati hiyo iliweka wazi kuwa hali hiyo inachagizwa na kiasi kikubwa cha fedha zinazokusanywa na serikali, kutumika kulipa Deni la Taifa. Kamati hiyo ilibainisha kuwa kwa mwaka wa fedha 2017/18, hadi kufikia Februari 2018, serikali ilikuwa imetumia Sh. trilioni 5.54 kulipa Deni la Taifa. Kati yake, Sh. trilioni 4.094 zilitumika kulipa madeni ya ndani na Sh. trilioni 1.446 kwa madeni ya nje.

"Kulingana na Tathmini ya Uhimilivu wa Deni (Debt Sustainability Analysis), deni letu ni himilivu kwa asilimia 34.4 ukilinganisha na ukomo wa asilimia 56.

"Hata hivyo, ukilinganisha makusanyo ya ndani yanayotokana na kodi na malipo ya Deni la Taifa, utaona kuwa mpaka Desemba 2017, makusanyo ya ndani yalikuwa Sh. trilioni 7.678 na malipo ya Deni la Taifa mpaka Februari yalikuwa Sh. trilioni 5.54.

"Ni kwamba kiasi kikubwa cha makusanyo ya ndani kinakwenda kulipa Deni la Taifa," Jitu Soni, aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, alisema.

Wakati kamati hiyo ikibainisha hayo, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2016/17, uliokuwa wa kwanza kwa serikali ya awamu ya tano kukaguliwa, ilionyesha malengo ya makusanyo ya serikali kwa mwaka huo wa fedha yalifikia asilimia 94, lakini fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa zilikuwa chini ya asilimia 50.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alizungumzia changamoto hiyo katika mkutano na waandishi wa habari bungeni jijini Dodoma Aprili mwaka jana, akieleza kuwa inasababishwa na sehemu kubwa ya makusanyo kutumika kulipa madeni ya serikali na mishahara ya watumishi wa umma.

Alisema serikali inakusanya wastani wa Sh. trilioni 1.3 kwa mwezi, lakini kati yake, Sh. bilioni 550 hutumika kulipa mishahara ya watumishi wa umma, Sh. bilioni 600 hutumika kulipa Deni la Taifa na kiasi kinachobaki hutumika kutekeleza miradi ya maendeleo.

"Kwa hiyo, kwenye Sh. trilioni 1.3 umebakiwa na takribani Sh. bilioni 200 ambazo ndizo unatumia kuendesha serikali," Dk. Mpango alisema na kufafanua zaidi:

"Lakini, humo namo kuna shughuli nyingine ambazo hazikwepeki. Kwa mfano, askari wetu shupavu wanalala nje, lazima serikali tuwape posho ya chakula, ndipo na sisi (wabunge) tunaweza kuendeleza vurugu huku bungeni, tukabishana, tukalala nyumbani kwa amani.

"Kuna mishahara ya majaji lazima ilipwe na marupurupu yao mengine, kuna viongozi wetu nao hawalali. Niwahakikishie ni kawaida kabisa kumpigia Rais simu saa nane usiku, saa tisa yuko macho.

"Hawa viongozi wamebeba dhamana kubwa, lazima serikali iwahudumie. Kwa hiyo, unaponiuliza 'hizi nyingine zinaenda wapi?' Ninaweza

INAENDELEA UK. 8

**Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-**

- **Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=**
- **Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=**
- **Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima**
- **Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku**

215227501



# Soko lafunguliwa baada ya kufungwa kwa miaka mitatu

**Na Rose Jacob,** SENGEREMA



NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (pichani), amefungua soko la samaki la Nyakaliro lililoko katika Halmashauri ya Buchosa mkoani Mwanza, lililokuwa limefungwa kwa miaka mitatu kutokana na kukosa usimamizi.

Sababu za kufungwa kwa soko hilo ni uzalishaji mdogo wa samaki na dagaa pamoja na mianya ya utoroshaji wa mazao ya uvuvi.

Ulega alisema juzi kuwa Rais John Magufuli amewatengenezea miundombinu ya soko kwa maslahi mapana ya taifa kwa kutaka wananchi wafanye kazi kwa bidii.

Kwa mujibu wa waziri huyo, wilaya hiyo ina wavuvi 19,383 wanaotegemea soko hilo kupata kipato.

"Sasa tumeweka mfumo mzuri wa usimamizi ndiyo maana leo (juzi) tumefungua soko hili, ili mapato ya serikali yakusanywe kwa haki na wananchi wa maeneo haya wafanye shughuli za kujiingizia kipato kwa kuwa ni kichocheo kikubwa cha uchumi kwa wadau wa sekta ya uvuvi ndani na nje ya halmashauri hii," alisema Ulega.

Aidha, alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Buchosa, Crispin Luanda, kuboresha soko hilo ili wananchi waanze kufanyabiashara ikiwamo kuondoa vikwazo dhidi yao.

Naibu Waziri huyo aliutaka uongozi wa uvuvi Kanda ya Ziwa kumpeleka ofisa ambaye atakuwa anasimamia ukaguzi na kutoa vibali katika soko hilo, ikiwa ni pamoja na mkurugenzi kutafuta mawakala wa huduma za kifedha sokoni hapo ili kuwapa urahisi wafanyabiashara.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi Halmashauri ya Buchosa, Shija Lyella, alisema wananchi wamefurahishwa na kufunguliwa kwa soko hilo ambalo ni chanzo muhimu cha mapato.

Naye Mbunge wa Jimbo la Buchosa, Dk. Charles Tizeba, alimuomba waziri huyo kuiagiza Halmashauri ya Wilaya ya Chato kuacha kuwasumbua wafanyabiashara wanaonunua samaki kutoka katika soko la Nyakaliro na kuruhusu uuzwaji wa samaki nje ambao hawajachakatwa.

# Taasisi za uhifadhi zapewa mchongo Tanga

**Na Mwandishi Wetu, TANGA**

TAASISI za Uhifadhi nchini zimeagizwa kujenga mabanda ya kudumu kwenye uwanja wa maonyesho ya biashara na utalii katika mkoa wa Tanga, ili kuyapa hadhi ya juu badala ya kuwa na mabanda ya muda mfupi.

Pia zimetakiwa kuhakikisha kila mwaka zinashiriki kwenye maonyesho hayo kutokana na mchango mkubwa yaliyo nao katika kuendeleza na kukuza biashara na utalii.

Akizungumza jana wakati akifunga maonyesho ya saba ya biashara na utalii mkoani Tanga, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alisema maonyesho hayo ni fursa ya kutangaza na kuhamasisha wananchi kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo nchini.

Kanyasu alizitaja taasisi hizo zinazotakiwa kushiriki kwenye maonyesho hayo kuwa ni Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa) Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tawa), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Makumbusho ya Taifa na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB).

Pia alizitaka idara za msingi za Wizara ya Maliasili na Utalii nazo kushiriki katika maonyesho hayo ili kuwaelimisha wananchi kuhusiana na shughuli za utalii, misitu, wanyamapori na mambokale.

Alisema kitendo cha baadhi ya taasisi za uhifadhi na idara husika kushindwa kushiriki kwenye naonyesho hayo ni kuwanyima fursa wananchi kufahamu vivutio vya utalii vilivyopo pamoja na maliasili.

Kutokana na agizo hilo, alisema katika maonyesho ya mwaka ujao, hatarajii kuona Tawa na Tanapa zikishiriki pekee kama ilivyotokea kwa mwaka huu.

Katika hatua nyingine, Kanyasu aliwataka wananchi wa Tanga ambao walikuwa wakiendesha maisha yao kwa kusafirisha baadhi ya wanyamapori hai wakiwamo vipepeo, wabuni mbinu zingine za kibiashara ili kuwavutia watalii kuja nchini kuona wanyama hao badala ya kuwapelekea huko waliko.

Alisema msimamo wa serikali upo pale pale wa kuhakikisha utalii unalindwa kwa kuhakikisha hakuna wanyamapori wanaosafirishwa kupelekwa nje ya nchi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigella, alisema Tanga imejaliwa kuwa na vivutio vingi vya utalii ambavyo kupitia maonyesho hayo vitajulikana kwa watu wengi, hivyo kuchagiza maendeleo ya mkoa na taifa kwa ujumla.

Alisema ushirikiano ambao mkoa unaoupata kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, unasaidia kutangaza vivutio vya utalii yakiwamo mapango ya Amboni, magofu ya kale na utalii wa fukwe, hivyo kuwezesha kuwavutia watalii wa ndani na nje ya nchi kutembelea Tanga.


## TANZANIA PORTS AUTHORITY

### BANDARI COLLEGE – DAR ES SALAAM

### LOCATED AT MAHUNDA STREET, TANDIKA

**P.O. Box 9184, Tel: (+255)22 2850970,Fax (+255)22 213938,**
**E-mail:pbc@ports.go.tz**

## APPLICATION FOR ADMISSION TO THE BANDARI COLLEGE FOR THE ACADEMIC YEAR 2019/2020; THE SEPTEMBER 2019 INTAKE

Applications are invited for admission into the following programmes at Bandari College (BC) for the academic year **2019/2020, the September 2019 intake.** The applications are open for Ordinary Diploma and Basic Technician Certificate programmes. An option for the evening session will be considered where possible.

1. **BASIC TECHNICIAN CERTIFICATES (NTA LEVEL 4)**

| S/N | COURSE | DURATION |
|---|---|---|
| 1 | BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE IN SHIPPING AND PORT MANAGEMENT | I YEAR |
| 2 | BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE IN FREIGHT CLEARING, FORWARDING AND PORT MANAGEMENT | |
| 3 | BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE IN ENGINEERING AND MAINTENANCE MANAGEMENT | |
| 4 | BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE IN LOGISTICS AND TRANSPORT MANAGEMENT | |
| 5 | BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE IN BUSINESS ADMINISTRATION | |
| 6 | BASIC TECHNICIAN CERTIFICATE IN INFORMATION COMMUNICATION AND TECHNOLOGY | |

2. **ORDINARY DIPLOMA PROGRAMMES (NTA LEVEL 5 & 6)**

| S/N | COURSE | DUR ATION |
|---|---|---|
| 1 | ORDINARY DIPLOMA IN SHIPPING AND PORT MANAGEMENT | 2 YEARS |
| 2 | ORDINARY DIPLOMA IN FREIGHT CLEARING, FORWARDING AND PORT MANAGEMENT | |
| 3 | ORDINARY DIPLOMA IN ENGINEERING AND MAINTENANCE MANAGEMENT | |
| 4 | ORDINARY DIPLOMA IN LOGISTICS AND TRANSPORT MANAGEMENT | |
| 5 | ORDINARY DIPLOMA IN BUSINESS ADMINISTRATION | |
| 6 | ORDINARY DIPLOMA IN INFORMATION COMMUNICATION AND TECHNOLOGY | |

**C. ENTRY REQUIREMENTS:**

a) Entry qualifications for the Ordinary Diploma (NTA 5 to NTA 6) are a form six certificate with at least one principal and a subsidiary pass (excluding religious subjects) OR a form four certificate with at least four passes (excluding religious subjects) and a Basic Technician Certificate (NTA level 4) in the related discipline obtained from a recognized Institution or College. The Engineering and Maintenance Management Course requires Form Four passes in Mathematics, Physics or Chemistry.

b) Entry qualification for the Basic Technician Certificate (NTA 4) is a form four certificate with at least four passes (excluding religious subjects). The Engineering and Maintenance Management Course requires passes in Mathematics, Physics or Chemistry.

**D. MODE OF APPLICATIONS**

1. Candidates who wish to appl y for admission in any of the courses can collect application forms from the Bandari College Admission Office at its Campus in Dar es Salaam. Application forms can also be downloaded from the Bandari College website: www.bandari.ac.tz

2. All applicants for admission into Basic Technician Certificates (NTA 4) and Ordinary Diploma (NTA 5 to NTA 6) courses are required to pay an application fee of **TZS. 10,000/-** (for Tanzanians) and **TZS. 30,000/-** (for international candidates). Dully filled application forms must be returned while attached with a non-refundable application fee pay slip (original). All application fees should be paid by using control number issued at the College by Finance office through the GEPG System.

3. Applicants should return the application forms on or before **20th August, 2019**

**For more information please contact**

**Principal**
**Bandari College- Dar es Salaam**
**Mahunda Street, Mwembeyanga, Tandika**
**P.O. Box 9184, Dar es Salaam, Tanzania**
**Tel: (+255)22 2850970, Fax (+255)22 213938,**
**E-mail: pbc@ports.go.tz**
**Website: www.bandari.ac.tz**

215258402

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wawakilishi wa Tanzania Caf sajilini kwa umakini

**KWA** mara ya kwanza katika soka la Tanzania, katika msimu mpya wa 2019/2020, Tanzania Bara itawakilishwa na timu nne kwenye michuano ya kimataifa, mbili Ligi ya Mabingwa na mbili Kombe la Shirikisho Afrika.

Tayari Shirikisho la Soka Afrika (Caf), limethibitisha kuwapo kwa nafasi hizo na kulitaka Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuhakikisha hadi mwishoni mwa mwezi huu linasajili timu zake zitakazoshiriki mashindano hayo kupitia mtandoa (CMS).

Na kwa mujibu wa Kanuni za Ligi Kuu zilizofanyiwa marekebisho na Kamati ya Utendaji ya TFF baada ya kupatikana nafasi hizo nne, timu zitakazoiwakilisha Tanzania Bara ni Simba na Yanga kwenye Ligi ya Mabingwa, huku Azam FC na KMC zikipeperusha bendera ya nchi katika Kombe la Shirikisho.

Ikumbukwe kupatikana kwa nafasi hizo nne kutoka mbili za awali, kumetokana na mafanikio makubwa ya Klabu ya Simba baada ya kufanikiwa kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa kabla ya kutolewa na TP Mazembe katika msimu huu uliomalizika wa 2018/19.

Kufika kwa Simba katika hatua hiyo kuliiwezesha Tanzania Bara kuvuna pointi 15, hivyo ukichanganya na pointi tatu ambazo zilipatikana kwa kipindi cha misimu mitatu iliyopita wakati Yanga ikishiriki michuano hiyo, ilifanya Tanzania kuwa na jumla ya pointi 18.

Kwa mantiki hiyo, Tanzania Bara ikafanikiwa kuwa timu ya 12 kwa ubora, huku ikizipita Ivory Coast (pointi 15) na Kenya (pointi 14) iliyokuwa ikitegemea mafanikio ya Gor Mahia kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho ambayo nayo iliishia hatua ya robo fainali.

Aidha, ikumbukwe pia nafasi hizo nne si za kudumu, kwani ikitokea katika michuano ya msimu ujao wa 2019/20 nchi nyingine klabu yake/zake zikafanya vizuri na kuvuna pointi zaidi, moja kwa moja Tanzania Bara itapoteza nafasi hizo na kurejea kwenye mbili za awali.

Pointi hizo hutolewa kadri klabu za nchi shiriki kwenye michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu Afrika, zinavyofanya vizuri kusonga mbele.

Kinachotakiwa sasa ni Simba, Yanga, Azam FC na KMC kuhakikisha zinajipanga vizuri kuelekea michuano hiyo ili kuweza kuongeza pointi zaidi ili Tanzania Bara iendelee kupata nafasi hizo nne.

Na katika hilo, Nipashe tunaishukuru Caf kwa kuijulisha TFF mapema kuongezeka kwa nafasi hizo kwani kunatoa nafasi chanya kwa klabu kujiandaa mapema hususan kipindi hiki cha dirisha la usajili.

Kinachotakiwa kwa wawakilishi wetu hao ni kuhakikisha wanafanya usajili makini kulingana na mashindano hayo ya kimataifa yaliyopo mbele yao na si vinginevyo.

Hatutarajii kuona moja ya wawakilishi wetu katika michuano hiyo akifanya usajili kwa kuita wachezaji kwa ajili ya majaribio kwanza, bali usajili unaotakiwa ni wa nyota ambao tayari walishawachunguza wakicheza na waliokidhi viwango kulingana na mapendekezo ya makocha.


Lengo na matarajio yetu ni kuona wawakilishi wetu wote kwanza wanafika hatua ya makundi na kisha robo fainali na hatimaye nusu na kucheza fainali.

Hilo likifanikiwa hakika Tanzania Bara itakuwa imejiongezea pointi na kuwa na uhakika wa kuingizia timu nne msimu unaofuata wa 2020/2021, kwani pointi nyingi huanza kutolewa katika hatua hizo.

Tunaamini hilo linawezekana kama maandalizi yataanza sasa kwa kusajili wachezaji wenye viwango vya hali ya juu, lakini pia wazoefu wa mechi za kimataifa, huku uboreshwaji wa mabenchi ya ufundi ya klabu hizo ukizingatiwa pia. Kila la Kheri Simba, Yanga, Azam na KMC katika dirisha la usajili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mkude, Ajibu wasiwe fimbo ya kumchapia Amunike Stars

Na Adam Fungamwango

**NIMEKUWA** nikisikiliza habari za michezo kwenye redio, kusoma mitandao ya kijamii na hata kusikiliza mijadala kwenye vijiwe na kwenye meza mbalimbali za kuuzia magazeti juu ya kuachwa kwa wachezaji vipenzi vya mashabiki wa soka nchini, Ibrahim Ajibu wa Yanga na Jonas Mkude wa Simba katika kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars.

Wachezaji hao wameachwa kwenye mchujo wa mwisho wa wachezaji waliokwenda nchini Misri kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019.

Kwa vyovyote itakavyokuwa kama wachezaji hao wameachwa kwa sababu hawakufanya vema mazoezini, wavivu wa mazoezi, au watovu wa nidhamu, lakini ni kocha mwenyewe Emmanuel Amunike ndiye anayefahamu.

Baba ndiye anayejua tabia za watoto wake. Kuna mwingine hamtumi kabisa dukani kwa sababu ana tabia ya kupoteza pesa au kuchelewa kurudi. Mwingine anateuliwa kula na wageni, mwingine haruhusiwi kabisa hata kukaa nao, akiwasalimu tu inatosha. Kama kawaida ya Wabongo, tayari watu wameshaanza kulalamika ni kwa nini wachezaji hao wameachwa.

Baadhi wanaaminishwa na wenzao kuwa wangekuwapo wachezaji hao basi Taifa Stars ndiyo itafanya vizuri kutokana na uwezo wao waliouonyesha kwenye Ligi Kuu wakiwa na klabu zao.

**Baadhi wanaaminishwa na wenzao kuwa wangekuwapo wachezaji hao basi Taifa Stars ndiyo itafanya vizuri kutokana na uwezo wao waliouonyesha kwenye Ligi Kuu wakiwa na klabu zao.**

Kukosekana kwa wachezaji hao, basi imejengeka imani kuwa Taifa Stars haitofanya vizuri, licha ya kwamba wachezaji hao wamekuwa wakichaguliwa kwenye kikOosi hicho na kuondoka, lakini hakuna kipya sana au cha ajabu sana kilichofanywa nao.

Hivi sasa baadhi ya mashabiki wamekuwa wakilalamika chinichini, lakini wengi wanasubiri Stars iondolewe kwenye michuano hiyo ili wampe makavu Amunike.

Ina maana kwa sasa Amunike angalau aombee kikosi hicho kifuzu kwenye makundi kwa kutinga 16-bora, lakini kama kikishindwa kuongoza kundi lake au kwenye nafasi ya pili, basi kazi anayo.

Ukiliangalia Kundi C ambalo Taifa Stars ipo, zipo timu za Kenya, Senegal na Algeria, kiuhalisia pamoja na kwamba mpira unadunda na chochote kinaweza kutokea, lakini wachambuzi wa masuala ya soka hawaipi nafasi Stars kufuzu kwenye kundi hilo.

Kiuhalisia hata kama Tanzania haikufuzu kwenye kundi hilo, haiwezekani kabisa lawama atupiwe Amunike kwa sababu zozote zile, ikiwamo hata kuwaacha Mkude na Ajibu, bali ni kwamba ilikuwa kwenye kundi gumu.

Sasa kuna baadhi ya mashabiki wanaonekana kutaka kutumia kigezo hicho kumlaumu na kumshambulia Amunike kwa kuwaacha Ajibu na Mkude endapo timu itafanya vibaya.

Mimi nina uhakika kuwa Stars inaweza kufanya vizuri au vibaya kwa jinsi tu itakavyojipanga na si kwa sababu ya uwapo au kutokuwapo kwa Ajibu na Mkude.

Ifike wakati mashabiki wa soka wasiwe na ushabiki na baadhi ya wachezaji, bali wawe mashabiki wa timu ya taifa, na pia hata kama timu ikitokea imetolewa basi itafutwe sababu ya kitaalamu na si kwa sababu eti Ajibu na Mkude hawakuwapo.

## BARUA/MJADALA

### *Mabondeni hakutufai wananchi, tuhame kama tunavyoelekezwa*

**Mhariri habari za majukumu**

*NIMEJITOKEZA kama raia mwema wa taifa hili kutoa mchango wangu katika eneo ambalo ni la msingi katika ustawi wa Watanzania, kwa sababu linagusa shughuli zao za kila siku kwa njia moja au nyingine.*

*Ninasikitika kwamba ni eneo ambalo miaka nenda miaka rudi, limekuwa likipigiwa kelele na watu wengi wenye mapenzi mema na hasa nyakati za masika ama za vipindi vya mvua nyingi kama vinavyoendelea katika Jiji la Dar es Salaam.*

*Lakini si kwa jiji tu la Dar es Salaam, pia kwa maeneo karibu yote ya ukanda wa Pwani kwa maana ya Tanga, mkoa wa Pwani wenyewe, Lindi na Mtwara na kwa mujibu wa vyombo vya habari, ni karibu nchi nzima. Nimejitokeza kuzungumzia tatizo moja ambalo linagusa mambo mawili kwa maana ya usalama wa watu, lakini pia afya zao.*

*Tatizo hili linawahusu watu wanaoendelea kuishi maeneo ya mabondeni ambao ndio waathirika wakuu. Ni waathirika wakuu wa madhara yatokanayo na wingi wa mvua za masika ama zinazoletwa na mabadiliko ya tabianchi kama ilivyojitokeza sasa kufuatia mvua ambayo imenyesha kwa takribani siku ya nane sasa. Mhariri kwa mfano mingi kwa mfano katika jiji la Dar es Salaam, watu wanaoishi katika Bonde la Mto Msimbazi, yale ya Magomeni, Jangwani, Mkwajuni, na Kigogo wameaswa kuyahama maeneo hayo. Wameaswa kuhama maeneo hayo kutokana na ukweli kuwa mafuriko ambayo yamekuwa yakijitokeza si kwamba yameleta athari za vifo kwa wanaong'ang'ania kuendelea kuishi katika maeneo hayo, bali pia athari za kiafya na mali zao.*

*Mbali na vifo, baadhi ya watu wamepoteza vifaa vya ndani, lakini mwishowe wamekumbwa na magonjwa ya milipuko kama vile kipindupindu, pamoja na malaria.*

*Magonjwa ya kipindupindu kwa sehemu kubwa huyakumba maeneo haya kutokana na tatizo lingine la wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, ambao baadhi yao hutumia kipindi hiki kufungulia maji ya vyooni wakiyaelekeza kwenye bonde hilo.*

*Wakati umefika sasa Mhariri kwa Watanzania na hasa wanaoishi maeneo ya mabondeni kurejesha fahamu zao katika mstari na hivyo kuhama kwenye maeneo hayo kama ambavyo serikali imekuwa ikielekeza kwa muda mrefu na wapenda maendeleo wengine. Hiyo ni kwa ustawi si wa waathirika peke yao, bali pia kuokoa rasilimali za nchi zinazotumika kuwahudumia wanapokumbwa na majanga hayo.*

**Yasinta Simoni, Dar**

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# KMC inastahili kimataifa, Lipuli ikubali tu yaishe




**Na Adam Fungamwango**

UMEZUKA mjadala mkubwa juu ya KMC kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa badala ya Lipuli FC.

Baadhi ya watu wanadai kuwa Lipuli ndiyo ilistahili kucheza mechi za kimataifa kwa sababu ilifanikiwa kufika fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF), maarufu kama Kombe la FA.

Nimewasikia hata baadhi ya viongozi wa Lipuli wakilalamika kuwa wao ndiyo waliostahili nafasi ya kucheza mechi za kimataifa badala ya KMC, inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni.

Wakasema wataiandikia barua ili kuulizia suala hilo na pia kuangalia uwezekano na wa kucheza badala ya KMC. Kabla ya kuendelea na mjadala huu, kwanza tuangalie jinsi nafasi hiyo ilivyopatikana.

Ni kwamba hakuna klabu yoyote iliyokuwa ikiota ndoto hii. Ligi Kuu ilikuwa imemalizika.

Ghafla, Shirikisho la Soka Afrika (Caf), likaitaarifu TFF kuwa kuanzia msimu ujao Tanzania Bara inatakiwa iwe na timu nne kwenye michuano ya kimataifa badala ya mbili.

Hii inatokana na Simba kufanya vema kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa iliyomalizika hivi karibuni, ambapo ilifika hatua ya robo fainali na kuifanya Tanzania kuvuna pointi 15 hivyo ukichanganya na alama tatu ilizovuna Yanga misimu mitatu iliyopita kufikisha pointi 18 na kuzipiku Ivory Coast (pointi 15) na Kenya (pointi 14).

Ilichofanya TFF ni kuzichukua timu mbili za kwanza za juu kutoka kwenye Ligi Kuu ambazo ni Simba na Yanga kwa ajili ya kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika. Mshindi wa tatu naye ilibidi aende moja kwa moja kucheza Kombe la Shirikisho Afrika, lakini kwa bahati nafasi hiyo ilichukuliwa na Azam FC ambayo ni hiyo hiyo iliyotwaa Kombe la FA linaloipa nafasi ya kucheza kombe hilo.

Kwa sababu Azam ilikuwa na sifa pande zote mbili, ikatolewa nafasi kwa mshindi wa nne ili ashiriki michuano hiyo. Kwa maana hiyo Simba na Yanga watacheza Ligi ya Mabingwa na Azam na KMC Kombe la Shirikisho.

Lipuli ilikuwa inataka nafasi hiyo kwa sababu tu eti imefika fainali ya Kombe la FA. Ina maana inataka kuilazimisha TFF ibadilishe kanuni zake na kuwa wacheza fainali ya Kombe la FA wote wawili ndiyo wataiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

TFF ikifanya hivyo, basi kutakuwa hakuna tena msisimko kwenye mechi ya fainali kwa sababu timu zote zinakuwa zimeshafuzu. Hapo ni kuua heshima na umuhimu wa fainali.

Ili thamani ya fainali ibakie pale pale, inapaswa timu moja tu ndiyo icheze Kombe la Shirikisho Afrika ili timu zipambane kutafuta ushindi na si kucheza tu mradi fainali wakati tayari timu zote zimeshafuzu.

Lipuli pamoja na kufika fainali ya FA, ilijichanganya yenyewe kwenye baadhi ya mechi za Ligi Kuu na kuonekana kama haikutilia maanani. Ilifungwa kizembe mabao 3-0 dhidi ya Mbeya City tena ikiwa nyumbani, lakini haikuchezesha wachezaji tegemeo kwenye mechi dhidi ya Biashara ya Mara na kunyukwa mabao 2-0. Mechi hizi pekee zingeiwezesha Lipuli kufikisha poiti 55 ambazo ni sawa na za KMC. Inawezekana pia kuna baadhi ya mechi za Ligi Kuu ambazo haikuzitilia maanani, na kama ingefanya hivyo ingeweza kuwa kwenye nafasi ya nne na kuiwakilisha nchini, na malalamiko haya yote yasingekuwapo.

KMC inastahili kucheza Shirikisho kwa sababu pamoja na kwamba ndiyo kwanza imepanda kwenye Ligi Kuu, lakini ilionekana kuwa ni timu isiyokuwa na mzaha kwenye mechi zote inazocheza.

Haikukamia mechi kama baadhi ya timu zikicheza na Simba na Yanga, badala yake mechi zote yenyewe ilicheza kwa nguvu ile ile.

Ilifika wakati timu hiyo ilikuwa ina pointi ambazo haziishushi daraja na iko pazuri kwenye msimamo wa Ligi, lakini pia haikuwa na pointi za kuipa ubingwa, ila ilikuwa ikicheza kana kwamba kuna kitu inatafuta na kuendelea kushinda mechi zake bila kujali haishuki daraja na haichukui ubingwa.

Hii ndiyo zawadi pekee ya KMC ambayo inatakiwa ipewe kwa kupambana ikiwa haijui nini itapata, lakini Mungu amewaangazia.

Kuna baadhi ya timu tena za siku nyingi kwenye ligi, zikishakuwa na pointi nyingi kwenye ligi na hazishuki na pia pointi ilizonazo haziwezi kuzipa ubingwa, basi zinaanza kupoteza mechi kwa namna ya ajabu kiasi cha baadhi ya mashabiki kuhisi kama wanauza mechi.

Kwa hili lililotokea kwa KMC sasa liwe somo kwa timu zote za Ligi Kuu, kupambana kuanzia mechi ya kwanza hadi ya mwisho kutafuta ushindi na si kuangalia baadhi ya mechi tu.

Nafasi za kuwakilisha nchi kwa sasa zimeongezeka, hivyo timu zipambane kuisaka hata nafasi ya nne kwa sababu chochote kinaweza kutokea, mwenye nafasi ya tatu akatwaa FA wa nne akaenda kimataifa. Kupambana na kuziona mechi zote ni sawa kumeibeba KMC, hivyo Lipuli na timu nyingine liwe somo kwao msimu ujao zipambane kuingia nne bora.

## KABWELA

## NA FADHIL MOHAMMED






# Chungu, tamu bajeti serikali awamu ya tano

**INATOKA UK. 4**

nikaendelea na kuendelea."

Mtaalamu huyo wa uchumi alibainisha kuwa serikali ya awamu ya nne ilikuwa inakusanya wastani wa Sh. bilioni 850 kwa mwezi, lakini tangu serikali ya awamu ya tano iingie madarakani Novemba 5, 2015, imekuwa ikikusanya wastani wa Sh. trilioni 1.3 kwa mwezi.

"Kwa hiyo, ni rahisi sana kuhesabu hicho kinachoingia mfukoni, lakini ni muhimu kuangalia kinachotoka, zinatoka zinakwenda kwenye nini? "Ulipaji wa Deni la Taifa inategemea, kwa mwezi inaweza ikatoka Sh. bilioni 600, tumewahi kwenda mpaka Sh. bilioni 900 kutegemeana na madeni hayo yanaiva wakati gani.

"Mwezi huu unaweza ukalipa Sh. bilioni 600 na kidogo, mwezi ujao ukalipa Sh. bilioni 700, ni kwa sababu ya tofauti ya ile mikopo inaiva wakati gani.

"Ukichukua wastani wa Sh. bilioni 550 mishahara, ukaongeza Sh. bilioni 600 kwa ajili ya kulipia Deni la Taifa, tayari Sh. trilioni 1.1 umeitumia kwa hivyo vitu viwili ambavyo huwezi kuvikwepa," Dk. Mpango alisema.

Mtiririko wa fedha za mradi ya maendeleo ya baadhi ya wizara kwa kipindi cha robo tatu ya kila mwaka wa fedha kuanzia 2015/16 hadi 2018/19.

**NINI KIFANYIKE**

Nipashe ilizungumza na Waziri Kivuli wa Fedha na Mipango, Halima Mdee, kuhusu changamoto hiyo na alisema kuwa ili kukabiliana na utekelezaji duni wa bajeti ya maendeleo, serikali inapaswa kuruhusu taasisi za nje kuja kufanya tathmini ya kifedha (credit rating).

Mdee ambaye pia ni Mbunge wa Kawe (Chadema), alisema anaamini kwa kuruhusu taasisi huru kufanya tathmini ya kifedha nchini, kutaisaidia Tanzania kupata mikopo yenye riba nafuu badala ya mikopo ya masharti magumu ya kibiashara inayopewa kwa sasa.

"Kwa hali ilivyo sasa, ninaona kuna haja kuruhusu taasisi huru zije kutufanyia 'credit rating' ili itusaidie kama taifa kujua deni letu halisi likoje," Mdee alisema na kuongeza: "Kwa kutofanyiwa credit rating, benki nyingi za kimataifa zenye mikopo ya riba nafuu zitaendelea kuogopa kutukopesha kwa sababu hazina uhakika kama tutalipa au la. Matokeo yake tutaendelea kukopa kwa masharti magumu ya kibiashara."

Mdee pia alisema ipo haja kufanya marekebisho katika Sheria ya Deni la Taifa kwa kuwa ina miaka zaidi ya 40 tangu kutungwa kwake pasi na kufanyiwa marekebisho.

Waziri kivuli huyo pia alisema kuwa kutokana na kupaa kwa Deni la Taifa, serikali sasa inapaswa kuwa makini zaidi katika ukopaji mpya, akisisitiza kuwa inapaswa kukopa kutekeleza miradi ambayo ina uhakika itarejesha fedha.

"Sheria yenyewe ya Deni la Taifa imepitwa na wakati. Ni sheria ya miaka ya 1970. Hoja yetu hapa ni kwamba; tuwe na sheria inayoitaka serikali kukopa pale tu inapotaka kutekeleza miradi yenye uhakika wa kurejesha fedha na kulipa deni," alisema.

| Mwaka | Wizara | Zilizotengwa | Zilizopokewa | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 2015/16 | Elimu | Bil. 582.67/- | Bil. 360.9/- | 61% |
| 2016/17 | Elimu | Bil. 897.658/- | Bil. 500.4/- | 55% |
| 2017/18 | Elimu | Bil. 916.841/- | Bil. 594.6/- | 65% |
| 2015/16 | Kilimo | Bil. 32/- | Bil. 5.1 | 15% |
| 2016/17 | Kilimo | Bil. 101.527/- | Bil. 3.369/- | 3.32% |
| 2017/18 | Kilimo | Bil. 150.253/- | Bil. 27.231/- | 18% |
| 2018/19 | Kilimo | Bil. 98.119/- | Bil. 41.222/- | 42% |
| 2015/16 | Mifugo | Bil. 19.4/- | 0 | 0% |
| 2016/17 | Mifugo | Bil. 15.873 | Bil. 1.252/- | 7.9% |
| 2017/18 | Mifugo | Bil. 4/- | 0 | 0% |
| 2018/19 | Mifugo | Bil. 12127/- | Bil. 6.186/- | 51% |
| 2015/16 | Utalii | Bil. 7.709/- | Bil. 1/- | 12.9% |
| 2016/17 | Utalii | Bil. 17.747/- | Mil. 156.69/- | 8% |
| 2017/18 | Utalii | Bil. 51.8/- | Bil. 27.9/- | 53.9% |
| 2015/16 | Katiba | Bil. 15.381/- | Bil. 13.209/- | 85% |
| 2016/17 | Katiba | Bil. 37.459/- | Bil. 3.523/- | 9% |
| 2015/16 | Habari | Bil. 3/- | Bil. 1/- | 33.3% |
| 2016/17 | Habari | Bil. 3/- | Mil. 190.32/- | 6.3% |
| 2017/18 | Habari | Bil. 6.32/- | Bil. 4.358/- | 69% |
| 2015/16 | Ndani | Bil. 79.689/- | Bil. 4.626/- | 5.8% |
| 2016/17 | Ndani | Bil. 47.923/- | Bil. 13/- | 28% |
| 2017/18 | Ndani | Bil. 40.008/- | Bil. 21.8/- | 54% |
| 2016/17 | Fedha | Bil. 791.998/- | Bil. 18.898/- | 2.3% |
| 2017/18 | Fedha | Trl. 1.429/- | Bil. 81.257/- | 5.7% |
| 2018/19 | Fedha | Tril. 1.295/- | Bil. 20.678/- | 1.6% |

**CHANZO: Taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge**

Wakati Mdee akishauri hayo, Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, anaona kuna haja Bunge liunde kamati maalum ili kufanya ukaguzi wa Deni la Taifa.

Wakati wa mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2019/20 bungeni jijini Dodoma Jumatatu iliyopita, Zitto alimwomba Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuunda kamati kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa deni hilo, akidai takwimu zinazotolewa hivi sasa si sahihi.

Kiongozi huyo wa ACT-Wazalendo alisema usimamizi wa deni hilo ni tatizo, akiwataka wabunge kutazama ripoti za Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka miwili iliyopita.

"Kwa sababu takwimu za sasa hivi siyo sahihi, mimi hapa nimesoma ripoti mbili za CAG; ya mwaka jana na ya mwaka huu, inaonyesha kuna tatizo kubwa sana katika utunzaji wa kumbukumbu.

"Nakuomba Mheshimiwa Spika, uruhusu ukaguzi maalum ili tuweze kujua tunadaiwa nini na tunadaiwa na nani kwa sababu inawezekana kuna madeni hewa," Zitto alisema.

# Vigogo TRA waingia mikononi Takukuru

**INATOKA UK. 2**

nzuri ya kukujibu kesho," alisema.

Akizungumza kwenye mkutano huo uliofanyika Ijumaa iliyopita, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema mfanyabiashara huyo mizigo yake ilishikiliwa na TRA kwa muda wa miaka mitatu baada ya kukataa kutoa rushwa ya Sh. milioni mbili.

Majaliwa alisema mfanyabiashara huyo alikamatwa mwaka 2016/2017 na mzigo wake ulirudishwa juzi kwa sababu aliyekamata aliomba rushwa na yeye alikataa kutoa.

"Huyu mfanyabiashara alikataa kutoa rushwa na alikubali bora mzigo wake ukae huko huko, siku alipokuja kueleza nashukuru kamishna wa kodi ya ndani ambaye ni mgeni TRA nilipomwagiza amshughulikie, alitekeleza na siku ya pili alisema ni kweli mfanyabiashara huyo ameonewa, tukaagiza arudishiwe mzigo, tabia hii kamishna wa TRA ipo huko ndani," alisema.

Aliongeza: "Walipomkamata alikataa kutoa rushwa usiku aliokamatwa, alisema fedha ninayo ipo nyumbani, wakamsindikiza hadi Kariakoo nyumbani kwake, walipofika yule mfanyabiashara aliwaambia rushwa hatoi wakitaka wamuue. "Kwa bahati nzuri kulikuwa na polisi waliokuwa kwenye doria, wakaangalia kuna nini wakaona kuna mgogoro nadhani wana bohari, walipompeleka, mzigo wake umekaa miaka mitatu amerudishiwa mwaka huu mwezi wa nne."

# Meli mpya kunufaisha Kanda ya Ziwa

**INATOKA UK. 3**

Alisema kwa sasa bandari hiyo ambayo inahudumia visiwa viwili vya Kerebe na Gozba, haina meli ya abiria bali wanategemea boti kwa ajili ya usafiri.

"Zamani kulikuwa na meli mbili za mizigo, lakini sasa kuna meli tano kubwa zinazoingia kwa mwezi mizigo mbalimbali ikiwamo vifaa vya dukani wa tani 200 mkubwa ukiingizwa na Kiwanda cha Kagera Sugar ambao ni tani 3,500," alisema.

Kwa upande wake, nahodha wa meli ya MV Luxury II, Peter Hiza, alisema anapata huduma nzuri ikiwamo kupakia na kushusha mzigo kwa wakati muafaka. Alisema meli yake imeingia ubia na Kampuni ya Bia ya Tanzania (TBL) kutoa na kupeleka Bukoba kutoka Mwanza.

"Tunatumia bandari za serikali kutokana na gharama za kawaida na huwa nakuja Bukoba mara mbili kwa mwezi kuleta mzigo," alisema.

Naye Mwakilishi wa Kagera Sugar, Shamsa Mohammed, alisema meli mpya kubwa kwa sababu kuna unafuu mkubwa katika usafiri wa njia ya maji kuliko barabara katika kusafirisha sukari. "Tani tunazosafirisha kutoka Bukoba kwenda mikoa mingine tunatumia meli kwa sababu ina gharama nafuu na inafika salama," alisema.

## JPM atajwa kubadili mfumo wa uongozi

**INATOKA UK. 2**

Alihoji kama asingetembelea shule hiyo, asingebaini matatizo yanayowakabili ikiwamo upungufu wa madarasa na madawati licha ya kutatuliwa kwa tatizo la ofisi za walimu kwa kujengwa jengo la kisasa.

Jengo hilo lenye uwezo wa kukaa walimu 60 pamoja na ofisi ya mwalimu mkuu limegharimu zaidi ya Sh. milioni 200.

Katika hatua nyingine, Makonda aliwataka wabunge wa mkoa wa Dar es Salaam nao kufanya ziara na kutatua kero za wananchi katika maeneo yao.

"Kama nimetafuta ufadhili nimejenga majengo haya, basi na wao wahangaike kuleta madawati, lakini wakisubiri uchaguzi (wa mwaka 2020), mimi nikiwapo wahesabu maumivu," alisema Makonda.

Alisema kuna baadhi ya wabunge ambao wamekuwa wakijiona wanashughulikia kitaifa lakini majimboni hawaonekani ili kusikiliza kero za wananchi badala yake wanasubiri wakapige kelele bungeni na kujirekodi.

Makonda alisema shule hiyo inakabiliwa na changamoto kwa kuwa walimu wako 47 idadi ambayo ni ndogo ikilinganishwa na wanafunzi 3,700 ambao wanakabiliwa na upungufu wa madawati, matundu ya vyoo na madarasa, hali ambayo ingeweza kuwa vikwazo kwa walimu kutofanya vizuri.

"Lakini nyie mmeweza vikwazo mkatanguliza upendo, utu na kiapo chenu hatimaye Vijibweni inafanya vizuri katika ngazi ya mkoa na taifa. Nawapongeza kwa moyo huo, naamini mtaendelea kufanya vizuri zaidi ifike hatua watu washangae jambo jema linafanyika Vijibweni," alisema.

"Najua mnazishinda baadhi ya shule ambazo ziko katikati ya mji, lakini nyie Vijibweni mmefanya vizuri," aliongeza.

Alitoa wito kwa wazazi na viongozi wa wilaya na manispaa kuona umuhimu wa kushirikiana kuhakikisha samani za viwango zinapatikana kwa ajili ya ofisi ili kuweka mazingira mazuri.

Shule hiyo inatajwa kuwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 64, wakati vilivyopo sasa ni 18, madawati ni 853 wakati mahitaji ni 1,254, matundu ya vyoo kwa wavulana yapo 13 badala ya 62 na kwa wasichana yapo 16, huku mahitaji yakiwa 79.

Meneja Kampuni ya CRJE (East Africa) ya China, Bai Hao Chen, alisema wamejenga jengo hilo kama mchango kwa jamii na ishara ya urafiki kati ya China na Tanzania.

Chen alisema CRJE ni kampuni ya ujenzi ya kimataifa yenye vitengo mbalimbali vya ujenzi duniani kote na kwa hapa nchini, baadi ya miradi iliyojenga ni pamoja na daraja la Kigamboni (Daraja la Mwalimu Nyerere), Jengo la Bunge Dodoma, RITA Tower na Uhuru Tower, Dar es Salaam.

Alisema ofisi hiyo ya walimu itasaidia kupanua na kuboresha kiwango cha elimu katika kanda na kutoa fursa zaidi kwa wanafunzi kupata elimu bora.

Aliahidi kuwa kampuni hiyo itaendelea kutoa misaada kwa jamii nchini kwa imani kwamba michango hiyo itasaidia kupatikana kwa idadi kubwa ya wasomi na kudumisha urafiki kati ya nchi hizo mbili.

Meya wa Manispaa ya Kigamboni, Maabadi Hoja, alisema kulingana na hadhi ya ofisi ilivyo wanapaswa kujipanga kuhakikisha samani nazo zinapatikana kulingana na mazingira yalivyo.

"Tutakaa kama halmashauri au kama wilaya, hii ofisi kama inavyoonekana nzuri siyo ya kuweka samani zinazolingana na hadhi yake, naamini tutajipanga vizuri kufanikisha hilo," alisema.

# Makandarasi wapewa kibano ujenzi stendi

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKUU wa Wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu, Festo Kiswaga, ametoa miezi miwili kwa makandarasi wa kampuni za Kings Builders na Harlem Consultancy kuhakikisha wanakamilisha ujenzi wa mradi wa stendi ya mabasi Somanda na barabara yenye urefu wa kilomita 1.5 uliotarajiwa kukamilika mwezi uliopita. Mradi huo wa kuimarisha miundombinu mijini (ULGSP) ambao unatekelezwa katika miji sita na manispaa 12 nchini umeanza kuwa mwiba kwa Halmashauri ya Mji wa Bariadi kutokana na makandarasi wa mradi huo kushindwa kukamilisha kwa wakati.

Akikagua mradi huo, Kiswaga alisema ametoa miezi miwili kwa makandarasi hao kuhakikisha wanakamilisha ujenzi kabla ya Agosti 8, mwaka huu na kama watashindwa kufanya, hivyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao. Alisema yeye kama msimamizi mkuu wa miradi ya maendeleo katika wilaya, hawezi kukaa kimya akiona utekelezaji wa miradi hiyo unakiuka utaratibu na mikataba iliyowekwa. "Mradi huu ni mkubwa na hadi kukamilika kwake utagharimu kiasi cha Sh. bilioni 7.2, hivyo sitakubali kuona unaharibiwa wala kucheleweshwa.

Naye Mratibu wa mradi huo ambaye pia ni Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) Wilaya ya Bariadi, Mhandisi Mathias Mugorozi, alisema umefikia asilimia 68 na kwamba utakapokamilika utaleta manufaa kwa wananchi wa Mji wa Bariadi na Tanzania kwa ujumla sambamba na kuiwezesha halmashauri kukusanya mapato.

Jeams Silaga, mfanyabiashara ndogo katika stendi ya zamani ya Somanda, alisema kuchelewa kwa stendi hiyo kunawanyima fursa ya kufanya shughuli zao za biashara.

Naye msimamizi wa kampuni hizo, Charles Lyamuya, alisema wako tayari kutekeleza agizo la Mkuu wa Wilaya.




Mkurugenzi Mtendaji msaidizi wa Kampuni ya Data Vision International, William Kihula (wa pili kutoka kushoto), Bwigane Mulinda, Meneja wa Maendeleo ya Biashara wa kampuni hiyo (wa pili kutoka kulia) wakiwa na baadhi ya washiriki kwenye utoaji tuzo za X-Prize, Los Angeles, Marekani. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni ya Tanzania yashiriki utoaji tuzo kimataifa Marekani

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya kitanzania ya Data Vision International inayojishughulisha na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), utafiti na mifumo ya malipo ya kielektroniki, imeshiriki utoaji tuzo za kimataifa za 'Global Learning X-Prize' zilizofanyika hivi karibuni jijini Los Angeles nchini Marekani.

Washindi waliotengeneza mfumo (app) bora zaidi wa kumsaidia mtoto kujua kusoma, kuandika na kuhesabu bila msaada wa mwalimu walizawadiwa dola za Marekani 10 milioni.

Ushiriki wa Data Vision International katika utoaji tuzo, katika hafla hiyo iliyofanyika Mei 15, 2019, ulitokana na ushiriki wake, kwa kushirikiana na Kampuni ya RTI ya Marekani, kufanya utafiti kwa kutumia programu tano zilizochaguliwa kutoka miongoni mwa kampuni zaidi ya 400 kutoka nchi mbalimbali duniani zilizoshiriki katika shindano hilo.

Mradi wa utafiti ulishirikisha watoto 3,000 wenye umri kati ya miaka 7 hadi 10 kutoka wilaya sita za Mkoa wa Tanga. Kupitia utafiti huo uliofanyika mwaka 2017, watoto hao walipewa 'tablets' zenye programu (software) maalum inayowasaidia kujifunza wenyewe bila kusaidiwa na mtu yeyote.

Taasisi ya X-Prize, yenye makao yake makuu Marekani, iliyoandaa na kuratibu mashindano hayo, iliyatangaza kampuni mbili kuwa zimeshinda zote kwa kulingana alama.

Kampuni hizo ni Kitkit School kutoka Korea Kusini na Onebillion kutoka Uingereza. Hivyo, kampuni husika ziligawana dola milioni 10 kwa lengo la kuwasaidia kuendeleza utengenezaji wa programu zao kwa ufanisi zaidi.

Taasisi ya X-Prize ilisema kupitia tovuti yao kuwa asilimia 90 ya watoto walioshiriki katika utafiti huo nchini walikuwa hawawezi kusoma hata neno moja la Kiswahili. Lakini, baada ya kutumia kwa miezi 15 moja kati ya programu zilizoshinda, nusu ya watoto hao walikuwa wanaweza kusoma baadhi ya maneno ya Kiswahili.

Mkurugenzi Mtendaji Msaidizi wa Kampuni ya Data Vision International, William Kihula, ambaye alishiriki na kupewa nafasi ya kuzungumza katika hafla ya utoaji wa tuzo hizo akiambatana na Bwigane Mulinda, Meneja wa Maendeleo ya Biashara wa kampuni hiyo, alisema:

"Ushiriki wetu kwenye zoezi hili linaloleta mapinduzi ya utoaji elimu ya awali duniani kwa kutumia teknolojia kukabiliana na uhaba wa walimu unatokana na ufanisi wa kazi zetu kwa kipindi cha miaka 20. Hii, ni heshima kwa taifa letu na serikali yetu kwa jinsi ilivyoweka mazingira mazuri ya kuhuisha maendeleo ya teknolojia katika kutatua matatizo ya kijamii."

"Dunia imeangalia Tanzania kama kitovu cha mapinduzi ya teknolojia hii muhimu katika kumsaidia mtoto kujua kusoma, kuandika na kuhesabu bila kuingia darasani," Kihula aliongeza.

Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni Duniani (UNESCO), zaidi ya watoto milioni 250 duniani kote hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu, huku kukiwa na upungufu mkubwa wa walimu wa elimu ya msingi na sekondari. Utafiti wa shirika hilo unaonyesha kuwa walimu milioni 68.8 wanapaswa kuajiriwa ili kila mtoto mwenye umri husika apate elimu ya msingi na sekondari kufikia mwaka 2030.

"Hili ni tatizo ambalo ni lazima tulitatue. Tunaweza kutumia nguvu ya teknlojia ili watoto kila mahali duniani bila kujali hali zao wanapata fursa ya kujenga maisha yao na kwa ajili yetu sote," alisema Dk. Emily Church, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya X-Prize.

# Matatani tuhuma wizi vifaa Tanesco

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma linawashikilia watu watatu katika matukio mawili tofauti likiwamo la wizi wa vifaa vya umeme vinavyomilikiwa na Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kupita Mradi wa Umeme Vijijini (REA) vyenye thamani ya Sh. 9,120,000.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Marwa Maigwa, aliwataja watuhumiwa hao ni Godfrey Ndiu 32, mkazi wa Lizaboni Manispaa ya Songea, Emmanuel Komba, mkazi wa Mfaranyaki Manispaa ya Songea na Kassimu Zuberi, mkazi wa kijiji cha Likuyusekamaganga wilayani Namtumbo.

Alifafanua zaidi kuwa tukio la kwanza lilitokea Juni 2 katika kijiji cha Nakahuga Kata ya Litisha Wilaya ya Songea Vijijini, ambapo Jeshi la Polisi lilipokea taarifa ya kuibwa kwa vifaa vya umeme ambavyo ni polymelk 36 , bolt pamoja na nuts 60 mali ya Tanesco vyenye thamani ya Sh. 9,120,000.

Alieleza zaidi kuwa vifaa hivyo ambavyo vilikuwa vinasimamiwa na kampuni ya mkandarasi Namis Corporate Ltd pamoja na makandarasi wa kujenga miundombinu ya umeme wa REA kwa laini ya eneo la Maposeni na Nakahuga.

Alisema Jeshi la Polisi baada ya kupata taarifa hiyo askari walifanya msako mkali na kuwakamata Godfrey Ndiu na Emmanue Komba, na kuwa katika mahojiano na walikiri kuiba vifaa hivyo na baadaye walikwenda kuonyesha mali hizo ambazo zilikuwa zimefichwa nyumbani kwa James, ambaye alikimbia na kutokomea kusikojulikana baada ya kuona askari.

HABARI KITAIFA

# Taasisi ya kimataifa kujenga kiwanda cha kahawa nchini

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

TAASISI ya kimataifa ya Josephat Torner Foundation of Europe (JTFE), imeunga kwa vitendo jitihada za serikali kwa kuanzisha mpango mkakati wa kufungua kiwanda cha kahawa mkoani Simiyu.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Mwanza, Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Josephat Torner, alisema taratibu za uanzishwaji wa kiwanda hicho ambacho kinategemewa kuajiri asilimia kubwa ya watu wenye ualbino zimeshaanza na kwamba ifikapo Juni mwaka 2020 ujenzi utakuwa umefikia hatua ya kuridhisha.

Torner alieleza mafanikio ya asasi hiyo ambayo ni kupungua kwa matukio ya utekaji na mauaji ya watu wenye ualbino, uwapo wa sera na mkakati, uwapo wa sheria ya watu wenye ualbino ya mwaka 2010 pamoja na serikali kuanza kuwarejesha watoto wenye ualbino kujumuika na familia zao kutoka katika makazi ya muda.

"Tunaiunga mkono serikali ya awamu ya tano katika kulinda na kutetea haki za binadamu, mazingira ya afya na elimu na kwa kuonyesha hilo tumeanza mpango wa kujenga kiwanda cha kahawa Simiyu, kupanda miti na kuhimiza usitishwaji wa matumizi ya mifuko ya plastiki ili kulinda afya ya mazingira, mimea pamoja na viumbe," alisema Torner.

Mwenyekiti wa chama cha watu wenye ualbino Mkoa wa Mwanza, Alfredy Kapole, alisema serikali imejikita katika kutoa elimu kwa watu namna gani mtoto mwenye ualbino anaweza kutokea jambo lililochangia kupungua kwa matukio ya mauaji ya watu wenye ualbino.

"Serikali pamoja na asasi kwa pamoja wamefanya juhudi za kutoa elimu, watoto wenye ualbino sasa wameanza kutambua haki zao za msingi na wanaonyesha juhudi kubwa katika masomo, zaidi ya watoto 300 wenye ualbino wanasomeshwa na mashirika mbalimbali," alisema Kapole.

Bennet Phunyanya, kutoka taasisi ya watu wenye ualbino Malawi, alisema watu wenye ualbino waliopo katika nchi za Afrika wanapata changamoto mbalimbali katika jamii inayowazunguka na kwamba ujio wao Tanzania ni kujifunza jinsi serikali, jamii na watu wenye ualbino wanavyoishi.



Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo (wa pili kushoto), akipokea maelezo juu ya mradi wa maji unaondelea wilayani Kisarawe mkoani Pwani, toka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu Dawasa, Mhandisi Cyprian Luhemeja. Wilaya ya Kisarawe inategemea kuanza kupata huduma ya maji ya Dawasa mapema mwisho wa mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bakwata yajitosa vita dhidi ya ndoa utotoni

**Na Dege Masoli,** TANGA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), limeridhia kampeni ya kupinga ndoa za utotoni, huku ikisimamia mambo tisa iliyodai ndiyo misingi, mwongozo, kanuni na sheria ya dini hiyo.

Hayo yalielezwa na Katibu wa Mufti wa Tanzania, Abuubakar Zuber, Shekhe Mussa Hemed Bin Jumaa, wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye kikao kilichoandaliwa na Shirika la World Vision. Shekhe Mussa alieleza kuwa Baraza la Maulamaa limeridhia kampeni inayoendeshwa na shirika hilo kwa kuzingatia mambo tisa ambayo ndiyo muongozo ulioachwa na Mtume Muhamad S.A.W kwa Waislamu kote duniani.

Mambo tisa kwa mujibu wa Shekhe Mussa ni kuzingatia kuwa ndoa ni moja ya nguzo muhimu sana kwa wanadamu na pili ni kutambua na kuikubali ndoa iliyopatikana kwa maridhiano kati ya wanandoa wenyewe.

Kuhusu umri, alisema Uislamu haukuweka umri stahiki kwa mtoto wa kike kuolewa, lakini unazingatia afya njema, utayari wa kuolewa na awe na akili timamu.

Jambo la nne ni kuwapo kwa mamlaka ya wazazi ya kumuozesha mtoto wa kike, lakini awe ametimiza vigezo kwa mujibu wa taratibu na maelekezo ya dini, huku jambo la tano ni mtoto aliyeolewa kuwa na haki ya kuvunja ndoa hiyo kwa kupitia kadhi kama ataona haikulinda haki yake.

Shekhe Mussa alisema jambo la sita la kuzingatiwa ni mtoto wa kike kuwa na haki ya kulinda maslahi yake ya utoto kama ilivyo kwa mtoto wa kiume na saba uislamu unatambua kuwa ndoa ni mkataba mzito, hivyo anayeingia ni lazima awe na uelewa wa kutosha kuhusu suala hilo.

Mkurugenzi wa miradi wa World Vision Tanzania, Dk. Kasilima Yosh, alieleza kuwa kampeni ya kuondoa ndoa za utotoni chini ya kaulimbiu yake ya 'Kumaliza ndoa ya utotoni ni jukumu la kila Mtanzania' imeshirikisha makundi mbalimbali ya kijamii na ya kidini.

Kwa upande wa Bakwata, Dk. Yosh alisema wameamua kushirikisha baraza hilo kwenye kampeni hiyo lengo likiwa ni kuona namna njema ya kufanikisha zoezi hilo ili kuinusuru jamii hiyo na changamoto ya ndoa za utotoni, na kwamba hatua hiyo itasaidia kuwanusuru watoto dhidi ya majanga hayo.

"Tumekuwa na ushirikiano mkubwa na Bakwata katika kuwaokoa watoto na ndoa za utotoni, hivyo kuwafanya kufikia ndoto zao na mradi huu sambamba na Bakwata, lakini tunashirikiana pia na taasisi nyingine kwenye kampeni hii," alisema Dk. Yosh.

Hata hivyo, aliomba viongozi wa kidini nchini kusaidia kampeni ya kupambana na mimba za utotoni inayoendeshwa na shirika hilo ili kufanikisha lengo la kuwaokoa katika athari zinazolikumba kundi hilo.

# Mkaa endelevu waleta fursa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WANANCHI wa vijiji 22, ambao ni wazalishaji mkaa maarufu kama mkaa endelevu na halmashauri za wilaya nchini wamenufaika kwa kupata fedha zaidi ya Sh. bilioni tatu kufuatia mauzo ya mkaa endelevu katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2014 mradi ulipoanza kuvunwa.

Hayo yalisemwa na Meneja Mradi wa kuleta mageuzi katika sekta ya mkaa Tanzania (TTCS, Leonard Charles, wakati akiwasilisha mada kwa maofisa mbalimbali kutoka Tamisemi na Serikali Kuu waliokutana mkoani Morogoro.

Charles alisema, mradi wa TTCS unatekelezwa katika vijiji 30 vya wilaya za Mvomero, Kilosa na Morogoro chini ya usimamizi wa Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Mtandao wa Jamii wa Kusimamia Misitu Tanzania (Mjukita), Shirika la Kuendeleza Nishati Asili Tanzania (TaTEDO) na kufadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Uswisi (SDC).

Alisema katika mradi huo vijiji 22 vimeanza kunufaika kiuchumi na utunzaji wa mazingira, huku nane vikiwa katika mchakato.

Alisema hadi kufikia Mei 2019, vijiji hivyo vimekusanya mapato halali zaidi ya Sh. bilioni 1.4, wazalishaji mkaa Sh. bilioni 1.2 na halmashauri Sh. milioni 500.


Alitaja baadhi ya vijiji ambavyo vimenufaika na mradi ni Ulaya Mbuyuni, Matuli, Kitunduweta, Mlilingwa, Ulaya Kibaoni, Diguzi na vingine.

Aidha, Leonard alisema mradi wa mkaa endelevu ulianza Machi 2012 katika vijiji 10, lakini baada ya kuonesha mafanikio wamelazimika kuongeza vijiji hadi kufika 30.

Alisema mafanikio ya mradi yamezingatia kutoa elimu kwa jamii husika, watendaji na wafanya maamuzi hivyo kurahisisha utekelezaji.

Meneja pia alisema utekelezaji wa mradi huo unazingatia uwapo wa mpango wa matumizi bora ya ardhi za vijiji, kutenga maeneo madogo ya mradi na kuvuna kwa kutumia vitalu.

Alisema pia mradi umefanikisha ujenzi wa ofisi za vijiji hali ambayo inarahisisha usimamizi wa mradi sambamba na ujenzi wa vyumba vya madarasa, kuweka huduma za maji ili kuleta maendeleo kwenye vijiji husika.



# CCM Arusha yakaribisha wanachama kugombea

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha, kimetaka wanachama wenye sifa, kujitokeza kuwania nafasi za uongozi zilizo wazi kwa sababu mbalimbali.

Katibu wa CCM Mkoa wa Arusha, Mussa Matoroka, alisema zoezi la kuchukua fomu lilianza juzi hadi leo.

Matoroka alisema nafasi zilizo wazi ni Katibu Mwenezi wa Mkoa, baada ya aliyekuwa anashikilia nafasi hiyo, Shaban Mdoe kuteuliwa kuwa Katibu wa CCM wa Wilaya ya Meru na baadaye kuhamishiwa Wilaya ya Rombo.

Nyingine ni nafasi ya Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa, baada ya mwenyekiti wake, Dk. John Palangyo kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Arumeru Mashariki.

Naye Katibu wa Umoja wa Vijana (UVCCM) Mkoa wa Arusha, Jamal Abbas Khimji, alisema uchaguzi wa kujaza nafasi ya mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Saitoti Zelote ambaye aliteuliwa kuwa Katibu Tarafa ya Mbulu Mbulu wilayani Karatu nao utafanyika sambamba na wa viongozi wengine.

Khimji aliwataka wanachama wa jumuiya hiyo wenye sifa, ikiwamo kuwa na kadi ya umoja huo, kadi ya CCM na awe na umri usizidi umri wa miaka 30 kujitokeza kuchukua fomu za kugombea.

Aidha, Khimji alisema zoezi la utoaji fomu likikamilika, watasubiri uteuzi wa vikao vya juu na tarehe ya uchaguzi itatangazwa na Kamati Kuu ya CCM Taifa.

Mmoja wa waliokuwa wagombea nafasi ya Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi mkoani hapa, Fadhili Maganya, alisema anakusudia kuchukua fomu kugombea nafasi ya mwenyekiti wa jumuiya hiyo.



Baadhi ya wafanyakazi wa TBL Arusha, wakishiriki katika zoezi la upandaji miti katika Shule ya Sekondari Muriet iliyopo jijini humo, mwishoni mwa wiki, katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, ambapo walipanda zaidi ya miti 1,000 katika shule hiyo na chanzo cha maji kilichopo Mtaa wa Kambarage, Kata ya Themi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kiongozi Mwenge aiagiza Takukuru

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

KIONGOZI wa mbio za Mwenge kitaifa, Mzee Mkongea Ally, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Wilaya ya Longido mkoani Arusha, kufuatilia na kukagua taarifa za mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Simba uliogharimu Sh. bilioni 15 fedha za serikali kuu ili kujiridhisha.

Aliyasema hayo alipotembelea mradi huo na kubaini kuna taarifa tatu ambazo zinaonyesha kupishana, huku zikidai baadhi ya taarifa kutokukamilika.

Alisema walichobaini katika mradi huo ni tangi kubwa la kuhifadhi maji lenye ujazo wa lita 400,000 kuwa linavuja, lakini kwa kuwa bado lipo kwenye kipindi cha majaribio, alimtaka mkandarasi kurekebisha.

Alifafanua kuwa kumeonekana kupishana kwa taarifa ya mkoa inayodai kuwa mradi huo umegharimu Sh. bilioni 15, huku taarifa ya wilaya ikionyesha kugharimu Sh. bilioni 10.

"Awali taarifa za wilaya zinaonyesha kuandikwa Sh. bilioni 15, lakini mmekata hapa kwa kutumia kalamu na kuandika Sh.bilioni 10," alisema.

"Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, naomba tumkabidhi mkuu wa Takukuru afuatilie jambo hili, na nina toa wiki mbili taarifa kamili za mradi huu zipatikane," alisema.

"Naomba niseme endapo itabainika kuna ubadhirifu wa fedha katika mradi huu, naomba sheria ichukue mkondo wake," alisisitiza.

# Magari ya umeme yaanza kutumika hifadhini

**Na Novatus Makunga,** ARUSHA

MAGARI yanayotumia nguvu ya umeme yameanza kutumika kwa ajili ya kusafirishia watalii katika hifadhi za taifa zilizoko katika ukanda wa kaskazini baada ya kubadilishwa kutoka katika mfumo wa kutumia mafuta ya dizeli na petroli.

Hayo yamebainika katika maonyesho makubwa ya utalii katika eneo la Afrika ya Mashariki yanayofahamika kama Karibu-Kili Far yaliyomalizika jana mjini hapa.

Ukanda wa utalii wa kaskazini unaundwa na hifadhi ya taifa ya Arusha, Kilimanjaro, Ziwa Manyara, Serengeti, Tarangire na Mkomazi pamoja na Mamlaka ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro (NCAA). Akikagua mabanda mbalimbali ya utalii, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alielezwa na Mwenyekiti wa mradi unaobadilisha mfumo wa magari na kuweka wa umeme wa E-Mission Afrika, Satbir Hanspaul, kwamba magari hayo ni rafiki kwa mazingira ya mbuga za wanyamapori. "Lazima tuungane na serikali pamoja na wadau wengine katika kuhakikisha tunalinda na kutunza mazingira huko porini katika hifadhi zetu za taifa," alisema.

Hanspaul alisema matumizi ya mfumo wa umeme unayafanya magari yasitoe moshi au gesi zinazochangia ongezeko la joto duniani ikiwamo hewa ya ukaa na ambazo ni hatari kwa mazingira.

Aidha, alisema kuwa faida nyingine ya magari hayo ni kutokuwa na kelele na hivyo kuleta utulivu na ustawi mkubwa wa wanyamapori katika hifadhi za taifa.

Alisema baada ya kuchaji vizuri, gari inauwezo wa kwenda kilometa 180 kwa mwendokasi wa zaidi ya kilometa 100 kwa saa moja. "Hii ni teknolojia mpya ambayo ni nafuu kuliko ya kutumia diseli au petroli kwa kuwa baada ya kuibadilisha gari hakuna gharama kubwa na hata kulifanyia gari matengenezo baada ya kwenda umbali fulani, haitahitaji mambo mengi na utaweza kudumu nayo kwa miaka zaidi ya 20," alisema.

Hanspaul alisema wanaangalia uwezekano wa kuwa na vituo vya kuchajia umeme hasa kwenye vituo mbalimbali vya kujaza mafuta ya magari hasa kwa kuanzia katika maeneo ya hifadhi za taifa za ukanda wa kaskazini.

Alisema kwa upande wa msaada ya kiufundi, tayari wameweka vituo vya uhakika katika maeneo mbalimbali aliyoyataja kuwa ni Hifadhi ya taifa ya Ziwa Manyara na Hifadhi ya Serengeti katika eneo la Seronera lilipo kaskazini mwa hifadhi hiyo, katika eneo la Kogatende na kusini katika eneo la Ndutu.

Hanspaul alisema mfumo huo umekuwa na mafanikio makubwa kwa injini ya gari aina ya Landcruiser, huku akifafanua wapo katika hatua ya mwisho kwa injini ya magari aina ya Landrover.

Hata hivyo Hanspaul alieleza hivi sasa wanayafanyia kazi magari yote ambayo yana injini inayozungusha magurudumu yote ambayo ndiyo kwa kawaida usafirisha watalii kwenda mbugani.

Alisema kuwa baada ya kukamilisha kubadilisha injini ya magari makubwa ya utalii wataingia katika magari ya kawaida yanayotumiwa mijini kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

Watumiaji wa awali wa magari hayo wanaeleza yana mfumo wa kuhifadhi nguvu ya umeme wa aina tatu, ambapo wa kwanza una uwezo wa umeme kwa saa nane, wa pili saa nne na wa tatu ukiwa na uwezo wa kuhifadhi umeme kwa saa mbili na robo.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Utalii ya Equtorial, Roman Chuwa, alisema matumizi ya mfumo wa umeme unaweza kuwa nafuu zaidi endapo baadhi ya maeneo yataweza kuwa na mfumo wa kuyajaza umeme magari hayo unaotumia nishati ya jua.

Naye Naibu Kamishna wa Uhifadhi na Maendeleo wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), William Mwakilema, alisema kuingia kwa teknolojia ya magari ya aina hiyo ni mapinduzi makubwa ya uhifadhi kwa kupunguza hewa ya ukaa inayotokana na moshi wa magari.

Mradi wa E-Mission Afrika unatekelezwa na kampuni ya maarufu nchini kwa kurefusha bodi ya magari ya utalii ya Hanspaul Automechs Limited kwa kushirikiana na Gadgetronix Limited yote ya jijini Arusha.



# Huduma msaada wa kisheria zasogezwa kwa tasnia habari

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HUDUMA za msaada wa kisheria ambazo hutolewa na wasaidizi wa sheria zaidi ya 3,000 nchini, sasa zitasogezwa kwa wanatasnia ya habari ili kutambua na kutathmini masuala yanayoikumba jamii katika haki na usawa.

Mratibu wa mpango huo anayeshughulikia vyombo vya habari, Neville Meena, kutoka Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), alisema huduma hiyo itaanza kupelekwa kwa wanataaluma ya habari wa mikoa minne ya Kanda ya Kaskazini ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga.

"Tunashirikiana na Shirika la Legal Services Facility (LSF) ambalo linatoa ruzuku kwa asasi zinazoshughulika na upatikanaji wa huduma za msaada wa sheria kwa lengo la kuwawezesha wananchi maskini kupata haki zao," alisema Meena.

"Shirika hili linafanya kazi zake katika wilaya na halmashauri 170 Tanzania Bara na Zanzibar. Wanawezesha Watanzania kupata huduma za msaada wa kisheria bure kupitia watoa huduma za msaada wa kisheria wajulikanao kama Paralegals."

Pia wanatoa elimu juu ya masuala ya sheria na kuwajengea uwezo wananchi kutambua haki zao pamoja na kutatua changamoto zinazoikumba jamii hasa wanawake, watoto na watoto wa kike katika kupata haki ya elimu, kurithi mali pamoja na kushika nafasi za uongozi.

Alisema ili kuwa na ufanisi katika masuala ya haki za binadamu na upatikanaji wa huduma za msaada wa kisheria, LSF imeona ni muhimu kufanya kazi na wadau mbalimbali wakiwamo waandishi wa habari.

Akieleza zaidi kwa nini LSF wameelekeza nguvu zaidi katika tasnia ya habari nchini, Meena alisema mchango wa wanahabari katika kufikia jamii na kupaza sauti umekuwa chachu ya mabadiliko na maboresho mengi katika nyanja mbalimbali na ustawi wa jamii kwa ujumla.

Kazi ya kuwajengea uwezo wanataaluma hao kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini itaanza rasmi Juni 11, mwaka huu, ambapo LSF itatoa elimu ya jinsi kuelekeza jinsi ya kuripoti habari za mambo ya kisheria, namna bora ya kuandika habari za kijamii na wajibu wa waandishi wa habari katika kuelimisha jamii juu ya haki zao na uwajibikaji wa viongozi wa serikali.

Pia wanataaluma hai wataangazia huduma za msaada wa kisheria na kazi zinazofanywa na wasaidizi wa kisheria, kutambua na kutathmini masuala yanayoikumba jamii katika haki



Kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa 2019, Mkongea Ali, akimkabidhi mama mjamzito Monika Gabriel chandarua kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa malaria, wakati alipokuwa akiweka jiwe la msingi katika chumba cha kuhifadhia maiti Hospitali ya Wilaya Patandi mkoani Arusha. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Waanza tahadhari kunusuru mifugo dhidi ya magonjwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WANANCHI wa Kata ya Uru Kusini katika Jimbo la Moshi Vijijini, wameanza kuchukua tahadhari ya kuikinga mifugo yao na maambukizi ya ugonjwa kimeta kwa kuchanja mifugo 3,856.

Diwani wa Kata hiyo, Wakili Wilhard Kitali, alieleza kuwa wameanza uhamasishaji wa juu ya umuhimu wa kuchanja mifugo kuzuia magonjwa mbalimbali.

Alikuwa akitoa taarifa kuhusu zoezi hilo katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kilichofanyika siku chache zilizopita.

"Ni kweli tumeshachanja ng'ombe 1,768, kondoo na mbuzi 1,567 na nguruwe 521 kwa ajili ya kuzuia magonjwa mbalimbali ikiwamo kimeta na zoezi bado linaendelea," alisema.

Aidha, uongozi wa kata hiyo umesema kazi nyingine zinazofanyika kwa umakini mkubwa ni pamoja na ukaguzi wa nyama na kukusanya ushuru wa ukaguzi.

Diwani Kitali alisema pia kuwa wafugaji 725 wanaendelea kupewa elimu juu ya ufugaji, kuchanja mifugo na kuotesha malisho.

"Yapo mambo ambayo tunadhani ni muhimu wananchi wa eneo hili wakapata mwanga wa elimu kwa mfano elimu juu ukamuaji wa maziwa na usindikaji," alisisitiza Kitali.

Kata ya Uru Kusini inaundwa na vijiji saba na vitongoji 20 vyenye kaya 5,926 zenye idadi ya watu 22,904.

# Ujenzi kituo afya kuanza

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SERIKALI katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, imepanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa kituo cha afya cha heshima kitakachopewa jina la cha Rais John Magufuli kutokana na mchango wake katika uboreshaji wa sekta ya afya.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amesema mchakato wa ujenzi wa kituo hicho umeiva na utagharimu zaidi ya Sh. milioni 500.

"Mpaka sasa tumeshakusanya zaidi ya Sh. milioni 260 za kuanza utekelezaji wa mradi huo. Tunategemea kiasi cha Sh. milioni 366 kuzipata kutoka katika vyama vya ushirika," alisema Ole Sabaya.

Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Hai, Dk. Getrude Anthony, akizungumzia mpango huo alisema utasaidia kuboresha huduma za afya kwa wananchi wa mjini wanaotegemea huduma katika hospitali ya wilaya.

Aidha, Idara ya Afya katika Halmashauri ya Wilaya hiyo, imethibitisha kuwa bado hamasa ya wananchi kuchangia damu kwa ajili ya kuokoa maisha ya wagonjwa iko chini na kwamba mpaka sasa hawajaweza kufikia asilimia 20 ya kiwango kinachohitajika.

"Uhitaji wa damu salama katika Hospitali yetu ya Wilaya ya Hai ni uniti 10 kwa siku na kwa mwezi ni uniti 30, lakini bado hatujafikia hata asilimia 20 ya kiwango kinachotakiwa. Tunaomba Watanzania wengine kujitokeza kuchangia damu ili kuokoa maisha ya wenzetu," alisema.

Kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama (NBTS), uchangiaji wa damu kwa hiari, una faida kwa mtoaji kwa vile unapunguza hatari ya magonjwa ya moyo, kuwapo kwa madini chuma mengi kupita kiasi katika damu kunakodhoofisha utendaji kazi na kuchangia damu mara kwa mara, hurekebisha madini chuma ya ziada katika mfumo wa damu.

Faida nyingine ni upimaji wa afya pasipo gharama kwa sababu wakati unapochangia damu mtaalamu wa tiba, daktari au muuguzi atapima shinikizo la damu yako, mapigo ya moyo na kukufanyia vipimo vya afya bure.

Kabla ya kuanza kwa uchangiaji huo wa damu salama, Kaimu Shekhe wa mkoa wa Kilimanjaro, Shaban Mlewa, alisema zoezi hilo kwao ni sehemu muhimu ya huduma za jamii na linakwenda sambamba na msaada wao walioutoa kwa wagonjwa ikiwamo sabuni na magodoro yenye thamani ya Sh. milioni 2.4.

Nipashe
Spotika



KIKOSI BORA LIGI KUU 2018/2019 HIKI HAPA UK.18



## ISIKUPITE

KWENYE mechi ya fainali ya Kombe la Europa League dhidi ya Arsenal, Chelsea ilianzisha kikosi cha kwanza kikiwa hakina mchezaji hata mmoja mzawa wa England, hiyo ikiwa ni timu ya kwanza katika mechi ya fainali ya michuano ya Uefa kikosi cha kwanza kutokuwa na mchezaji mzawa wa klabu ya nchi husika tangu Inter Milan ilipocheza dhidi ya Bayern Munich katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2010.

# JUU KWA JUU...

Beki wa Ufaransa, Ferland Mendy (kushoto), akiwahi na kuucheza mpira kwa kichwa dhidi ya kiungo wa Uturuki, Cengiz Under wakati wa mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 iliyopigwa Konya, Uturuki na wenyeji hao kushinda 2-0. HABARI UK. 15. **PICHA: MTANDAO**

# MADOGO WA5 MUHIMU ARSENAL MSIMU UJAO




Ainsley Maitland - Niles kazini.

**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Arsenal kwa sasa ipo katikati ya muda muhimu wa mpito. Kuondoka kwa Arsene Wenger ambaye aliitoa klabu hiyo kwenye shida na sasa ipo kwenye mchakato wa kujengwa upya. Mfaransa huyo alikuwa hapo kwa zaidi ya miaka 22 na alitekeleza falsafa yake katika kila nyanja ya klabu hiyo. Kila njia klabu hiyo ilifanya kazi ni ya Wenger, sasa hawana chaguo bali kufanya mambo tofauti.

Unai Emery alichaguliwa kuwa kocha mpya kipindi cha majira ya joto na alionekana kuwa mkombozi mpya na ahadi ya kuwa kichocheo cha mabadiliko katika bodi.

Hata hivyo, kushindwa kwa klabu hiyo kupata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, inamaanisha kuwa sasa wana bajeti ya uhamisho wa wachezaji wapya kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chao.

Kwa mafanikio yoyote klabu hiyo inatakiwa kuwajengea uwezo vijana wake. Akademi ya Arsenal ni moja ya akademi bora zaidi Ulaya na imekuwa ikizalisha wachezaji wengi kwenye Ligi Kuu tano za Ulaya.

Kwa sasa klabu hiyo inalazimika kutafuta wachezaji wake vijana na kama klabu hiyo ikiwa na nafasi iweze kuwapandisha kwenye timu ya wakubwa. Hapa tunawaangalia wachezaji watano vijana ambao wanaweza kuwa msaada kwa kikosi hicho...

**5. Eddie Nketiah**

Eddie, Eddie, Eddie, zilikuwa ni shangwe za mashabiki wa pale dimba la Emirates siku ambayo Eddie Nketiah alipojitangaza mwenyewe kuwa ni mtu muhimu kwa kikosi cha 'Washika Bunduki' hao alipofunga mabao mawili kwenye mchezo wa Kombe la Ligi dhidi ya Norwich.

Usiku ule ndio ulikuwa muda mzuri kwa mashabiki wa Arsenal walipoonyesha mapenzi yao kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, na kuonyesha kuibeba klabu kwenye mabega yake. Ulikuwa ni wakati wa kuvutia kwa mchezaji huyo kijana ambaye amekuwa na timu hiyo tangu akiwa na umri wa miaka 15, akifunga mabao yake kwa mara ya kwanza kwa kikosi cha timu ya wakubwa.

Na tangu wakati huo Eddie Nketiah ameonekana kuwa kwenye mapenzi makubwa na klabu hiyo, kwa sasa akiwa kwenye umri wake wa miaka 19, amekuwa akifanya kazi ya ziada kwenye kila muda anaopewa nafasi. Anaonekana kuwa kwenye ubora zaidi na wengine wanamtaja kama Ian Wright mpya.

Wote Pierre-Emerick Aubameyang na Alexandre Lacazette wakiwa kwenye ubora wao, lakini umri wao unakimbia wakiwa na miaka 28 na 29. Hiyo inamaanisha kwamba Eddie Nketiah anaweza kuwa mchezaji muhimu zaidi kwa washika bunduki hao.

**4. Lucas Torreira**

Arsenal ilimsajili Lucas Torreira kwa ada ya pauni milioni 26 kipindi cha majira ya joto kilichopita, baada ya kuonyesha kiwango bora kwenye Kombe la Dunia. Ujio wake ulikuwa muhimu kwa mafanikio ya timu. Katika umri wake wa miaka 23, anaonekana kuwa na nyota nzuri zaidi na kocha, Emery amekuwa akimuanzisha kwenye kikosi chake cha kwanza.

Tangu siku za Gilberto Silva zilivyomalizika pale Arsenal kumekuwa hakuna kiungo mwingine mkabaji ambaye ana mfano wake. Lakini kwa ujio wa mchezaji huyu wa kimataifa wa Uruguay inaonyesha wazi kwamba, ndiye mrithi wake sahihi. Katika umri wake wa miaka 24, ana nafasi kubwa zaidi ya kuisaidia Arsenal katika siku za usoni.

**3. Matteo Guendouzi**

Kutoka kwenye Ligi Daraja la Pili nchini Ufaransa hadi kwenye fainali ya Kombe la Ligi ya Europa, Matteo Guendouzi amepata uzoefu wa kutosha kwa kipindi cha miezi 13 iliyopita. Katika umri wake wa miaka 19 alisajiliwa kwa pauni milioni nane, lakini sasa thamani yake ni kubwa zaidi.

Sasa ana umri wa miaka 20 na ni wazi kwamba ni mchezaji ambaye anaonekana kuwa na matarajio makubwa zaidi kwa kikosi cha Arsenal na Emery amemwanzisha katika mechi 23 za Ligi Kuu.

**2. Ainsley Maitland-Niles**

Arsenal wanamwelezea Ainsley Maitland-Niles kama ni mmoja wa 'watoto' wao, kwa sababu amekuwa katika klabu hiyo tangu akiwa na umri wa miaka sita. Yeye ni zao la akademi ya Hale End, alisaini mkataba wake wa kwanza mwaka 2014.

Tangu utoto wake, Maitland-Niles ameonekana kuwa ni mchezaji mwenye kipaji cha ukweli. Kuna wakati alipelekwa kwa mkopo pale Ipswich kabla ya Arsene Wenger kuamua kumpa mkataba. Na sasa Emery ameonyesha kuwa na imani kubwa na uwezo wa 'dogo' huyo.

Kwa kawaida yeye anacheza kama kiungo wa kati na baada ya kuumia kwa Hector Bellerin yeye alikuwa akichezeshwa kama beki wa kulia. Kwa msimu wote, mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 22 ameonyesha kuwa anaweza kupewa mikoba kamili ya kuibeba klabu hiyo.

Huku Aaron Ramsey akiwa amekwenda kuanza maisha mapya pale Juventus, Arsenal sasa inaweza kumtumia mchezaji huyo kama mbadala wake.

**1. Rob Holding**

Kuna mjadala kwamba, Rob Holding ulikuwa moja ya usajili bora zaidi kuwahi kufanywa na Wenger. Washika Bunduki hao walimsajili kwa pauni milioni mbili mwaka 2016, kitu ambacho hakiwezi kufanyika katika soko la sasa.

Kitu cha kushangaza kwa Rob Holding ni kwamba katika umri wake wa miaka 23, anacheza kama mtu mwenye umri wa miaka 32. Ana uwezo mkubwa dimbani.

Hivyo kwa namna yoyote anaonekana kuwa mchezaji muhimu zaidi kwa kikosi hicho kwa msimu unaokuja na atakuwa mchezaji muhimu zaidi kwa Arsenal kama akiendelea kupewa nafasi na majukumu yake dimbani.

**JE, WAJUA?**



Liverpool imekuwa timu ya kwanza kutwaa ubingwa wa Ulaya, huku ikiwa imemiliki mpira kwa asilimia chache zaidi (35.4%) ya mpinzani wake (Spurs), tangu Jose Mourinho alipoiongiza Inter Milan kuichapa Bayern Munich katika fainali ya michuano hiyo mwaka 2010.

# MICHEZO


Ajibu na jezi yake

# NYOTA WA BONGO WALIOKO SOKONI

**Na Adam Fungamwango**

INGAWA kuna baadhi ya klabu zimeshaanza usajili kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu, ni mchezaji mmoja tu wa Kitanzania ndiye amesajiliwa rasmi kutoka timu moja kwenda nyingine. Mtanzania huyo pekee ambaye ametangazwa rasmi kusajiliwa ni Abdulaziz Makame kutoka Zanzibar aliyetua Yanga.

Yanga tayari imeshawatangaza rasmi Patrick Sibomana na Issa Bigirimana kutoka APR ya Rwanda, huku ikimuongezea mkataba mwingine wa kuitumikia klabu hiyo, Mkongoman Papy Tshishimbi. Klabu ya Namungo nayo imetangaza kumsajili straika wa Alliance FC raia wa Rwanda, Bigirimana Blaise kwa ajili ya msimu ujao wa ligi.

Hapo utaona kuwa wachezaji waliotangazwa rasmi kusajiliwa na klabu za Ligi Kuu wengi ni wa kigeni, lakini ni mmoja tu wa Kibongo. Pamoja na hayo wachezaji wengi wa Kibongo kwa sasa wapo sokoni na wamekuwa wakiwindwa na klabu mbalimbali kubwa na ndogo.

Wachezaji wengi wanaowindwa ni wale walioonekana kufanya vema kwenye Ligi Kuu msimu uliomalizika, lakini kumekuwa na ukimya sana, baadhi ya wachezaji walisubiri mpaka fainali za Afcon zimalizike, wengine wanadaiwa kusajili kimya kimya na kusubiri tu tarehe ya mikataba yao ya awali imalizike, huku baadhi wakiangalia ofa gani iko juu zaidi, wapo pia wanaoangalia sehemu ambayo wanaona wakienda watapata namba na si kukaa benchi.

Hawa ni baadhi ya wachezaji wanaowindwa kwa sasa na klabu mbalimbali za Ligi Kuu na kuna asilimia kubwa wasiwapo kwenye klabu zao walizokuwa wakizitumikia msimu uliomalizika.

**1. Benno Kakolanya- Yanga**
Kwa muda mrefu alikuwa na mgogoro na klabu yake ya Yanga kiasi cha kujiondoa, lakini pia baadaye Kocha Mkuu Mwinyi Zahera kumchukulia kama kirusi anayeweza kuambukiza wenzake, hivyo kumkataa kufanya naye kazi. Amekuwa nje ya uwanja wa kwa muda mrefu, licha ya kwamba mwanzoni mwa msimu alikuwa tegemeo kwenye lango la timu ya Yanga. Tetesi zinaeleza kuwa anawindwa na Mabingwa wa Soka nchini, Simba ili kusaidiana na Aishi Manula na Deogratus Munishi 'Dida'. Pia kuna taarifa kuwa Azam nayo inamnyemelea. Kosa la kiufundi ambalo Simba inaweza kulifanya basi inaweza kuwa faida kwa Azam.

**2. Metacha Mnata- Mbao FC**
Ni kipa mahiri wa Mbao FC ambaye alionyesha umahiri mkubwa kwenye michuano ya Kombe la SportPesa na kutwaa tuzo ya ukipa bora na hata kwenye Ligi Kuu.

Tetesi za usajili zinadai kuwa kipa huyu yuko sokoni na huenda msimu ujao akavaa uzi wa Yanga kwani wapo katika hatua za mwisho za kumalizana.

**3. Aron Kalambo- Prisons**
Kwa msimu miwili mfululizo Yanga imekuwa ikimkosa kipa huyu ambaye yeye mwenyewe anaonekana yuko radhi kutua kama watampatia anachohitaji. Msimu huu pia, kuna taarifa kuwa Yanga imeanzisha tena mazungumzo naye na kama mambo yataenda vizuri huenda akavaa uzi wa Yanga.

**4. Salum Kimenya- Prisons**
Tetesi za misimu mitatu mfululizo kuwa anawindwa na Simba, msimu huu pia zimeanza kusikika wiki hii.

Simba inatafuta mbadala wa Shomari Kapombe ambaye bado ni majeruhi. Hata kama akipona kuna wasiwasi kuwa atachukua muda hadi kurejea kwenye kiwango chake cha kawaida, lakini pia hakuna uhakika wa moja kwa moja kama anaweza kumaliza michuano yote ya msimu bila kupata majeraha.

Imeonekana Kimenya, Afande wa Prisons ndiye suluhisho. Tatizo ni lile lile la miaka yote. Jamaa anahitaji mkwanja wa maana ili iwe kama kiinua mgongo chake, kwa sababu tayari ni mwajiriwa wa Jeshi la Magereza.

**5. Kennedy Juma- Singida United**
Ni mchezaji ambaye moja kwa moja ameonekana kwenye jicho la Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems.

Taarifa zinasema kuwa kocha huyo amewaambia mabosi wake wamsajili beki huyo ambaye pia alichaguliwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars, lakini kwa bahati mbaya ameachwa kwenye mchujo wa mwisho. Ni beki wa kati wa Singida United mwenye nguvu na akili, ambaye tetesi zinasema kuwa msimu ujao huenda akavaa jezi nyekundu.

**6. Salum Kihimbwa- Mtibwa Sugar**
Kwa misimu mitatu sasa amekuwa akihusishwa na kuondoka kwenye kikosi cha Mtibwa Sugar, lakini anabaki kwenye dakika za mwisho.

Misimu miwili iliyopita alikuwa anahusishwa kusajiliwa na klabu za Simba na Yanga, lakini msimu huu ni Yanga pekee inayoonekana kuwa inamhitaji. Naye pia yuko sokoni.

**7. Mwinyi Haji- Yanga**
Ni mchezaji ambaye anamaliza mkataba wake na Yanga. Yeye tetesi za usajili zinamhusisha kutimkia kwenye Klabu za Azam na KMC ambazo zote inasemakana kuwa zinahitaji huduma ya beki huyu wa kushoto.

**8. Gadiel Michael- Yanga**
Tangu kumalizika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara, kumekuwa na tetesi kuwa beki huyo anatakiwa kwa udi na uvumba na Klabu ya Simba.

Hata hivyo, kwa sasa zimefifia na zimeibuka taarifa kuwa huenda beki huyo wa kushoto akasalia kwenye klabu yake ya Yanga, au akarejea kwenye klabu yake ya zamani Azam FC.

**9. Ramadhani Kapera- Kagera Sugar**
Ni straika mwenye matumizi mazuri ya akili na uwezo mkubwa wa kukaa na mpira kwa muda mrefu mguuni.

Straika huyu machachari naye pia yuko sokoni. Klabu ya pesa zake na maelewano inaweza kuchukua kifaa hiki. Kwa sasa anawindwa na klabu kubwa za Simba na Yanga.

**10. Ibrahim Ajibu-Yanga**
Kabla hata Ligi Kuu haijamalizika, tayari tetesi zimemhusisha kuwa ameshamalizana na Simba.

Na inasemekana hata dili la kwenda TP Mazembe lilikwama kwa sababu tayari alikuwa ameshaingia mkataba wa awali na mabingwa hao, hivyo TP Mazembe ambao walitarajia kumsajili kama mchezaji huru wakakuta tayari ana mkataba wa awali na klabu nyingine, kitu ambacho kingewafanya watoe pesa zaidi ya ile ya awali, wakaghairi.

## NJE YA UWANJA

### Uturuki yawashika pabaya Ufaransa

UFARANSA ni mabingwa wa dunia, lakini wameshindwa kupata hata shuti moja lililolenga goli katika mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Uturuki wakati wakichezea kichapo cha mabao 2-0 Jumamosi.

Katika mechi hiyo, mabao ya Uturuki yalifungwa na Kaan Ayhan na Cengiz Under, lakini tofauti hiyo ya mabao ingeweza kuwa kubwa zaidi na kukishangaza kikosi hicho cha Didier Deschamps.

Kwa Ufaransa, mchezo huo ulikuwa wa kwanza katika kipindi cha miaka 10 kwa kucheza bila kutengeneza shuti lililolenga goli. Licha ya kupiga pasi 559 ukilinganisha na pasi 322 za Uturuki.

Uturuki walikuwa wazuri zaidi, wakitengeneza mashuti 11, sita kati ya hayo yakilenga goli katika ushindi huo uliowapeleka kileleni mwa Kundi H wakiongoza kwa pointi tatu zaidi.

Kwa kuweka takwimu, ukweli ni kwamba wachezaji tisa kati ya 11 wa kikosi cha kwanza cha Ufaransa walioanza kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Dunia 2018, wakati wakishinda dhidi ya Croatia, pia walianza katika mechi hiyo iliyopigwa juzi mjini Konya, Uturuki.



## Extra Time

# NYOTA WANAO-SUBIRIWA SOKONI


PHILIPPE COUTINHO

David De Gea

**LONDON, England**

HATIMAYE Eden Hazard muda wake wa kukaa Chelsea umefikia mwisho na sasa anatua Real Madrid tayari kwa ajili ya msimu mpya wa 2019-20.

Hazard hajafanya siri mpango wake wa kutua pale Los Blancos na licha ya Chelsea kufungiwa kutofanya usajili kwa misimu miwili, yeye hakuwa na namna yoyote zaidi ya kubainisha anaondoka.

Madrid imetangaza kwamba itatumia kiasi cha pauni milioni 150 kwa ajili ya kumsajili Hazard kwenda kujiunga na kikosi hicho kilichopo chini ya kocha Zinedine Zidane.

Makala haya yanakuchambulia wachezaji ambao wanaweza kuzihama timu zao kipindi hiki cha usajili wa kipindi cha majira ya joto...

**ANTOINE GRIEZMANN**

Wachezaji wengine huwa hawapendi kujionyesha hadharani hasa kuhusu mawakala wao, wanachozungumza kuhusu mambo yao binafsi. Na hilo ndilo lilipo kwa Antoine Griezmann. Baada ya kubainisha wazi kwamba hana mpango wa kuondoka Atletico Madrid katika mahojiano yake kwenye televisheni mwaka moja uliopita, kwa kutangaza kwamba atabakia klabuni hapo. Lakini sasa mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa amebainisha kwamba anataka kuondoka.

> **Barcelona imebakia kuwa timu pekee ambayo mchezaji huyo anaweza kutua, kwani tayari imeripotiwa kwamba Griezmann ameshafikia makubaliano na miamba hao wa Catalunya. Hata hivyo, pia anahusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu za Manchester United na Paris Saint-Germain.**

**NEYMAR**

Neymar amekuwa akivumishiwa kwamba hana furaha pale PSG na nyota huyo wa kimataifa wa Brazil anatajwa kuwa anataka kuondoka kipindi hiki cha majira ya joto.

Klabu ya Real Madrid imekuwa ikihusishwa na mpango wa kumsajili Neymar, lakini ujio wa Hazard pale kwenye dimba la Santiago Barnabeu unaweza kubadilisha mambo. Lakini pia Neymar anatajwa kwamba kuna uwezekano akarudi katika klabu yake ya zamani ya Barca.

**PHILIPPE COUTINHO**

Kwa Barca kuanzisha mpango wa kutaka kumrudisha Neymar kutahitaji wawe na fedha, na kuna uwezekano mkubwa wa Philippe Coutinho kutumika katika kutafuta fedha za usajili.

Amekuwa akitajwa kwamba ada yake ni pauni milioni 105, huku kocha Ernesto Valverde akipenda kumtumia zaidi Ousmane Dembele kama mshambuliaji wake wa tatu, pamoja na Lionel Messi na Luis Suarez, kuna uwezekano mkubwa Coutinho akarudi kwenye Ligi Kuu ya England, huku Chelsea ikitajwa kumuwania pamoja na PSG ya Ufaransa.

**PAUL POGBA**

Baada ya kuondoka kwa Jose Mourinho, Paul Pogba alionekana kama amezaliwa upya chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer. Hata hivyo, kiwango chake hakijawa cha kuvutia zaidi na baada ya kufungwa na Cardiff City kwenye mchezo wao wa mwisho wa Ligi Kuu ni wazi kwamba nafasi yake hapo ni ndogo.

United inahitaji kukifanyia marekebisho kikosi chake. Kwa muda mrefu Madrid imekuwa ikihusishwa na kutaka kumsajili, huku pia klabu yake ya zamani ya Juventus ikitajwa kumuwania.

**PAULO DYBALA**

Kuwasili kwa Cristiano Ronaldo pale Turin ilikuwa ni habari mbaya kwa mchezaji Paulo Dybala ambaye ameshindwa kuwa kwenye ubora wake. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina alikuwa anatajwa kuwa mmoja wa wachezaji watakaokuwa na majaliwa bora sana ya baadaye, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 anaonekana kutokuwa kwenye wakati wake bora.

Mahusiano yake na kocha aliyetimuliwa, Massimiliano Allegri hayakuwa mazuri katika simu za mwisho, hivyo kuna uwezekano mkubwa wa mchezaji huyo kuondoka, Klabu za Bayern Munich na Manchester United zinatajwa kuwa ndio zinazomuwania.

**NICOLAS PEPE**

Ni Kylian Mbappe pekee aliyefunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, msimu huu wa 2018-19 kuliko nyota wa Lille, Nicolas Pepe, huku PSG ikitajwa kwamba inataka kumsajilii mchezaji huyo.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast, Pepe anaweza kuwa na wakati mzuri zaidi kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, lakini klabu za Ligi Kuu ya England Liverpool, Manchester United na Arsenal zote zinatajwa kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.

**KYLIAN MBAPPE**

PSG mara kadhaa imeripotiwa kukataa kuwauza nyota wake Neymar na Mbappe, lakini inaonekana wazi kwamba nyota hao hawana mpango wa kubakia hapo. Mbappe anaweza kuweka rekodi ya usajili popote atakapokwenda na ni wazi kwamba, Real Madrid wapo tayari kutumia kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya kumsajili.

Pamoja na kwamba Mbappe mwenyewe anawaniwa na Real Madrid, lakini pia Klabu ya Manchester City inatajwa kuisaka saini yake.

**MATTHIJS DE LIGT**

Mabeki mara nyingi sio wachezaji wanaokuwa kwenye soko kubwa la usajili, lakini kwa sasa nahodha wa Ajax, Matthijs de Ligt anaonekana kuwa kwenye soko kubwa mno kwa klabu za Ulaya. Uimara wa uongozi wa De Ligt dimbani umeifanya klabu yake kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini wakatolewa na Tottenham.

Mchezaji mwenzake na De Ligt, Frenkie de Jong tayari amekamilisha usajili wa kutua pale Barca na beki huyo wa kati anatajwa kwamba atafuata nyayo zake. Hadi sasa bado haijajulikana ni klabu ipi anakwenda, lakini kuna uwezekano mkubwa wa kutua pale Barcelona.

**GARETH BALE**

Kocha wa zamani wa Real Madrid, Fabio Capello amesema klabu hiyo inapaswa kutumia kiasi cha pauni milioni 500 kwenye usajili na maana yake kwamba hawatakuwa na namna nyingine zaidi ya kuwauza baadhi ya nyota wake. Mchezaji ambaye anatajwa kuwa kwenye wakati mzuri wa kuuzwa ni Gareth Bale. Huku uhusiano wake na kocha Zinedine Zidane ukiwa haupo vizuri ni wazi kwamba, ataondoka.

Habari kutoka nchini Hispania zinaeleza kwamba, Bale mwenyewe ameshaonyesha wazi kwamba anataka kuondoka. Klabu za Manchester United na Tottenham ndizo zinazotajwa kuwa mchezaji huyo atakakokwenda.

## Nukuu

"Ninasema huwezi kwenda duniani huku ukiwa na mwalimu wa daraja la tatu, hawezi kuwa na jibu la maswali yako kwa daraja unalolitaka, anahitaji kuwa na profesa. [Rob] McCracken ni mwalimu, lakini kwa sasa [Anthony] Joshua hawezi kuendelea kuwa chini yake kwa sababu daraja lake ni la chini, sidhani kama kuna umuhimu wa kuendelea kuwa na mwalimu ambaye kiwango chake kipo chini," Bondia wa zamani wa uzito wa juu na bingwa wa dunia, **Lennox Lewis** baada ya Joshua kuchezea kichapo kutoka kwa Andy Ruiz.



"Mchezaji bora duniani anapaswa kuwa mshindi, kama Juventus ingetwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya tungeweza kusema kwamba [Cristiano] Ronaldo atashinda Ballon d'Or, na endapo Barcelona ingetwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya, tayari ikiwa imeshinda ubingwa wa La Liga, na kama itashinda Copa America tuzo itakuwa kwa Lionel Messi,"
**Jose Mourinho aliliambia Gazeti la Marca.**



"Tunaposema Simba ni timu ya Taifa tunamaana hii, kupeleka timu nne katika mashindano ya kimataifa si mchezo. Simba ipewe nishani ya Uhuru ya Uzalendo uliotukuka," **Mbunge wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe** baada ya Shirikisho la Soka Afrika (Caf), kuthibitisha Tanzania itapeleka timu nne kwenye michuano yake msimu wa 2019/20 kutokana na mafanikio yaliyochangiwa na Simba katika Ligi ya Mabingwa msimu wa 2018/19.



# KIKOSI BORA LIGI KUU 2018/2019 HIKI HAPA



Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere (kulia), akiwa na Emmanuel Okwi, akishangilia moja ya mabao yake msimu huu katika Uwanja wa Taifa.

**Na Adam Fungamwango**

Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2018/19, imemalizika kwa Simba kutwaa ubingwa, ikiwa imejikusanyia jumla ya pointi 93.

Watani zao wa jadi, Yanga wanakamata nafasi ya pili kwa kujikusanyia jumla ya pointi 86, Azam ikimaliza kwenye nafasi ya tatu na pointi zao 75, huku KMC, timu inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni ikikamata nafasi ya nne ikiwa na pointi 55.

Kwa mujibu wa Shirikisho la Soka nchini Tanzania (TFF), timu zote hizi zitaiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya kimataifa.

Simba na Yanga zitacheza Ligi ya Mabingwa Afrika, Azam na KMC zitaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho.

KMC itashiriki kwa sababu Azam ambayo nafasi yake ya tatu ilitosha kuiwakilisha nchi, lakini yenyewe tayari ina nafasi hiyo baada ya kutwaa Kombe la FA, hivyo mshindi wa nne anachukua nafasi hiyo.

Shirikisho la Soka barani Afrika (Caf), ndilo lililoiandikia TFF kuieleza kupatikana nyongeza ya nafasi hizo baada ya Simba kufanya vema kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na kuvuna jumla ya pointi 15.

Ilikuwa ni ligi ngumu iliyokuwa na kila aina ya ushindani, huku wachezaji wengi wakitia fora kwa kuonyesha viwango vya hali ya juu.

Katika mfululizo wa makala haya, tutawaletea mambo yaliyojiri kwenye Ligi Kuu, ikiwamo kikosi cha wachezaji bora wazawa na pia kikosi cha wachezaji bora wageni, leo tunawaletea kikosi bora cha jumla cha msimu kinachojumuisha wachezaji wote bora wazawa na wageni 2018/19 na klabu walizotoka...

**1. Aishi Manula- Simba**

Hakuna mjadala wowote kwa hili. Manula mbali na kuwa ni namba moja kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars, lakini amekuwa mhimili kwenye klabu yake ya Simba kwenye mechi mbalimbali za Ligi Kuu na za kimataifa.

Amekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu kwa muda mrefu, akiwa ameiwezesha klabu yake, si tu kutwaa ubingwa, lakini pia kuwa timu iliyofungwa mabao machache.

**2. Boniface Maganga- Singida United**

Ni shujaa asiyeimbwa. Boniface Maganga ni mmoja wa mabeki mahiri kabisa kwenye Ligi Kuu akiichezea Singida United, lakini amekuwa hatazamwi sana kwa sababu hana makeke.

Kwa watu wanaofuatilia takwimu ndio wanaoweza kujua nini anakifanya. Anacheza kama beki wa kulia, ana uwezo wa kupanda na kushuka. Lakini pamoja na uwezo wake wa kusaidia mashambulizi, lakini ni mfungaji mzuri wa mabao. Mpaka ligi inamalizika, alikuwa amefunga mabao matano akiifungua timu yake ya Singida United, idadi ambayo hata baadhi ya mastraika kwenye Ligi Kuu hawajafikisha.

**3. Bruce Kangwa- Azam FC**

Kwenye timu yako ukiwa na beki kama huyu basi umemaliza. Kangwa ni mmoja wa mabeki bora kabisa kwenye Ligi Kuu ya Tanzania Bara. Ni raia wa Zimbabwe mwenye uwezo mkubwa wa kukaba na kupeleka mashambulizi mbele. Kikubwa ni wepesi wake na kasi kubwa, ikiwamo uwezo wa kutoa pasi za mabao. Anastahili kuwamo kwenye kikosi hiki.

**4. Aggrey Morris- Azam FC**

Ni mmoja wa mabeki wachache wa Tanzania ambaye ana mwili uliojengeka kimazoezi, lakini akiutumia vilivyo akiwa uwanjani. Uzuri wake ni kwamba anatumia nguvu kwenye ulazima wa kufanya hivyo, lakini kunakotakiwa kutumia akili pia anafanya hivyo.

Ni beki wa Azam ambaye kila klabu kubwa ingependa kuwa naye hasa ikizingatiwa kuwa si mabeki wengi wa Kibongo wenye kaliba kama yake, bali wengi ni wa kutoka nje ya nchi.

**5. Erasto Nyoni- Simba**

Huyu ni beki wa kikosi cha Taifa Stars. Ni beki mkongwe, lakini mwenye uwezo mkubwa, akiwa na matumizi zaidi ya akili kuliko nguvu, mnyumbulifu na mwenye uwezo mkubwa wa kumiliki mpira kwa sababu pia ana uwezo wa kucheza kama kiungo.

Amekuwa mhimili mkubwa kwenye klabu yake ya Simba kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa.

**6. Pappy Tshishimbi- Yanga**

Msimu huu amemaliza vizuri na anastahili kuingia kwenye kikosi bora cha msimu ambao umemalizika. Mbali na kucheza kwenye nafasi ya kiungo wa kukaba, lakini amefunga mabao kwenye mechi nyingi muhimu ambazo Yanga ilikuwa inahitaji zaidi matokeo.

**7. Ayoub Lyanga- Coastal Union**

Kwa zile timu ambazo zinahitaji mawinga asilia wale wa kizamani, huyu ndiye anawafaa.

Lyanga ambaye pia ana uwezo wa kucheza kama straika, ana uwezo wa kumiliki mpira wa miguuni, mbio, wepesi, lakini pia machachari na uwezo wa juu wa kufunga mabao.

Mpaka ligi inamalizika yupo kwenye orodha ya wachezaji 10 bora kwenye kupachika mabao, akiwa amepachika jumla ya mabao 10.

**8. Cleotus Chama- Simba**

Ni mmoja wa viungo bora kabisa wa kigeni kuwahi kutokea kwenye soka la Tanzania. Ni mchezaji ambaye hatumii nguvu sana, lakini mwenye maarifa mengi na uwezo wa kunyumbulika na kupiga chenga za maudhi.

Kikubwa pia kwake ni uwezo wa kufunga mabao ambao pia unambeba, lakini pia akiwa na pasi nyingi za mabao kwenye klabu yake ya Simba. Chama ambaye ni raia wa Zambia, anastahili kuwa kwenye kikosi hiki.

**9. Meddie Kagere- Simba**

Raia huyu wa Rwanda ni binadamu ambaye ana sifa zote za kuwa straika. Ana mwili uliojengeka kimazoezi, ana nguvu, stamina na pumzi.

Akiwa uwanjani hakai sehemu moja kiasi cha mabeki kumzoea, badala yake atazunguka kila mahali, kulia, kushoto na katikati ili mradi tu kutafuta sehemu sahihi ya kuwadhuru wapinzani wake.

Ana uwezo wa kufunga mabao kwa kutumia kiungo chochote kile kilichohalalishwa kwenye mpira wa miguu, kuanzia mguu wa kulia, kushoto na kichwa.

Ni mtu hatari zaidi akiwa kwenye eneo la timu pinzani, kwani ni kama vile macho yake yako mguuni, badala ya kichwani.

Ndiye kinara wa mabao kwenye Ligi Kuu msimu huu, akiwa amecheka na nyavu mara 23 na kutwaa Kiatu cha Dhahabu. Mabao hayo yameipa ubingwa timu yake ya Simba.

**10. Heritier Makambo- Yanga**

Ni mmoja wa mastraika hatari kwenye Ligi Kuu msimu huu. Makambo, raia wa Congo DR, hakusajiliwa kwa makeke sana, lakini alitokea kuwa kipenzi cha wanachama na mashabiki wa Yanga kutokana na uwezo wake mkubwa wa kupachika mabao kwa namna ambayo haielezeki.

Amekuwa akifunga baadhi ya mabao akiwa kwenye mazingira magumu. Kwa bahati mbaya msimu ujao hatokuwapo kwani amesajiliwa na Horoya ya Guinea, lakini ameacha rekodi ya kufunga mabao 17 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

**11. Hassan Kabunda- KMC**

Kikosi hiki hakitokamilika kama hajawekwa mchezaji mmoja, Hassan Kabunda kutoka KMC.

Ni mchezaji mwenye kasi, msumbufu mwenye uwezo wa kucheza winga ya kushoto, lakini pia kama straika.

Amekuwa mmoja ya wachezaji waliofanya timu hiyo kuwa tishio hasa kwenye kipindi cha dirisha dogo alichosajiliwa akitokea Mwadui FC na kuifanya kuweza kumaliza nafasi ya nne na kupata nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa.

**NAJUA WAJUA**

UEFA CHAMPIONS LEAGUE

MECHI ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kati ya Liverpool na Tottenham iliyopigwa Uwanja wa Wanda Metropolitano jijini Madrid Juni Mosi mwaka huu, na Liver kushinda 2-0, imeweka rekodi kwa kuwa fainali ya kwanza kuchezwa bila hata kadi moja kutolewa.

SOKA

# LIVERPOOL INAHITAJI WAWILI KAMA HAWA



ADRIEN RABIOT

**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Liverpool ilianza kuonyesha ishara ya ubora wake msimu wa 2017-18 wakati walipocheza vizuri na kumaliza nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England. Safari yao kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa ilithibitisha hilo. Hata hivyo, 'Wekundu' hao hawakuwa na uwezo wa kulitwaa taji hilo wakati Real Madrid ilipokifunga kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kwenye fainali.

Mwaka mmoja baadaye, vijana hao wa Merseyside wakashinda taji la Ligi ya Mabingwa kwa kuifunga Tottenham Hotspur mabao 2-0 kwenye fainali, na hivyo wakalibeba taji lao hilo la sita la Ulaya.

Kwa bahati mbaya walilikosa taji la Ligi Kuu mbele ya Manchester City kwa tofauti ya pointi moja, lakini ushindi wa Liverpool kwenye taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya unaifanya kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kutwaa taji la Ligi Kuu msimu ujao.

Hata hivyo, Wekundu hao wanatakiwa kufanyia marekebisho katika sehemu kadhaa za kikosi chake. Hapa tunawaangalia wachezaji wawili ambao msimu huo Liverpool inapaswa kuwasajili ili kujiimarisha zaidi...

**2. Adrien Rabiot**

Adrien Rabiot yupo huru katika kipindi cha majira ya joto na klabu kadhaa zimekuwa zikuhusishwa na kutaka kumsajili mchezaji huyo wa Paris Saint-Germain. Hata hivyo, kama Liverpool itamsajili Rabiot, kiungo huyo anaweza kukisaidia kikosi cha Klopp kutawala kwa miaka inayokuja.

Liverpool imekuwa na viungo vizuri kama Jordan Henderson, Fabinho, Naby Keita na Georginio Wijnaldumna wakifanya vizuri msimu huu. Hata hivyo, Wekundu hao wa Anfiled wameshindwa kuwa na kiungo ambaye anatawala kiungo wote.

Rabiot ni aina ya mchezaji ambaye anawafaa kutalawa sehemu ya kiungo ya kati kwa kuweza kuichezesha timu na kuitengenezea mashambulizi.

Ana uwezo mkubwa wa kutengeneza mashambulizi kwa timu pinzani na pia kusaidia katika ukabaji na kwa uhakika Liverpool wanahitaji aina ya mchezaji kama yeye. Pia ni mzuri kwenye pasi na kutengeneza pasi za mwisho.

Ingawa Klabu ya Manchester United nao wanatajwa kutaka kumsajili Rabiot, imekuwa ikidaiwa kwamba mchezaji huyo anaweza kuikataa ofa hiyo na kutua kule kwa Wekundu hao wa Anfield.

**1. Nicolas Pepe**

Kwa Mohamed Salah, Roberto Firminio na Sadio Mane, Liverpool ni moja ya timu yenye safu bora zaidi ya ushambuliaji Ulaya. Safu hiyo imekuwa bora kwa kipindi cha misimu iliyopita na kiwango chao cha msimu huu wa 2018-19 kimeonekana bora zaidi baada ya kufanikiwa kulibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na kumaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu.


Hata hivyo, wakati mchezaji mmoja au wawili hao anakuwa hayupo dimbani, wachezaji kama Divock Origi, Daniel Sturridge na Xherdan Shaqiri ndio waliobeba majukumu yao mbele ya goli.

Msimu ujao, Liverpool watahitaji mchezaji ambaye atabeba majukumu hayo na kuimarisha benchi lao. Liverpool imekuwa ikiwategemea zaidi wachezaji hao kwenye safu ya ushambuliaji.

Liverpool imekuwa ikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili Nicolas Pepe, ambaye amekuwa na msimu wa kuvutia kule kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, akiwa na klabu yake ya Lille. Mshambuliaji huyo amewafungia mabao 22 na kutoa pasi za mwisho 11. Mchezaji huyo huyo wa kimataifa wa Ivory Coast amekuwa na wakati mzuri zaidi kwenye ligi hiyo na kama Liverpool itamsajili atakuwa msaada mkubwa kwao.

Anaweza kuifanya safu ya ushambuliaji ya Liverpool kuwa bora zaidi na kuendelea kutamba Ulaya na Ligi Kuu. Na katika umri wake wa miaka 24, anaweza kuwabeba vizuri zaidi.

NDANI YA 18



MABAO mawili Eden Hazard aliyoifungia Chelsea katika mechi ya fainali ya Europa League dhidi ya Arsenal mwezi uliopita, yanamfanya kuwa mchezaji wa kwanza kutoka Klabu za England kuweza kufanya hivyo katika fainali za Uefa, tangu Mark Hughes alipoifungia Manchester United dhidi ya Barcelona kwenye Kombe la Washindi mwaka 1991.

Nipashe Spotika




HUKU msimu wa 2018-19 ukiwa umefikia ukingoni, kwa sasa macho ya wapenzi wengi wa mpira wa miguu yapo kwenye kuangalia majina ya wachezaji ambao watasajiliwa na klabu zao. Klabu kwa sasa zinaingia sokoni kwa...

Uk. 16-17

# USAJILI MBOVU ZAIDI KUWAHI KUTOKEA EPL




**LONDON, England**

LIGI kuu ya England imekuwa ikifuatiliwa zaidi duniani kwa sasa na mamilioni ya mashabiki na kuifanya kuwa na mafanikio makubwa zaidi. Klabu zimetumia fedha nyingi kuwashawishi wachezaji wake. Na hilo limeifanya ligi hiyo kuwa ya ushindani zaidi duniani.

Kwa kutumia fedha nyingi kumezifanya klabu nyingi kuwa na mafanikio makubwa zaidi katika miaka ya hivi karibuni. Tumeona mechi kubwa na pia wachezaji wakubwa waliochomoza kwenye ligi hiyo. Na hilo limeifanya ligi hiyo kuwa ya kuvutia zaidi duniani.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano ambao walishindwa kufikia matarajio ya wengi baada ya kusajili katika historia ya Ligi Kuu ya England.

**5. Angel Di Maria**

Ni jambo la kushangaza kuona mchezaji wa hadhi yake akishindwa kufikia matarajio ya wengi wakati aliposajiliwa na Manchester United msimu wa 2014-15. Akiwa amewasili pale United kwa ada iliyoweka rekodi kwenye soka la Uingereza kwa zaidi ya pauni milioni 59.7, wengi walitarajia mengi kutoka kwa winga huyo wa kimataifa wa Argentina. Ilitumainiwa kwamba, Di Maria angeweza kuimarisha zaidi timu, lakini akajikuta akiwa na msimu mbaya zaidi katika maisha yake ya uchezaji soka.

Alipewa jezi namba saba iliyokuwa ikivaliwa na magwiji wa klabu hiyo, Ronaldo na Beckham. Ishara zilionekana kuwa chanya kwa Di Maria na klabu, kwani alianza msimu vizuri. Alishinda tuzo ya mchezaji bora wa mwezi Septemba.

Lakini baada ya Oktoba mwaka huu, kiwango cha Di Maria kilianza kushuka kwa kasi. Aliumia Novemba na alikaa nje ya dimba kwa kipindi cha Januari yote. Halafu akarudi dimbani lakini akashindwa kuonyesha kiwango chake. Na mwisho wa siku aliweza kufunga mabao matatu tu katika mechi 27 za klabu hiyo, hatimaye akaondoka United na kuelekea PSG msimu uliofuata. Anatajwa na wachambuzi wa soka kama moja ya usajili mbovu zaidi kufanywa na Man United.

**4. Radamel Falcao**

Mmoja wa washambuliaji bora wa kiazi chake, alisajiliwa na Manchester United mwaka 2014 kwa mkopo akitokea Monaco, huku kukiwa na kipengele cha kumsajili moja kwa moja. United walikuwa wanaangalia namna ya kukijenga kikosi chao baada ya kumaliza kwenye nafasi ya saba katika msimamo na ilionekana kwamba, Falcao angekuwa suluhisho muhimu zaidi.

Lakini kama ilivyokuwa kwa mchezaji mwenzake, Di Maria, Falcao alishindwa kufikia matarajio aliyotarajiwa akifunga mabao manne katika mechi 26 alizocheza kwenye Ligi Kuu. United ilikataa kumnunua moja kwa moja mwishoni mwa msimu baada ya kuonyesha kiwango kibovu.

Kipindi chake cha pili pale England kilikuja alipotua Chelsea, wakati aliposajiliwa na Jose Mourinho kwa mkopo na kukiwa na kipengele cha kumsajili moja kwa moja kutoka Monaco mwishoni mwa msimu. Tena akawa na msimu wa kukatisha tamaa baada ya kushindwa kufikia matarajio ya wengi.

Mara nyingi alitumika akitokea benchi na katika nusu ya kwanza ya msimu pale Chelsea alishindwa kabisa kupata namba kwenye kikosi cha kwanza. Kutokana na kiwango hicho duni, Mourinho alifukuzwa Desemba na nafasi yake ikachukuliwa na Guus Hiddink kama kocha wa muda. Kutokana na kukabiliwa na majeraha ya mara kwa mara, kiwango cha Falcao kikashuka na mwishoni mwa msimu akatemwa. Alikuwa amecheza mechi 10 na akarudi tena Monaco msimu uliofuata.

**2. Andy Carroll**

Ni mshambuliaji mwenye muonekana wa kuvutia kama mchezaji. Carroll alisajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 35. Alisajiliwa kama mrithi wa Fernando Torres aliyeondoka. Carroll alikuwa akilinganishwa na wachezaji kama Alan Shearer na Didier Drogba katika kipindi chake cha mwanzo cha uchezaji.

Alisajiliwa na Liverpool msimu wa 2010-11, lakini alilazimika kusubiri hadi Machi mwaka 2011 kutokana na majeruhi aliyoyapata akiwa pale Newcastle. Alicheza mechi yake ya kwanza kwa Liverpool dhidi ya wapinzani wao wakubwa katika soka la England, Manchester United mchezo ambao Liverpool walishinda 3-1.

Katika misimu miwili na klabu hiyo, alijikuta kwenye wakati mgumu wa kufunga bao. Ingawa alionekana kuwa ni mwenye kipaji cha kuvutia, lakini hakuwa kwenye kiwango chake. Alifunga mabao sita tu kwa klabu yake katika mechi 44 alizoichezea klabu yake. Hivyo wakaamua kumuachia. Alipelekwa kwa mkopo West Ham msimu wa 2012-13 na baadaye msimu uliofuata wakamnunua moja kwa moja.

**1. Alexis Sanchez**

Kila mmoja alitarajia kwamba Alexis Sanchez angeweza kufanya makubwa zaidi kwa Manchester United akitokea Arsenal Januari mwaka 2018. Lakini kilichofuata kilishangaza kila mmoja kwani Sanchez alishindwa kabisa kuwa kwenye kiwango chake.

United walishinda kwenye mbio za kuwania kumsajili dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja, Manchester City na kumsajili Sanchez akitokea pale Arsenal na ndiye mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu ya England. Alitarajiwa kwamba anaweza kuwa mchezaji muhimu zaidi kwa United na kocha Jose Maounriho kumsajili. Lakini akashindwa kufikia kiwango na akatemwa kikosi cha kwanza na Mourinho.

Katika msimu uliofuata, Sanchez pia alishindwa kuonyesha kile kilichotarajiwa na hata Solskjaer ameshindwa kumtumia. Amecheza mechi 32 kwenye Ligi Kuu akiwa na Man United na sasa Sanchez anatazamiwa kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

## USILOLIJUA



Esperance imetwaa Kombe Ligi ya Mabingwa Afrika kwa mara ya pili mfululizo bila kupoteza mechi hata moja na hivyo kufikia rekodi yake ya mwaka 1994. Hata hivyo, Shirikisho la Soka Afrika (Caf), limetoa uamuzi wa mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Esperance na Wydad Casablanca kurudiwa baada ya mechi hiyo kuvunjika katika dakika ya 60 kutokana na Wydad kugomea mchezo kufuatia bao lao kukataliwa.



## Wavamizi barabara watangaziwa kiama

**Na Grace Mwakalinga,**
SONGWE

MENEJA wa Wakala wa Barabara (Tanroads), Mkoa wa Songwe, Mhandisi Yohana Kasaini, ametangaza kufanya operesheni ya kuwafukuza wananchi wote waliovamia Hifadhi ya Barabara kuu ya Mbeya –Tunduma.

Lengo ni kukomesha shughuli za kibinadamu na uchafuzi wa mazingira uliokithiri kwenye hifadhi ya barabara hiyo.

Mhandisi Kasaini aliyasema hayo juzi, wakati zoezi la usafi lililofanyika kwenye hifadhi ya barabara, kipande cha kilomita nne mjini Vwawa, alisema uharibifu unaofanyika kwenye hifadhi ya barabara ni mkubwa na kwamba serikali haiwezi kufumbia macho.

Alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wakiiba vifaa, kuhifadhi takataka kando ya barabara na wengine kujenga karibu na barabara, alidai operesheni hiyo itasafisha maeneo yote bila kujali makazi ya watu kwa sababu hawajatii sheria.

"Kwa kuonyesha msisitizo wa suala hili, Tanroads tumeamua kufanya usafi wa barabara hapa mjini Vwawa ni salamu kwa maeneo mengine hatufanyi usafi bali tutaenda kutekeleza sheria... nawaomba wananchi wote wanaofahamu wamejenga kando na hifadhi ya barabara kuu waondoke," alisema Mhandisi Kasaini.

Mmoja wa wananchi walioshiriki operesheni ya usafi, Selina Mkwali, alisema serikali inatumia fedha nyingi kwenye ujenzi wa barabara na kwamba kwa umuhimu huo kila mmoja anatakiwa awe mhifadhi wa barabara.

Alisema mwananchi yeyote atakayekaidi agizo la serikali la kujenga karibu na barabara au kutupa taka kando ya barabara, achukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria ili liwe fundisho kwa wengine.



Wananchi wakipita kwa shida kwenye mlango wa kuingia katika Soko la Temeke Sterio, jijini Dar es Salaam jana, kutokana na maji machafu yanayotiririka kutoka kwenye taka. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Watetezi haki za binadamu wawapa somo wanahabari

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) Tanzania, umewataka waandishi wa habari kutoogopa kuandika habari zenye ukweli ambazo zinalenga kuibua maovu ikiwamo vitendo vya rushwa na matumizi mabaya ya madaraka.

Ushauri huo ulitolewa juzi wakati wa mafunzo ya siku tatu kwa waandishi wa habari wa Nyanda za Juu Kusini na Mweeshaji na Wakili wa Mtandao huo, Deo Bwire, kwa kusema baadhi ya waandishi wamekuwa waoga kuripoti habari zinazoibua vitendo viovu wakihofia kutishiwa.

Bwire aliongeza kwamba mwandishi asiogope kuandika habari za ukiukwaji wa haki za binadamu, isipokuwa cha msingi azingatie maadili na ukweli wa habari husika.

Wakili Bwire alisema habari zinazoibua maovu ni nzuri kwa sababu zina lengo la kufichua maovu ya watu au mtu na kuchukuliwa hatua kuliko kuendelea kuandika habari za kusifia kila mara ambazo wakati mwingine hazileti changamoto.

Aliwataka waandishi wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ya Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe na Rukwa ambao walishiriki mafunzo hayo kuyafanyia kazi kwa kuhakikisha wanakuwa chachu ya mabadiliko kwa kuzingatia weledi na kuzingatia sheria za nchi.

"Mafunzo haya ya usalama na sheria za habari kwa wanahabari yanalenga kuwakumbusha juu ya usalama wao wanapotimiza majukumu hasa kipindi hiki tunapoelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa kufahamu sheria za kujilinda ili kujiweka salama wasiingie kwenye matatizo," alisema Wakili Bwire.

Aidha, aliwasisitiza kuzingatia usalama wao wakati wanatimiza majukumu kwa kuhakikisha wakati wa kuripoti habari za vurugu au mikusanyiko ya watu wanakaa sehemu salama ili wasiharibiwe vifaa vyao au kudhuriwa miili yao.

Alisema tahadhari hiyo itawasaidia kutekeleza majukumu yao bila bughudha yoyote na kusisitiza waandishi kutii sheria na mamlaka wanapotafuta habari.

Naye Wakili Jones Sendodo alisema waandishi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, walifundishwa namna nzuri ya kuripoti habari zenye kuibua changamoto za haki za binadamu.

Alisema mbinu walizofundishwa zitatoa nafasi kwa wananchi wasio na uwezo wa kifedha au mali kupaza sauti zao na kusaidiwa kisheria.

Alisema waandishi kwa kushirikiana na Mtandao huo wakitetea haki za binadamu kwa pamoja, watasaidia kila mwananchi kuheshimu haki za mwenzake.

Mnufaika wa elimu hiyo, Joshua Joel kutoka Mkoa wa Rukwa, alisema mafunzo hayo yametolewa kwa wakati sahihi ambapo taifa linaelekea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, na kuwa walijifunza njia za kujihami wanapotekeleza majukumu yao ya kihabari.

Mercy Sikabogo kutoka Mkoa wa Songwe, alisema waandishi wanakabiliwa na changamoto katika kutekeleza majukumu yao hasa pale wanaporipoti habari zinazohusu rushwa kutoka kwa baadhi ya viongozi.

# W'biashara Tanzania, Zambia wakubaliana mifuko ya plastiki

**Na Grace Mwakalinga,**
SONGWE

WAFANYABIASHARA wa Tanzania na Zambia wamekubaliana kutekeleza agizo la serikali la katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki baada ya Zambia kutangaza kusitisha matumizi ya mifuko hiyo ifikapo Agosti Mosi mwaka huu.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya ya Momba, Juma Irando, katika kikao cha pamoja na Mkuu wa Wilaya jirani ya Nakonde nchini Zambia.


Alisema walikubaliana kutekeleza mikakati ya pamoja kuhakikisha katazo hilo pande zote mbili linafanikiwa kwa asilimia 100 kwa wafanyabiashara na wananchi wa nchi hizo.

Alisema mwitikio wa wafanyabiashara na wananchi wa Zambia umekuwa mkubwa kwa kuwa wametambua athari za matumizi ya mifuko ya plastiki, na kwamba serikali yao itaanza kutekeleza agizo hilo Agosti Mosi.

"Katika kutekeleza hayo, ninawaomba wafanyabiashara ambao wanafanya biashara zao katika boda ya Tunduma kuendelea kutekeleza agizo la Serikali ya Tanzania la kuzuia matumizi ya plastiki ili wasichukuliwe hatua za kisheria," alisema Irando.

Mkazi wa Wilaya ya Nakonde, Maria Kunchule, alidai kufurahishwa na katazo la serikali la matumizi ya mifuko ya plastiki.

Alisema katazo hilo linatoa fursa kwa wafanyabiashara na wawekezaji kuanzisha viwanda vidogo na vikubwa vya kuzalisha mifuko mbadala.





# CWT yafafanua umiliki mali zake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BODI ya Wadhamini wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), imesema umiliki wa mali za CWT upo chini ya chama hicho, na kuwataka walimu nchini kupuuza maneno yanayozungumzwa kuwa mali hizo si zao.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Clement Mswanyama, alipokuwa akitoa ufafanuzi wa umiliki wa majengo, mali na Benki ya Mwalimu (MCB) ambavyo vilidaiwa kuwa si mali ya walimu.

Alisema kumekuwapo na taharuki kuhusu umiliki wa mali hizo jambo ambalo si la kweli na zinaenezwa na wanachama walioshindwa kwenye uchaguzi.

Akizungumzia kuhusu umiliki wa kampuni tanzu ya CWT ijulikanayo kwa jina la TDCL, mwenyekiti huyo alisema kampuni hiyo ilianzishwa kwa ajili ya kusimamia uwekezaji unaofanywa ndani ya chama.

"CAG alipofanya ukaguzi maalum ndani ya chama alibaini kuwa kampuni hiyo ni mali ya CWT isipokuwa hayakuwapo makabidhiano rasmi ya usimamizi wa kampuni hiyo kitu ambacho alishauri kifanyike mapema na tayari tupo hatua za mwisho kukamilisha suala hili," alisema.

Alifafanua kuwa umiliki wa hisa kwenye kampuni hiyo awali uliwekwa kwa majina ya viongozi wa CWT, lakini hawakuwahi kuchukua gawio lolote. Hata hivyo, alisema kwa sasa hisa hizo zipo chini ya wadhamini wa CWT na Katibu Mkuu wa CWT.

"Hata hivyo kutokana na kuwa na marekebisho ya mara kwa mara ya mgawanyo wa hisa za TDCL bado kuna jitihada zinaendelea za kuhakikisha nyaraka zote za Msajili na Kampuni(Brela) zinasomeka kwa majina ya wadhamini na Katibu wa CWT," alisema.

Kuhusu Benki ya MCB, Mswanyama alisema benki hiyo inamilikiwa na walimu kwa asilimia 51.35, huku PSSSF ikimiliki hisa asilimia 16.17, NHIF asilimia 16.17 na umma asilimia 16.31.

"Hata hii bodi yake ya wakurugenzi wa benki wapo sita na miongoni mwao walimu ni wakurugenzi wanne, hichi ni kitega uchumi cha chama kilijengwa kwa kutumia mapato asilimia mbili za wanachama," alisema.

Alieleza kuwa kitega uchumi hicho kinasimamiwa na kampuni ya chama ya TDCL na kilianzishwa kuwahudumia wanachama pindi ambapo chama kitakuwa na mdororo wa kiuchumi katika vyanzo vingine.

Mswanyama akizungumzia kuhusu majengo ya mikoa na wilaya, alisema majengo hayo yote ni mali ya chama na yamejengwa kwa ajili ya kuhudumia wanachama wake.

Alisema kwa upande wa viwanja 29 vya TDCL vilinunuliwa mwaka 2015 mkoani Morogoro na tayari viwanja 15 vimeshapata hati miliki, huku vilivyosalia vikisubiri mchakato ukamilike.

# Waitara azibana asasi za kiraia

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imezitaka asasi za kiraia (AZAKI) kuhakikisha zinaweka mifumo mizuri ya usimamizi wa fedha za miradi wanayoitekeleza, ili iweze kuwafikia walengwa.

Sambamba na hilo, zimeagizwa kufanya kazi kwa karibu na watendaji wa serikali za mitaa katika maeneo wanayotekeleza majukumu yao.

Maagizo hayo yalitolewa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Mwita Waitara, katika kikao na wakurugenzi wa asasi hizo ambacho kiliambatana na kusaini mikataba ya ruzuku kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo Tanzania Bara na Visiwani.

Waitara alisema serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na asasi za kiraia katika kusukuma mbele maendeleo vijijini, hususani kuleta teknolojia mpya na rahisi kwa wananchi kupinga mila potofu na kandamizi miongoni mwa jamii katika maeneo ya pembezoni.

Alisema wakurugenzi hao wanapaswa kufanya matumizi sahihi ya fedha za mradi jambo ambalo litaleta tija kwa jamii na serikali.

"Nitafurahi kuona walengwa wamefikiwa na fedha za mradi, nisingependa kusikia jamii inalalamika juu ya suala hilo," alisema Waitara.

Aidha, Naibu Waziri huyo alisema pamoja na AZAKI kujenga uwezo wa wananchi katika kutatua changamoto zinazowakabili wanapaswa pia kuwajengea uwezo viongozi wa serikali za mitaa ili wajue jinsi ya kutekeleza majukumu yao kiufanisi kupitia mafunzo mbalimbali yanayotolewa katika miradi.

Akizungumzia ruzuku kwa mwaka huu, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Uwezeshaji Asasi za kiraia (FCS), Francis Kiwanga, alisema kwa mwaka huu wametoa kiasi cha Sh. bilioni 11.7 kwa asasi za kiraia 154 ambazo zimekidhi vigezo vya kupata ruzuku hiyo ili wakatekeleze majukumu yao.

Alisema lengo la taasisi hiyo ni kuwekeza katika utoaji wa ruzuku kwa AZAKI na kuleta mabadiliko chanya yanayogusa maisha ya Watanzania.

"Lengo hasa la uwekezaji huu ni kuwajengea uwezo wananchi kupitia AZAKI na nafasi kubwa tunatoa kwa asasi kutoka ngazi za chini kabisa kwa jamii, ambapo wananchi wanabainisha matatizo yao na kupendekeza utatuzi nasi tunawapatia nguvu ya ruzuku kupitia AZAKI," alisema Kiwanga.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Taasisi ya Tusonge kutoka Moshi, Aginata Rutazaa, alisema wao kama asasi za kiraia watahakikisha wanaweka uwazi katika matumizi ya fedha hizo ili ziweze kuleta tija kwa wahusika.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa CCM Wilaya ya Bahi, Hassani Kadoke, akizungumza na vijana wa kata ya Chikola wakati wa ziara yake ya kuimarisha chama kuelekea uchaguzi wa serikali ya mitaa na vijiji. **PICHA PETER MKWAVILA**

# REA yawakalia kooni makandarasi wake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA) umewataka makandarasi wanaotekeleza mradi wa REA awamu ya tatu kwenye mzunguko wa kwanza kuhakikisha ifikapo Desemba mwaka huu, wawe wamekamilisha kazi hiyo la sivyo watanyang'anywa kazi.

Sambamba na hilo, watalazimika kulipa gharama za usumbufu watakaokuwa wamewasababishia wananchi kwa kukosa umeme.

Agizo hilo lilitolewa jana na Kaimu Mkurugenzi wa REA, Amos Maganga, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, baada ya kumalizika kwa kikao kilichowashirikisha wadau wa usambazaji vifaa, wazalishaji na wahandisi nchini.

Alisema lengo lao ni kuhakikisha kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo inaongezeka.

Alibainisha awali mradi huo ulikuwa ukamilike mwezi Juni mwakani, lakini sasa wanapaswa wakamilishe mwaka huu ili miezi inayobaki ya mwakani waitumie kwa matengenezo madogo madogo.

"Mpango uliopo ni kuwa mradi huo ukamilike kati ya mwezi Mei na Julai mwakani, lakini katika kikao hiki tumekubaliana makandarasi na wasambazaji wa vifaa wahakikishe mradi huu unakamilika Desemba, ili miezi sita inayobaki 2020 iwe ni kazi ya kumaliza matatizo madogo madogo," alisema.


Aliongeza, "Mkataba upo wazi kwamba wale makandarasi watakaoona kwamba kufika Desemba hawataweza kumaliza mikataba yao, ni kwamba serikali kupitia REA watakuwa tayari kusitisha mikataba yao na kuwanyanganya kazi," alisema.

Maganga alisema kwa sasa serikali inatekeleza mradi mkubwa wa REA unaogharimu Sh. trilioni 1.2, ikiwa ni mradi mkubwa kusini mwa jangwa la sahara, ambapo vijiji 3,559 vitanufaika kwa kupatiwa umeme na wateja zaidi ya laki tatu watafaidika.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya REA, Dk. Michael Nyagoga, alisema lengo la kikao hicho ilikuwa ni kufahamiana, kujadili changamoto na kuzitatua kwa pamoja. Alitaja changamoto kubwa ambayo imezungumzwa ni upatikanaji wa vifaa na elimu ambapo wamekubaliana kuzitatua.

Naye mmoja wa makandarasi Anord Zali kutoka Kampuni ya CRCEBG ambayo inatekeleza miradi ya REA mkoani mkoa wa Katavi, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanakamilisha mradi kama mkataba unavyosema.

Alisema walikuwa wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa vifaa na utaratibu wa LC inayotolewa na Benki Kuu, lakini kupitia kikao hicho wameweza kujua na kwa sasa hakuna jambo la kuwakwamisha.





Meneja Msaidizi wa Hoteli ya Serena mjini Zanzibar, Ellieta Mbise (wa pili kulia), akishirikiana na wafanyakazi wa hoteli hiyo kufanya usafi kuadhimisha Siku ya Usafi Duniani jana, baada ya kuahirishwa wiki iliyopita kutokana na Idd El Fitr. Washiriki walisafisha maeneo ya fukwe za bahari karibu na hoteli hiyo. **PICHA: MARTIN KABEMBA.**

# Tamwa yamfagilia RC kupinga udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa), Ofisi ya Zanzibar, imempongeza Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, kwa kupambana na udhalilishaji wa kijinsia mkoani humo.

Akizungumza na wajumbe wa kamati ya utetezi ya Tamwa, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Shifaa Said Hassan, alisema Tamwa inaunga mkono jitihada zinazofanywa na kiongozi huyo kwa kupambana na vitendo hivyo ambavyo ni kinyume na taratibu za dini, na desturi.

Aidha, alimtaka mkuu huyo wa mkoa kutovunjika moyo bali kuendelea na kasi hiyo ili kuweza kupunguza au kutokomeza kabisa vitendo hivyo.

Alisema hivi sasa kumekuwa na vitendo vya udhalilishaji, ambapo wanawake wanabakwa na kuuawa huku watuhumiwa wa kesi hizo hawakamatwi.

Kwa mujibu wa Hassan, wanashtushwa kuona baadhi ya kesi ambazo waathirika wa matukio hayo mwanzo hutoa ushirikiano mzuri, lakini kila kesi inapofikia pazuri wanakataa kwenda mahakamani.

"Tuna ushahidi wa kesi moja iliyopo mahakamani na mwathirika alikuwa anatoa ushirikiano, lakini hivi sasa kesi imefikia hatua nzuri na mshtaki hapatikani anakataa kwenda mahakamani...tuna wasiwasi pengine wanatishwa au rushwa imetawala," alisema.

Naye Meneja Sera na Utetezi wa Tamwa, Hawra Shamte, alisema kukosekana kwa ushahidi kwa kesi za udhalilishaji ni changamoto kubwa kwa kuwa watuhumiwa hawajulikani walipo na kesi nyingi hazifiki mahakamani.

Alisema mwaka 2016 hadi 2019 matukio 18 ya mauaji ya wanawake yaliripotiwa, lakini watuhumiwa wameshindwa kutiwa hatiani kwa sababu hawajulikani. "Tutapata ufumbuzi gani wa matatizo haya hasa kwa hawa ambao wanafanya vitendo vibaya halafu wanatoweka," alihoji.

Alieleza kuwa mataifa mengine yanapojitokeza matukio kama hayo hutumia polisi wa kimataifa (Interpol) ambao huwakamata watuhumiwa kwa urahisi na kwa wakati.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Mahmoud, alisema tatizo la udhalilishaji ni kubwa na kwamba serikali inatambua na ndiyo maana ikaandaa mpango maalum wa miaka mitano wa kukabiliana na tatizo hilo.

Alisema katika mpango huo lipo jukumu la serikali, jamii, asasi za kiraia, madaktari, Jeshi la Polisi, Mahakama, DPP na ofisi ya mwanasheria mkuu wa serikali, ili kesi hizo kwenda kwa haraka bila ya vikwazo vyovyote na kutafakari namna ya kukomesha vitendo hivyo.

"Kuna viashiria vinne vinavyosababisha udhalilishaji ikiwamo dawa za kulevya, miziki isiyodhibitiwa na ndio maana nikapiga marufuku uvutaji wa shisha na upigaji miziki kiholela katika mkoa huu na badala yake upigwe siku za mapumziko," alisema.

Alisema kiashiria kingine ni baa zisizodhibitiwa ambazo zimewekewa utaratibu maalum wa kufunguliwa saa kumi jioni na kufungwa saa sita usiku ndani ya mkoa huo.

Alieleza pia kulikuwa na nyumba nyingi zikitumika kama madanguro ambazo zimejaa madada na makaka poa, lakini jambo hilo hivi sasa limepungua baada ya kufanya operesheni maalum.

"Tunahitaji kwanza wenyewe tupige vita, bahati mbaya hawa wanaofanyiwa udhalilishaji hawafichi wanawataja baadhi ya viongozi wanaowafanyia vitendo hivyo na ndio maana wengi wao wanaogopa usalama wao na wanaogopa nafasi zao za kazi," alisema.

Mkuu wa mkoa huyo alisema baadhi ya watendaji sio waaminifu wamekuwa wakiwaambia watuhumiwa wa udhalilishaji wakimbie ili ushahidi usiweze kupatikana.

# Dk. Shein ataka ushiriki wa Z'bar kuongezwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameitaka taasisi ya Al – Hikma Foundation kuzingatia kiwango chenye uwiano kwa washiriki wa Zanzibar, pale inapoandaa mashindano ya kuhifadhisha Qur-ani.

Akizungumza jana na Uongozi wa taasisi hiyo Ikulu mjini Zanzibar, alisema kuna umuhimu mkubwa kwa taasisi hiyo pale inapofanya shughuli zake, hususan zinazoambatana na mashindano ya kuhifadhi Qur-ani.

Aidha, alisema eneo jingine ni upatikanaji wa fursa mbalimbali zikiwamo za kijamii, kuzingatia umuhimu wa kuongeza kiwango cha kuishirikisha Zanzibar kwani kiwango cha sasa ni kidogo.

Dk. Shein ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alisema amevutiwa na juhudi zinazofanywa na taasisi hiyo na kwamba ni matunda yanayotokana na kuwapo kwa viongozi bora, sambamba na kuitaka kuendelea kuitumia kikamilifu fursa ya kuwa na mlezi, Ali Hassan Mwinyi.

Aidha, Dk. Shein amesema usimamizi wa mashindano ya kuhifadhisha Qur-an kunakofanywa na taasisi hiyo ni njia bora katika kuwajenga watoto kupenda kuhifadhi Qur-an.

Dk. Shein aliipongeza taasisi hiyo kwa kufikisha miaka 22 tangu kuanzishwa kwake, sambamba na kutekeleza jukumu lake la kusimamia mashindano ya Qur-an kwa kipindi chote hicho.

Aidha, alipongeza taasisi hiyo kwa hatua mbalimbali inazozichukuwa katika uimarishaji wa huduma za kijamii, ikiwamo uchimbaji wa visima na ujenzi wa misikiti, ambapo ni hatua nzuri na muhimu kwa jamii ya Watanzania.

Awali, Mwenyekiti wa Al-hikma Foundation, Sheikh Nurdin Muhammed Ahmeid Al-Ahdal 'Kishki' alisema Qur-an ni msingi wa dini na yule mwenye kuifahamu huwa mcha Mungu na raia mwema.

Alisema kamati iliyoundwa kwa ajili ya kuhifadhisha Qur-an kutoka taasisi hiyo, pamoja na shughuli nyingine pia inajishughulisha na suala la kuhubiri amani nchini kwa kuzingatia umuhimu wake kama ulivyobainishwa katika dini ya kiislamu.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Al-Hikma Foundation Zanzibar, Omar Hussein Mussa, alimhakikishia Dk. Shein kuwa taasisi hiyo inafanya kazi zake kwa kuzingatia pande mbili za Muungano, akibainisha hekima zake zimeiwezesha kufanikisha shughuli hizo kwa uwazi na mafanikio makubwa.

Aidha, aliiomba serikali kuipatia eneo la ujenzi taasisi hiyo, ili iweze kuanzisha rasmi tawi lake visiwani humo, hatua itakayofungua milango ya uendelezaji wa huduma mbalimbali za kijamii zinazofanywa na taasisi hiyo, kama vile uchimbaji wa visima, ujenzi wa misikiti na uanzishaji wa skuli za msingi na sekondari.

Mwenyekiti huyo alimweleza Dk. Shein kuwa kupitia Jumuiya ya Kuhifadhisha Qur'an Zanzibar, watoto kadhaa wamepata mafanikio ya kuwa washindi katika mashindano tofauti ya kuhifadhi Qur'an yaliofanyika katika nchi mbalimbali barani Afrika.

# Serikali yatakiwa kuajiri mkalimani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar, imeombwa kuajiri wakalimani wa alama katika taasisi zake muhimu ikiwamo Mahakama, ili kutoa fursa kwa watu wenye ulemavu hasa viziwi kutoa ushahidi na kupata haki zao.

Mwanasheria Haji Suleiman Tetere, alisema ikiwa serikali itaajiri watu hao basi kesi nyingi za udhalilishaji zinazowahusu watu hao zitasikilizwa bila kikwazo chochote na haki itatendeka.

Mwanasheria huyo alisema kuwa kuna kesi nyingi za udhalilishaji zinazowahusu watu wenye ulemavu, lakini zinashindwa kusikilizwa kutokana na kukosekana wakalimani.

"Tunaona kesi nyingi mahakamani zinashindwa kuendelea mbele kutokana na kukosekana mkalimani na wengine kukodi wakalimani wa nje ambao wengine wanakuwa hawajasomea lugha ya alama," alisema Tetere ambaye pia ni wakili wa kujitegemea.

Kwa mujibu wa mwanasheria huyo, upo umuhimu wa kuhakikisha taasisi za umma kuajiri watu hao, ili kutoa fursa kwa walengwa kupata haki zao za msingi ikiwamo mawasiliano kwa kuwa zipo kisheria.

Akizungumzia haki ya kupata taarifa katika vyombo vya habari, Tetere, alisema sheria ya watu wenye ulemavu kipengele cha 22 kinaeleza upatikanaji wa habari na taarifa.

Aidha, alisema sheria hiyo imetoa jukumu la vituo vyote vya habari vilivyosajiliwa Zanzibar, kuhakikisha vinaweka mkalimani au maandishi ili watu wenye ulemavu waweze kujua taarifa zilizokuwapo katika nchi yao.

Kwa mujibu wa Tetere, kuna kikwazo katika upatikanaji wa habari kwa watu wenye ulemavu hasa viziwi, kwani kwa mujibu wa sheria imewekwa kuwa ni lazima kwa vyombo vyote vya habari kuweka maandishi katika taarifa za habari, matukio makubwa ya nchi na kuweka mkalimani wa lugha ya alama.

HABARI MIKOANI

# Wanafunzi kupimwa mimba kila miezi mitatu

**Na Lilian Lugakingira,**
BUKOBA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Muleba mkoani Kagera imeweka mikakati ya kuwapima mimba wanafunzi kila baada ya miezi mitatu, ikiwa moja ya jitihada za kupambana na mimba za utotoni.

Akizungumza wakati wa tathmini ya kampeni ya upingaji ndoa na mimba za utotoni wilaya humo, iliyoanzishwa mwaka 2018 na shirika lisilo la kiserikali la World Vision Tanzania kanda ya Mkoa wa Kagera, Ofisa Ustawi wa Jamii wilayani Muleba, Rosemary Nicodemu, alisema tatizo la mimba za utotoni limekuwa kikwazo kwa wanafunzi wa kike kutimiza malengo yao.

Nicodem alisema kuwa katika mkakati walioupanga wataishirikisha jamii nzima ikiwamo wazazi wa wanafunzi, ambao watahusika kuripoti matukio ya mimba na kukemea shughuli za usiku.

Alitaja baadhi ya sababu zinazochangia uwapo wa mimba za utotoni ni mmomonyoko wa maadili kwa watoto katika jamii, kutokana na baadhi ya wazazi kushindwa kutimiza wajibu wao katika malezi ya watoto wao.

Hata hivyo, alisema licha ya serikali kuweka mikakati mbalimbali ya kupambana na tatizo hilo, wazazi wamekuwa kikwazo kwa kushindwa kutoa ushirikiano wa taarifa kwa ajili ya ufuatiliaji wa watuhumiwa.

Alisema katika kukabiliana na tatizo hilo, halmashauri hiyo imekuwa ikifanya kila jitihada kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo Shirika la World Vision kuendesha mikutano shuleni na katika jamii, juu ya uhamasishaji wa kampeni na uelewa wa madhara ya mimba za utotoni.

Kaimu Ofisa Elimu wilayani Muleba, Godelina Ngirwa, alisema wanafunzi wa kike kwa shule za msingi na sekondari hushindwa kutimiza ndoto zao za kielimu kutokana na changamoto ya mimba.

Ngirwa alisema kwa shule za msingi na sekondari wanafunzi waliopata mimba katika kipindi cha miaka miwili na nusu ni 138 wakiwamo wa shule za msingi 34 na shule za sekondari 104.

Kwa upande wa kitengo cha Dawati la Jinsia kutoka Polisi Muleba, Shangwe Mlela, alisema kuwa kila mmoja kwa wakati wake anapaswa kuongeza jitihada ili kusaidia kupunguza msongamano wa kesi zinazopokelewa polisi.

Alisema tatizo kubwa ni mzazi kushindwa kutoa ushahidi na kuficha kesi kwa kupoteza uhalisia, hali inayochochea kuendelea kwa vitendo vya mimba shuleni na ndoa za utotoni.

Aliongeza kuwa kwa mwaka 2018 kesi 94 ziliripotiwa, ambapo watuhumiwa waliokamatwa ni 29 na waliofikishwa mahakamani ni 16. Kati ya hao waliofungwa ni wanne, huku watuhumiwa tisa wakilazimika kuripoti polisi kusubiri vipimo vya vinasaba (DNA).

Alisema kuwa kwa mwaka 2019, hadi mwezi Juni, kesi 39 zimeripotiwa na watuhumiwa 13 wamekamatwa, ambapo saba wamefikishwa mahakamani na kesi zinaendelea, huku wengine sita wakisubiri vipimo vya DNA.

Naye mratibu wa World Vision wilayani Muleba, Godluck Inko, alisema kwa kutambua haki ya mtoto, shirika hilo limejikita zaidi kumwepusha mtoto wa kike na madhara ya mimba na ndoa za utotoni, kwa kuweka vipaumbele mbalimbali ikiwamo kutoa elimu kwa jamii.

## Vodacom yakusanya tril. 1/-

**Na Enock Charles**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania, imefanikiwa kukusanya Sh. trilioni 1 kufikia Machi 31 mwaka huu, ikiwa ni asilimia 5.4 inayotokana na utoaji wa huduma na ukuaji wa asilimia 9.6 katika kuhodhi soko la kampuni hiyo nchini.

Hayo yalibainishwa kwa waandishi wa habari mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mkuu wa Vodacom Tanzania, Hisham Hende, alisema pato hilo limetokana na ukuaji huduma za M-Pesa, intaneti na meseji zinazotumiwa na wateja wake nchini kote.

"Kutokana na ukuaji huo kampuni yetu imeendelea kuwa namba moja kwa huduma za simu na M-pesa na tunahodhi soko kwa asilimia 32," Hendi alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kukua kwa huduma ya M-pesa kunaongeza uchumi jumuishi kwa wananchi hasa kwa kuanzishwa kwa huduma kama "Lipa kwa m-pesa", ambayo imerahisisha wananchi kutuma na kutumiwa fedha na hivyo kuwasaidia mamilioni ya Watanzania kupata ajira.

Alisema kampuni hiyo yenye wateja wanaokadiriwa kufikia milioni 14 nchini kwa sasa hufanya miamala yenye thamani ya Sh. trilioni 4.1 kwa mwezi kupitia M-pesa na hivyo kuisaidia serikali katika kukuza uchumi wenye ushindani na kutoa ajira rasmi na zisizo rasmi.

"Pato la M-pesa limekua kwa asilimia 14.5 kufikia Sh. bilioni 333.5 tunahodhi soko la huduma fedha kupitia simu kwa asilimia 38.6 na tunawafikia watumiaji wa M-pesa milioni 7 na miamala ya thamani ya Sh. trilioni 4.1 hufanyika kila mwezi," Hendi aliongeza kusema.



Meneja Mkuu wa Kampuni ya KNAUF Tanzania Ltd, Georgios Zachopoulos (kulia), akitoa maelezo kwa Mwenyekiti na Kamishna wa Tume ya Madini, Prof. Idris Kikula (kushoto) wakiwa kwenye eneo la machimbo ya madini. **PICHA:WM**

## Wahujumu miundombinu sasa wasakwa

**Na Mwndishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangapo, amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Kalambo pamoja na kamati yake ya ulinzi na usalama ya wilaya kuwasaka na kuwatia nguvuni wananchi wanaosadikiwa kuhujumu miundombinu ya maji katika Kijiji cha Kisongamile.

Kijiji hicho kipo jirani na ujenzi unaoendelea wa Hospitali ya Wilaya ya Kalambo, hali inayosababisha kurudisha nyuma kasi ya ujenzi wa hospitali hiyo.

Alisema kuwa hospitali hiyo ni ya kwao na kwamba wao ndio wa kwanza kufaidika na ujenzi wa hospitali hiyo itakapokamilika, hivyo amemtaka mkuu huyo wa wilaya kuhakikisha analimaliza tatizo hilo ndani ya muda mfupi ili kuendana na ratiba ya umaliziaji wa ujenzi wa hospitali hiyo.

"Nimeona hii changamoto ya maji pamoja na kwamba wanachimba kisima, lakini kile kijiji pale ambacho kinakwamisha kinahujumu miundombinu ya maji, DC pamoja na kamati ya usalama muende pale, pamoja na mwenyekiti wa halmashauri, mkazungumze na kile kijiji, lakini kama kuna watu ambao wanadhaniwa wanahujumu kwa makusudi miundombinu. Haiwezekani kijiji kizima kikawa kinahujumu miundombinu, mchukue hatua ya kuwakamata hao wote wanaohujumu miundombinu ya maji," alisisitiza.

# Waliovamia msitu waamriwa kuondoka

**Na Yasmine Protace, KIBITI**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kibiti mkoani Pwani, imewataka wananchi, waliovamia msitu wa Ngumbuluni na kuufyeka kisha kupanda mazao ya ufuta na korosho kuondoka mara moja katika msitu huo.

Imeelezwa kuwa kufyekwa kwa msitu huo kunaweza kuisababishia halmashauri hiyo, kuupoteza.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Khatibu Chaulembo, katika kikao cha robo mwaka cha Baraza la Madiwani.

Chaulembo alisema wilaya hiyo ina misitu miwili, ambapo msitu wa Ngumbuluni upo mpakani mwa Kibiti na Rufiji, lakini umevamiwa na wakazi wa Ikwiriri kwa kufyekwa ikiwamo kupanda ufuta na miti ya mikorosho.

"Wanaojijua wamevamia katika msitu huo na kupanda ufuta na korosho wahame wenyewe kabla hatua dhidi yao hazijachukuliwa," alisema.

Aliongeza kuwa kama hatua hazitachukuliwa kuulinda msitu huo, halmashauri itaupoteza.

Chaulembo aliongeza kuwa kila wiki wamejiwekea utaratibu wa kufuatilia msitu huo ili kuhakikisha watu hawaingii, ikiwamo na kutoa elimu kwa wananchi juu ya kutovamia katika msitu huo.

Chaulembo aliwataka wananchi kutoendelea kulima katika msitu huo.

## HABARI KIMATAIFA

# WHO: Mmoja kati ya wanne ameambukizwa ugonjwa hatari wa ebola

**KINSHASA,** Congo

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema kuwa mtu mmoja kati ya wanne katika Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ameambukizwa ugonjwa hatari wa ebola, lakini hafahamu.

Imetoa kauli hiyo wakati huu inapoendelea kusaidia kupambana na maambukizi ya ebola hasa mjini Beni, ambapo watu zaidi ya 2,000 wameambukizwa na wengine 1,357 wamepoteza maisha tangu Agosti, 2018.

Siku za hivi karibuni, wizara hiyo ilieleza kuwa maofisa wa afya wamejitahidi kutoa taarifa kuhusu namna ya kujizuia kupata ugonjwa huo, lakini wataalamu wanaonya kuwa ni muhimu sana kuwapo kwa uangalifu mkubwa.

WHO imesema matukio ya maofisa na vituo vya afya kushambuliwa, pia vimepungua ikilinganishwa na miezi iliyopita.

Ugonjwa wa ebola uligundulika katika Jimbo la Kivu Kaskazini mwa DRC Agosti Mosi mwaka jana na ukasambaa katika maeneo mengi na kufika Ituri, lakini haujasambaa katika mataifa jirani.

Hii ni mara ya 10 kwa ebola kuikumba nchi ya DRC, mara ya kwanza ikiwa mwaka 1976 na maambukizi haya ni mabaya baada ya yale yaliyoshuhudiwa katika nchi za Afrika Magharibi kati ya mwaka 2014 hadi 2016 na kusababisha vifo vya watu 11,300 katika nchi ya Sierra Leone.

RFI




Mwanamke nchini Sudan akiwa ameshika bango lenye maandishi ya kuhamasisha jeshi kusitisha mauaji ya raia. PICHA: REUTERS. **PICHA: MTANDAO**

# Jeshi lawakamata viongozi wa upinzani nchini Sudan

**KHARTOUM,** Sudan

VIKOSI vya usalama nchini Sudan vimewakamata viongozi watatu wa upinzani baada ya kukutana na Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed mjini Khartoum, ili kusaidia katika mazungumzo ya amani.

Mmoja wa viongozi waliokamatwa ni Mohamed Ismat wa muungano wa upinzani ambaye alikamatwa siku ya Ijumaa, huku Imsail Jalab na Mubarak Ardol wa kundi la waasi wa SPLM-North walikamatwa Jumamosi.

Hatua hiyo inajiri siku chache baada ya kuzuka kwa ghasia, ambapo wafuasi wengi wa upinzani waliuawa.

Kukamatwa kwa viongozi hao kunajiri siku chache baada ya utawala wa jeshi nchini Sudan kusema kuwa uko tayari kwa mazungumzo na muungano wa upinzani.

Ijumaa, Waziri Mkuu wa Ethiopia, Ahmed, alizuru taifa hilo, ili kuzipatanisha pande hizo mbili ambazo alikutana nazo katika mikutano miwili tofauti.

Lakini saa chache baadaye, habari zilisambaa kuhusu kukamatwa kwa Mohamed Ismat - mwanachama wa muungano wa upinzani na ofisa mkuu wa benki kuu nchini Sudan.

Baadaye wanajeshi walieleza kumkamata ofisa mwandamizi wa SPLM-North, Ismail Jalab na msemaji Mubarak Ardol, ambapo kiongozi wa chama hicho, Yasir Arman yeye alikamatwa Jumatano.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa, kukamatwa kwa viongozi hao kutazua kutoaminika kwa baraza la kijeshi linalotawala, ambapo makundi ya waandamanaji yanapanga kuendelea na kampeni yao Jumapili.

Esmat na Jalab ni viongozi wakuu wa muungano wa upinzani uitwao 'Freedom for Change' mwavuli wa upinzani unaoshirikisha viongozi wa maandamano na makundi ya waasi.

"Hii ni sawa na baraza la jeshi kusema kwamba linapinga juhudi za mpatanishi waziri mkuu wa Ethiopia," alisema Khalid Omar Yousef, ambaye ni kiongozi wa muungano wa upinzani.

Hata hivyo, baraza la serikali ya mpito TMC halijatoa tamko lolote kuhusu kukamatwa kwa viongozi hao.


Alhamisi Muungano wa Afrika (AU) ulisitisha uanachama wa Sudan na kuonya kuichukulia hatua zaidi iwapo mamlaka hayatakabidhiwa kwa raia.

Mwenyekiti wa Tume ya Muungano huo, Moussa Faki Mahamat, alitaka uchunguzi wa wazi kufanyiwa kuhusu mauaji yaliotokea nchini humo.

Wakati wa ziara yake mjini Khartoum, Waziri Mkuu wa Ethiopia Ahmed alizitaka pande zote mbili kuwa na ujasiri na kukubaliana kuhusu hatua zitakazolipeleka taifa hilo katika demokrasia.

Ahmed alikuwa amependekeza kuanzisha baraza la utawala wa mpito lenye raia nane na wanajeshi saba, huku kukiwa na rais ambaye atakuwa akibadilishwa mara kwa mara. **BBC**

# Kundi la G20 lajadili uzee kama hatari kwa dunia



Rais wa China, Xi Jinping (kushoto) akiwa na Rais wa Urusi, Vladimir Putin, alipohudhuria kongamano la kiuchumi la Urusi mjini St. Petersburg. **PICHA: REUTERS**

**TOKYO,** Japan

WATUNGA sera wa juu kutoka mataifa 20 yalioendelea zaidi kiuchumi (G20) wanashughulikia masuala ya kiuchumi yanayohusiana na uzee na kupungua kwa viwango vya kuzaa watoto.

Pia maofisa hao wanaangazia gharama za matibabu zinazoongezekana na upungufu wa wafanyakazi kwa wazee.

Mawaziri wa fedha kutoka mataifa hayo yalioendelea na yanayoinukia kiuchumi duniani pamoja na magavana wa benki kuu za mataifa hayo wanaokutana nchini Japan, ambapo idadi kubwa ya wazee ni kubwa, ambapo wameonywa kuangazia suala hilo kabla ya hali kuwa mbaya zaidi.

Waziri wa Fedha wa Japan, Taro Aso, ambaye ndiye mwenyeji wa mkutano huo, anasema kuwa cha msingi ni kwamba iwapo uzee utaanza kuonyesha athari zake kabla ya mtu kuwa tajiri, hakuna hatua zozote mwafaka zinazoweza kuchukuliwa.

Kundi hilo la G20 ni mchanganyiko wa mataifa yalioko kwenye ngazi tofauti za maendeleo na umri wa wakazi, kuanzia Japan ambayo idadi kuba ya wakazi wake wanazeeka kwa kasi.

Mkutano ujao utafanyika nchini Saudi Arabia ambayo ndiyo iliyo na idadi kubwa ya watu wa umri mdogo.

**DW**

# RC aunda kamati kuchunguza tuhuma

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel, ameunda kamati ya kuchunguza madai ya wananchi na madiwani walioandamana wiki iliyopita kupinga kuporwa ardhi yenye dhahabu katika machimbo ya Nyakafulu, wilayani Mbogwe.

Robert alisema jana kuwa ameamua kuunda kamati itakayovihusisha vyombo vya usalama kutokana na baadhi ya viongozi wa serikali kuhusishwa kwenye malalamiko.

Alitaja viongozi waliohusishwa na suala hilo ni Serikali Kuu, Halmashauri na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kushirikiana na matajiri kwamba wako nyuma ya mgogoro huo kwa lengo la kupora ardhi hiyo yenye dhahabu.

Gabriel alisema kamati hiyo itachunguza na kuwahoji wanaotajwa kuwa nyuma ya mgogoro huo.

Aidha, alisema licha ya kesi kuhusu eneo hilo iliyokuwa katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Kata kutolewa uamuzi, mdaiwa alikata rufani.

Awali, Diwani wa Nyakafulu ambako kuna mgogoro, Mathias Nyololo, na mwenzake wa kata ya Ushirika, Daud Mabenga, ambao walikuwa miongoni mwa waandamanaji, walisema walifanya hivyo kuishinikiza serikali ya mkoa kuingilia kati.

Kwa mujibu wa madiwani hao, wanaishinikiza serikali kuchukua hatua za haraka baada ya uongozi wa wilaya kuonekana kutotoa uzito madai hayo.

Maandamano hayo yamefanyika siku tatu toka hukumu ya madai ya ardhi kati ya mdai Julius Njololo kwa niaba ya familia ya Mzee Nyanga Njololo katika shauri lenye namba 20/2019 la madai ya ardhi katika Baraza la Usuluhishi wa Ardhi na Nyumba kata ya Nyakafulu wilayani Mbogwe dhidi ya Lutonja Mashilingi na Sandu Mboje kutolewa Mei 30, mwaka huu, kwa kumpa ushindi mdai wa kipande cha ardhi kilichokuwa kikibishaniwa uamuzi ulioibua maswali mengi.

Katika shauri hilo, upande wa madai ulidai katika baraza hilo kuwa kipande cha ardhi wanachokidai ni mali ya familia hiyo, lakini walihama tangu mwaka 1989 na kukiacha kabla ya kurudi mwaka huu na kukidai.

Upande wa wadaiwa unapinga madai hayo kwamba ulinunua ardhi hiyo tangu mwaka 1990 kutoka kwa Tungu Kisinza, utetezi unaoungwa mkono pia na baadhi ya wanajamii na serikali ya kijiji.

Baadhi ya wananchi, wakiwamo wanaodai kuwa waathirika wa uamuzi wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Kata ya Nyakafulu, walioshiriki kuandamana Juni 3, mwaka huu, Emmanuel Lutonja, Jackson Manyama na Lutonja Mashilingi, walisema kilichowasukuma kuandamana ni baada ya kuona hawakutendewa haki.

Aidha, walisema wamekata rufani katika Baraza la Ardhi na Nyumba kupinga uamuzi wa awali.



Mtaalamu wa huduma ya kwanza wa kampuni ya Zantel, Abbas Hussein, akionyesha jinsi ya kumsaidia aliyepata matatizo ya ugonjwa wa moyo akiwa katika kazi za kupanda juu, wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Afya na Usalama mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Naibu Waziri ataka NMB kukuza utalii kusini

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amepongeza juhudi za taasisi za fedha nchini kwa kuwakopesha wajasiriamali kwenye sekta utalii ili kuiwezesha kutoa mchango katika maendeleo ya uchumi.

Akizungumza juzi katika banda la benki ya NMB kwenye maonyesho ya wadau wa utalii yaliyoandaliwa na kampuni ya Karibu-Kili Fair, ambayo benki hiyo ni mdhamini, Kanyasu alisema uwepo wa taasisi za fedha utasaidia wadau wa utalii kupata mikopo kwa urahisi zaidi.

"Serikali inaunga mkono juhudi za NMB, mnafahamu namna ambavyo tumekuwa tukifanya kazi pamoja na umuhimu wa benki hii katika kusukuma juhudi za wananchi kujiletea maendeleo. Nitoe wito sasa mjielekeze kuwasaidia ukanda wa kitalii katika mikoa ya kusini ambako kuna fursa kubwa," alisema Kanyasu.

Alisema serikali imedhamiria kufungua eneo la ukanda wa Kusini na imewaleta makatibu tawala wa mikoa hiyo kuhudhuria maonyesho makubwa katika nchi za Afrika Mashariki ili kupata maarifa watakayoyatumia kutekeleza mradi wa Regrow unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwenye mikoa hiyo.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, David Kafulila, alisema Rais John Magufuli ametoa maagizo ya ukanda wa kusini kufunguliwa na wakiwa watendaji wa serikali wanaamini NMB itasaidia kuhakikisha wafanyabiashara wanapata mikopo.

Alisema wataweka mikakati ya kuhakikisha mikoa ya ukanda wa kusini ambayo ni Ruvuma, Songwe, Njombe, Iringa, Mbeya na Katavi inainuka kwenye utalii, ili ifanane na mikoa ya kaskazini ambako biashara hiyo imestawi kwa wingi.

Naye Mkuu wa Idara ya Wateja Wakubwa wa NMB, Filbert Mponzi, alisema benki hiyo imetenga Sh. bilioni 500 kwa ajili ya wajasiriamali wakiwamo walio katika sekta ya utalii eneo ambalo halijachangamkia sana mikopo kwa ajili ya kuongeza uwekezaji wao.

Alisema wamejipanga kushirikiana na serikali katika kuinua sekta ya utalii ukanda wa kusini baada ya kubainika vipo vivutio vingi maeneo hayo, lakini baada ya msukumo wa serikali ya awamu ya tano kuongeza juhudi litakuwa ni eneo la kimkakati kwao.



# Lugola aridhishwa na usalama JNIA

**Na Felix Mwagara**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, jana alifanya ziara katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (Terminal III) kukagua vyombo vyake vinavyotarajiwa kutoa huduma.

Lugola aliwasili katika uwanja huo akiwa ameambatana na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara yake, pamoja na taasisi zake na kupokewa na uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA).

Akizungumza baada ya kufanya ukaguzi uwanjani hapo, Lugola alisema hana shaka na utoaji wa huduma wa vyombo vyake katika uwanja huo mpya, kwa kuwa ameridhika na mipango ya utoaji huduma wenye weledi baada ya uwanja huo kufunguliwa.

"Wizara yangu ni wadau wakubwa katika utoaji huduma katika uwanja huu wa ndege. Ni lazima nijue Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na Idara ya Uhamiaji wamejipangaje katika kutoa huduma bora hapa uwanjani. Sina shaka nao, nimeridhika baada ya kumaliza ukaguzi," alisema.

Pia Waziri Lugola alimhakikishia Mkurugenzi Mkuu wa TAA, Mhandisi Julius Ndyamukama, kuwa ameridhishwa na mpangokazi wa vikosi hivyo vilivyojipanga kutoa huduma.

"Nimeridhishwa na utendaji kazi wa vyombo vya ulinzi na usalama vilivyoko chini ya wizara yangu vilivyojipanga juu ya utendaji kazi na watakavyotoa huduma kwa wasafiri wa uwanja huu. Lakini nimeelezwa baadhi ya changamoto chache na tunaahidi kuzifanyia kazi mapema kabla ya uwanja huu kufunguliwa," alisema.

Lugola alihakikishiwa na viongozi wa majeshi hayo kuwa watafanya kazi kwa nguvu zote kwa kutoa huduma bora katika uwanja huo.

"Tupo tayari kuutumikia umma na kwa kuwa kazi zetu ni kuusaidia umma wa Watanzania tupo tayari kuhakikisha uwanja huu mpya pamoja na viwanja vyote vinakuwa salama muda wote," alisema Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala.

Ndyamukama alimshukuru Waziri Lugola pamoja na viongozi wa wizara kwa kufika uwanjani hapo kufanya ukaguzi, ila alimuomba waziri huyo magari ya zimamoto yaongezwe ili kuhudumia uwanja huo mpya.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**ASI LINAKODISHWA,** Basi aina oyota HIACE dungu liko Dar nakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 754 316570 au 0715 316570 au 629 316570.

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI**
IT – DIPLOMA anahitajika kidato cha nne na sita. MESSENGER kidato cha nne na sita. Mawasiliano: 0715 885533.

## MAGARI NA VIPURI

**CRANE FUSO FOR SALE,**
(1.) Fighter 2002, SAKAI_340,3 stages, New in TZ,
2. Magnum 1991, TADANO_290, 2 Stages, 3 years in TZ.
**"Dalali Hatakiwi" Simu 0692 469 669**

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311**

## GOROFA INAUZWA



**BOKO KAMWANGA STR**
**LOW DENSITY AREA**
**BLOC "C",**
**PLOT NO. 65**

**SIMU**: 0754 226 687 / 0756 410 345.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HATIBU YUSUFU MADUDU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yake aina ya **TOYOTA RAV4** Yenye Engine **No. 1AZ0093494** na Chassis **No. ACA210034792**

Kwa atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu nae.

**USR/TR/RB/1841/2019.**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0767 223 311***

## JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

# Nipashe

NI JIBU LAKO,
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0767223311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Chelsea yamruhusu Sarri kwenda Juve



**LONDON,** England

KOCHA Maurizio Sarri amepewa ruhusu ya kuachana na Chelsea na kwenda kujiunga na Juventus kwa dili la miaka mitatu.

Kwa mujibu wa Sky Sports, wakala wa Mtaliano huyo, Fali Ramadani amekutana na mabosi wa Chelsea juzi na kufikia makubaliano hayo.

Juve sasa watalazimika kuilipa Chelsea fidia ya pauni milioni tano kwa ajili ya kupata huduma ya Sarri, ambaye katika miezi yake 12 aliyodumu huko Stamford Bridge amewasaidia kubeba ubingwa wa Europa League.

Hata hivyo, Sarri alisaini mkataba wa miaka miwili tu wakati alipotua Stamford Bridge mwaka jana akitokea Napoli.

Katika msimu wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu England, Sarri ameiwezesha 'The Blues' kurudi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao licha ya mashabiki wamekuwa wakimkosoa sana.

Chelsea ilimaliza nafasi ya tatu na walifungwa kwa penalti na Manchester City katika fainali ya Kombe la Ligi, kabla ya kwenda kuwachapa Arsenal kwenye fainali ya Europa Leauge na kumaliza msimu kibabe.

Pale Juve, Sarri atakwenda kurithi mikoba ya Massimiliano Allegri, ambaye alifutwa kazi mwishoni mwa msimu baada ya kushindwa kutamba kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya licha ya kwamba alitamba kwenye Serie A akibeba taji kwa misimu mitano mfululizo.

Kocha Allegri sasa anaweza kutua Chelsea, huku makocha wengine wanaotajwa kwenye mpango wa kwenda kufanya kazi Stamford Bridge ni Javi Gracia, Nuno Espirito Santo na Frank Lampard.

# PEREIRA KUPEWA MKATABA MPYA MAN U



**MANCHESTER,** England

NI wazi kwamba Klabu ya Manchester United msimu uliopita ilifanya vibaya na kukosa mafanikio kwani ilimaliza msimu bila kuambulia chochote ambapo walikosa mataji yote yakiwamo Ligi Kuu England, taji la Kombe la Ligi, FA, Uefa na hata pia wamekosa nafasi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Uongozi wa timu hiyo kwa kuliona hilo sasa wameonekana kuweka nguvu katika suala la kusuka upya kikosi hicho, ili kuweza kurudi kwenye makali yake kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Imeripotiwa kwamba, mchezaji wa timu hiyo, Andreas Pereira huenda akapewa mkataba mpya utakaomfanya adumu kwenye klabu hiyo hadi mwaka 2023.

Gazeti la The Sun limeripoti kwamba endapo mchezaji huyo atapewa mkataba mpya utaupiku mkataba wa sasa ambao unatarajiwa kuisha Machi mwakani, baada ya kocha mkuu wa timu hiyo, Ole Gunnar Solskjaer hapo awali kufanikisha jitihada za kumfanya mchezaji huyo adumu ndani ya timu hiyo hadi sasa.

Imeripotiwa kuwa Solksajer anapambana ili kumbakiza mchezaji huyo kwa muda mrefu ikiwezekana hadi kufikia miaka minne ijayo aendelee kuitumikia timu hiyo.

# Neymar aonyesha jeraha lake



**SAO PAULO,** Brazil

NYOTA wa timu ya Taifa ya Brazil, Neymar, hatimaye ameamua kuonyesha majeraha yake ambayo ameyapata mwishoni mwa wiki iliyopita kwenye mchezo wa kirafiki kati ya timu yake ya Brazil na Qatar.

Mchezaji huyo wa Klabu ya Paris Saint-Germain ameonyesha jeraha hilo kupitia akaunti yake ya kijamii ya Instagram, ambapo mguu wake wa kulia ukionyesha namna alivyojeruhiwa.

Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 27, alipata majeraha kwenye kifundo cha mguu dakika za mapema tu wakati timu yake ikiibuka na ushindi wa jumla ya mabao 2-0 dhidi ya Qatar Jumatano iliyopita.

Alisaidiwa kutoka nje ya uwanja kupitia madaktari wa wachezaji wa timu, huku akionekana akitokwa na machozi.

Kocha wa Brazil, Tite alinukuliwa akisema majeraha ya nyota huyo si makubwa licha ya Neymar kuonekana akitolewa nje ya uwanja kwa msaada wa madaktari, huku akiwa amevalia bandeji ngumu 'piopio'.

Kutokana na uzito wa jeraha "ankle" alilopata Neymar hatukuwa kwenye hali nzuri na huenda akachelewa kuwa sawa kimwili kwa ajili ya michuano ya Copa America mwaka 2019.

Kwa upande wa timu ya taifa, tayari umethibitisha kukosekana huduma yake kwenye mechi dhidi ya Bolivia Juni 14, mwaka huu.

## HABARI MICHEZO



# NDOA YA OZIL YAZUA HISIA KALI UJERUMANI

**INSTANBUL,** Uturuki

RAIS Recep Tayyip Erdogan alimsaidia mchezaji wa Arsenal, Mesut Ozil, kufunga ndoa na mpenzi wake jijini Istanbul nchini Uturuki na kuibua hisia kali kwa nchi yake ya sasa Ujerumani.

Ozil, ambaye chimbuko lake ni Uturuki, alizua hisia kali alipopiga picha na Rais wa Uturuki, Erdogan kabla ya Kombe la Dunia mwaka uliopita.

Baadaye alistaafu soka la kimataifa, akidai ubaguzi wa rangi na kutoheshimiwa baada ya picha hizo kusambaa nchini Ujerumani.

Kiungo huyo wa Arsenal alimuoa mpenzi wake malkia wa urembo wa Uturuki, Amine Gulse, katika hoteli moja ya kifahari karibu na kingo za mto Bosphorus.

Wanandoa hao walianza kuchumbiana 2017 na kutangaza kilichokuwa kikiendelea kati yao Juni mwaka jana.

Ozil alitangaza Machi mwaka huu kwamba alimuomba Rais Erdogan kuwa mshenga wake suala ambalo lilizua hisia kali nchini Ujerumani.

Helge Braun, Waziri wa Chansela wa Ujerumani, Angela Merkel, aliliambia Gazeti la Bild kwamba ilikuwa uchungu kumuona Ozil akimchagua kiongozi kama huyo baada ya shutuma alizopata na rais huyo wa Uturuki mwaka uliopita.

Erdogan wakati huo huo aliripotiwa kwamba ni nadra sana kwa yeye kuhudhuria harusi nchini Uturuki hususan wakati wa kampeni za uchaguzi.

Hatua yake ya kuhudhuria harusi ya Ozil inajiri wakati ambapo uchaguzi wa marudio wa Meya unasubiriwa mjini Instanbul.



# Guardiola auhofia msimu ujao EPL

**MNACHESER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema kwamba msimu ujao wa Ligi Kuu utakuwa na ushindani mkubwa zaidi na kwamba, bingwa wake atapatikana baada ya vita kubwa.

Msimu wa Ligi Kuu ya England wa 2019/20 unatarajiwa kuanza miezi miwili ijayo na Guardiola ameibuka na kuonyesha woga wake kuhusiana na ligi hiyo.

Man City iliweza kutetea ubingwa wa wake msimu uliopita licha ya kupata upinzani mkubwa kutoka kwa Liverpool katika msimu wa mwaka 2018/19.

Guardiola amesema Liverpool na Manchester City zilionyesha ushindani mkubwa ila msimu ujao timu zitaongezeka.

"Hapa kuna ushindani mkubwa wa ajabu japo msimu huu ilionekana ni sisi na Liverpool, lakini timu nyingine tano zipo zenye nguvu ndio maana ligi inakuwa ngumu, tusubiri msimu ujao utakapoanza tutaona kitakachotokea," alisema.

# Griezmann afunguka atakapotua msimu huu

**PARIS,** Ufaransa

ANTOINE Griezmann amesema anajua wapi atakapokuwapo msimu ujao, huku akihusishwa na kujiunga na mabingwa wa La Liga, Barcelona.

Griezmann ataondoka Atletico Madrid baada ya kuitumikia kwa kipindi cha miaka mitano na mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa, ameripotiwa atajiunga na Barca.

Wakati Griezmann, Atletico na Barcelona bado suala hilo likiwa halijatatuliwa, mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 28, anaonekana ameshafanya maamuzi kichwani.

"Ninajua wapi nitakapocheza msimu ujao," Griezmann, ambaye pia amekuwa akihusishwa na Paris Saint-Germain na Manchester United aliiambi Telematin.

"Ninaweza kusema tu haitakuwa Miami."

Griezmann – ambaye kwa sasa yupo katika majukumu ya kitaifa akiwa na Ufaransa, alijiunga na Atletico akitokea kwa wapinzani wao wa Hispania, Real Sociedad mwaka 2014.

Tangu ametua, Griezmann ametwaa ubingwa wa Kombe la Europa League, UEFA Super Cup na Supercopa de Espana in Madrid.

Griezmann amefunga mabao 15 kwenye La Liga wakati Atletico ikimaliza nafasi ya pili nyuma ya Barca wakati akitupia mabao 21 katika mashindano yote msimu huu.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAZARD AWEKA REKODI YA USAJILI REAL MADRID

●●● Kwa sasa ni wazi, nataka kuweka katika rekodi, kitu kimoja kilichokuwa wazi kwangu ni... **Hazard.**

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imeingia makubaliano ya kumsainisha mshambuliaji Eden Hazard kwa dau la pauni milioni 150.

Hazard amekubali kusaini mkataba wa miaka mitano na atatambulishwa kama mchezaji wa Real Madrid Juni 13, mwaka huu, baada ya kufanyiwa vipimo vya afya.

Mchezaji huyo wa Ubelgiji alifunga mabao 110 katika mechi 352 akiichezea Chelsea baada ya kujiunga akitoka ile ya Ufaransa mwaka 2012 na kucheka na nayavu mara mbili, wakati wakishinda Kombe la Ligi ya Ulaya wiki iliopita.

**"Kuondoka kwangu Chelsea ni uamuzi mkubwa na mgumu zaidi katika kipindi changu chote cha kucheza soka," alisema**

Akiandika katika mtandao wa facebook aliongezea: "Natumai mnaelewa kwamba nililazimika kutafuta changamoto mpya kama vile inavyokuwa kawaida wakati mtu anapowania kufikia ndoto yake.

"Kwa sasa ni wazi, nataka kuweka katika rekodi kitu kimoja kilichokuwa wazi kwangu, nimependa kila wakati wangu nilipokuwa chelsea na hakuna hata siku moja nilifikiria kwamba huenda nikahamia klabu nyingine.

Mkurugenzi wa Chelsea Marina Granovskaia alisema kumbukumbu alizowaacha nazo hazitaangamia.

"Aliwafurahisha wote walioitazama Chelsea ikicheza na kwa hivyo tunamshukuru sana Eden Hazard. Amekuwa mtaalamu wa kuigwa katika kipindi chake chote akiichezea Chelsea , mtu vizuri kushirikiana naye na kufanya kazi naye."

Katika misimu saba akiichezea Chelsea Hazard ambaye mkataba wake katika Klabu ya Chelsea ulikuwa unakaribia kukamilika baada ya mwaka mmoja, alishinda Kombe la Ligi na lile la Ulaya mara mbili Kombe la FA na lila la Ligi.

Pia alichaguliwa kuwa mchezaji bora wa Chelsea mara nne.

"Japokuwa ni uchungu sana kumwambia kwaheri Hazard licha ya klabu kumtaka kusalia, tunaheshimu uamuzi wake wa kuchukua changamoto mpya katika taifa tofauti na kufuata ndoto yake ya utotoni kuichezea Real Madrid," aliongezea Granovskaia.

Chelsea itaendelea kutumikia adhabu yake ya kifungo cha usajili, ikiwa na maana kwamba hawataweza kumsajili mbadala wa Hazard hadi mwisho mwa Januari 2020.

Walishindwa katika rufani yao ya kwanza na sasa wamewasilisha rufani yao ya pili katika mahakama ya inayoshughulika na mambo ya michezo, Cas.

## KWA UFUPI

### BALE KWA MKOPO UNITED
Manchester United inataka kumsajili kwa mkopo winga wa Wales, Gareth Bale, 29, kutoka Real Madrid. (Sunday Mirror)

### BECKHAM AMTAKA VALENCIA
David Beckham anamtaka beki wa kulia wa Ecuador, Antonio Valencia, 33, kujiunga na klabu yake ya Inter Miami. Valencia ameondoka Manchester United majira haya ya joto baada ya mkataba wake kumalizika. (Sun on Sunday)

### CITY KUIACHIA UNITED MAGUIRE
Manchester United na wapinzani wao, Manchester City wanataka kwenda kumsajili beki wa kati wa Harry Maguire, 26, lakini City inaweza kuwekwa kando na dau la pauni milioni 90 linalotakiwa na Leicester. (Mirror)

### CARRASCO AKARIBIA ARSENAL
WINGA wa Dalian Yifang na Ubelgiji, Yannick Carrasco, 25, anakaribia kutua Arsenal. (Sport)

### LIVERPOOL YAKITA KWA LIGT
Liverpool ni miongoni mwa klabu sita zinazohitaji huduma ya beki wa Ajax, Matthijs de Ligt. (Mirror)

### LINGARD KUFUNGWA TENA UNITED
KIUNGO wa England, Jesse Lingard, 26, anajiandaa kupewa ofa ya mkataba mpya utakaomwezesha kulipwa pauni milioni 130,000 kwa wiki hapo Manchester United. (Sun on Sunday)

### MOURINHO AITAKA NEWCASTLE
Jose Mourinho amewaambia marafiki zake kwamba atahitaji kuinoa Newcastle na anafungua mazungumzo na mmiliki mpya wa klabu hiyo, Sheikh Khaled bin Zayed Al Nehayan. (Sunday Mirror)

### ARSENAL KUNASA WAWILI
Arsenal inakaribia kukamilisha usajili wa nyota wawili kutoka Sampdoria, kiungo Mbelgiji Dennis Praet, 25, na beki wa kati, Mdenmark Joachim Andersen, 23. (Gazzetta dello Sport, via Talksport)

### BUFFON KURUDI TENA PARMA
KIPA mkongwe wa Italia Gianluigi Buffon, 41, atakuwa anajiandaa kurudi klabu yake ya kwanza ya Parma baada ya kutangaza ataondoka Paris St-Germain majira haya ya joto. (La Gazzetta dello Sport, via Goal - in Italian)

### FELIX AIPASUA KICHWA BENFICA
RAIS wa Benfica, Luis Filipe Vieira, amesema njia pekee ya kumbakisha mshambuliaji wao, Joao Felix, 19, ni kumuuza kwa mkopo kwa lengo la kumrudisha msimu ujao. Mchezaji huyo anawaniwa na Manchester United na Manchester City zinavutwa na nyota huyo wa kimataifa wa Ureno. (Sunday Mirror)

### UNITED YATOA OFA KWA KOULIBALY
Manchester United imetoa ofa ya pauni milioni 84 kwa beki wa kati wa Napoli na Senegal, Kalidou Koulibaly, 27. (Corriere dello Sport, via Mail)

### TOTTENHAM YAMUWINDA AKE
Tottenham itatoa ofa ya pauni milioni 40 kwa beki wa kati wa Bournemouth na Uholanzi, Nathan Ake, 24. (Sun on Sunday)

### LIVER KUMPIGA BEI WILSON
Liverpool ipo tayari kumruhusu winga raia wa Wales, Harry Wilson, 22, kuondoka kwa ada ya pauni milioni 21. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 aliutumia msimu uliopita akicheza kwa mkopo Derby na Hoffenheim na RB Leipzig imeripotiwa kuvutiwa naye. (Sunday Mirror)

## HABARI MICHEZO

# AIYEE: MLANGO UPO WAZI SIMBA, YANGA

**Na Mwandishi Wetu,**

BAADA ya kufanikiwa kuibakiza Mwadui FC Ligi Kuu Tanzania Bara, mshambuliaji tegemeo wa timu hiyo ya Shinyanga, Salim Aiyee, amesema milango iko wazi kwa Simba, Yanga na klabu za nje ya nchi kufanya naye mazungumzo kwa ajili ya kumsajili.

Aiyee ambaye alifunga mabao 17 msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliomalizika hivi karibuni, juzi alicheka na nyavu mara mbili katika ushindi wa 2-1 dhidi ya Geita Gold FC na kuiwezesha klabu yake ibakie katika ligi hiyo ya juu nchini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Aiyee, alisema amepokea ofa mbalimbali, lakini bado hajaridhishwa na dau alilopewa, hivyo ataendelea kujihesabu yeye ni mchezaji wa Mwadui FC.

Aiyee alisema anakiamini kiwango chake na kwa sasa hana haraka ya kufanya uamuzi wa kusajili mpaka pale atakavyoona, amepata dau linalomridhisha.

"Kuondoka ni mapenzi ya Mungu, sisi wacheza mpira ni kama wafanyabiashara, kama itakuja klabu na hela nzuri, basi nitakwenda, nina ofa nyingi kutoka klabu za ndani na nje ya Tanzania, lakini bado hawajafikia kiwango cha pesa ninachokitaka," alisema Aiyee.

Aliongeza kwamba hatakiwi pia kuona anakwenda katika timu ambayo haitaendeleza kipaji chake, kwa sababu bado ana ndoto za kusonga mbele katika mchezo huo.

"Naamini nitapata timu nzuri na bora ya kuitumikia kwa ajili ya msimu ujao, sitaki kufanya uamuzi wa haraka, ila kama nitakosa, nitabakia hapa Mwadui, kwangu ni kama nyumbani, ingawa mimi ni mtu wa Tanga, ila kipaji changu kimeonekana kupitia hapa Mwadui," Aiyee aliongeza.

Mwadui FC na Kagera Sugar iliyoshinda mabao 2-0, zimebakia katika ligi hiyo baada ya kushinda mechi zao za marudiano za mchujo 'Play off' na kuzifanya Geita Gold na Pamba kuiendelea kubaki Ligi Daraja la Kwanza msimu ujao.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania "Taifa Stars" wakiwa mazoezini katika Uwanja wa Movenpick jijini Cairo, Misri jana asubuhi kujiandaa na fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019. **PICHA: TFF**.

# Vita ya kucheza Afcon yapamba moto Stars

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA hali inayoonyesha kila mchezaji anataka kuwapo katika kikosi kitakachopeperusha bendera ya Tanzania (Taifa Stars), kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, ushindani kwenye mazoezi ya timu hiyo umeongezeka.

Kikosi cha Stars kilichoondoka nchini Ijumaa iliyopita kikiwa na wachezaji 32, ambapo baadaye watachujwa na kubakia 23, kinafanya mazoezi yake kwenye Uwanja wa Movenpick jijini Cairo.

Nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta, alisema wachezaji wote walioko katika kambi hiyo sasa wanapambana na huwezi kujua kirahisi nani atatemwa kutokana na namna wanavyojituma.

"Tulifika Misri salama na tumeanza mazoezi, tunaamini mambo yatakwenda vema, tunachoomba ni uzima, tufanye vitu ambavyo Watanzania hawatarajii, tunataka kuweka historia," alisema kwa kifupi mshambuliaji huyo wa KRC Genk inayoshiriki Ligi Kuu Ubelgiji.

Stars iliyoko chini ya Mnigeria Emmanuel Amunike, inajiandaa kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Misri itakayochezwa Alhamisi mjini Alexandria na nyingine dhidi ya Zimbabwe watakayovaana Juni 16, mwaka huu.

Katika mechi za Afcon, Stars ambayo iko Kundi C itacheza mechi yake ya kwanza dhidi ya Segenal Juni 23, halafu itakutana na Kenya (Juni 27) na itamaliza hatua ya makundi Julai Mosi, mwaka huu kwa kupambana na Algeria.

# Maxime afunguka 'kuichinja' Pamba

**Na Lilian Lugakingira,**
BUKOBA

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema "Nilijua nitawachinja", baada ya timu yake kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Pamba FC ya jijini Mwanza na kujinusuru na janga la kushuka daraja.

Mabao ya Kagera Sugar katika mchezo huo yalifungwa dakika ya 51 na Ally Ramadhan, huku bao la pili likifungwa na Japhet Makalayi dakika ya 78.

Akizungumza na Nipashe, Maxime alisema hakuwa na wasiwasi wowote katika mchezo huo, kutokana na uzoefu aliokuwa nao yeye pamoja na wachezaji wake.

Alisema kilichotokea mpaka timu yake kufikia hatua ya kucheza mechi ya mchujo 'Play Off' ni "mitihani ya Mungu", lakini anawapongeza wachezaji wake kwa kupambana na hatimaye kubakia Ligi Kuu Tanzania Bara.

**"Kwanza niseme kuwa sikuwa na wasiwasi, ninaiamini timu yangu, naamini taaluma yangu, ila kilichotokea ni mitihani ya Mungu, katika mpira na katika maisha changamoto hizi ni za kawaida, Mungu alitaka tujifunze kitu, tumejifunza tunasonga mbele, " Maxime alisema.**

Kocha Mkuu wa Pamba, Ally Kisaka, kwa upande wake alisema timu yake imefungwa "nje ya uwanja" kutokana na vitendo walivyofanyiwa siku moja kabla ya mchezo.

Kisaka alisema wamepoteza mchezo, watafanya tathmini na baadaye kujipanga upya kwa ajili ya msimu ujao.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, aliwashukuru wananchi wa mkoa huo kwa kuonyesha uzalendo na hamasa kubwa kwa wachezaji na kusababisha timu kupata ushindi na kusalia Ligi Kuu.

"Hakuna timu iliwahi kujaza watu kama leo, nawashukuru sana wana Kagera, sasa nimeshinda, tuendeleze umoja tusonge mbele," alisema Gaguti.

Aliongeza kuwa sasa watajipanga kuhakikisha timu yao inakuwa ya ushindani katika kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kusahau yaliyopita kwa sababu walikuwa wanaichukulia "poa" timu hiyo.

Michezo

Jumatatu Juni 10, 2019

Nipashe

Hazard aweka rekodi ya usajili Real Madrid



HABARI UK. 30

RAIS MPAMBE...



Kiungo wa Arsenal, Mesut Ozil, akipozi katika picha baada ya kufunga ndoa mwishoni mwa wiki na mpenzi wake, malkia wa urembo wa Uturuki, Amine Gulse, jijini Istanbul nchini Uturuki, huku akiwa na mpambe wake [Best Man] Rais wa nchi hiyo, Recep Tayyip Erdogan (wa saba kulia) na mkewe. Wengine ni ndugu jamaa na marafiki wa Ozil waliohudhuria shughuli hiyo. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA NAYO KAMA SIMBA KAGAME CUP

## ●●● Yatoa sababu kuu nne kujitoa michuano hiyo, Azam pekee yatangaza kambi huku...

**Na Somoe Ng'itu**

SIKU chache baada ya mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kutangaza kujitoa kushiriki katika mashindano ya Kombe la Kagame, watani zao Yanga nao wametangaza kutoshiriki michuano hiyo ambayo mwaka huu inatarajiwa kufanyika kuanzia Julai 7 hadi 21 jijini Kigali, Rwanda.

Yanga ilikuwa timu mwalika katika mashindano hayo kwa mwaka huu, wakati Simba walikuwa wanaenda kama mabingwa wa Tanzania Bara na Azam FC iliyobakia, wao ni mabingwa watetezi wa michuano hiyo inayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

Tayari Azam FC inayotarajia kuwa na kocha mpya Mrundi Etienne Ndayiragije, imetangaza kikosi chake kitaingia kambini Juni 18, mwaka huu, ili kuanza maandalizi ya kutetea kombe hilo kwa mara ya tatu.

Ofisa Habari wa Yanga, Dismas Ten, alisema jana kuwa Yanga inaishukuru Cecafa kwa kuwapa mwaliko wa kushiriki mashindano hayo, lakini wanaamua kujitoa kutokana na changamoto kuu nne walizonazo katika kikosi chao baada ya msimu wa mwaka 2018/19 kumalizika.

Ten aliitaja sababu ya kwanza ni kutokuwa na wachezaji wenye mikataba hivyo, wanashindwa kufahamu hatima yao na wachezaji wengine wapya waliowasajili, bado hawajakamilisha taratibu za kuachana na klabu zao za awali.

Msemaji huyo alianika sababu ya tatu iliyowafanya wachukue uamuzi huo ni kutokuwapo kwa Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera na baadhi ya wachezaji wao watakuwa kwenye mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019), ambayo yanafanyika nchini Misri kuanzia Juni 21 hadi Julai 19, mwaka huu.

Aliitaja sababu nyingine ni kuwapa likizo wachezaji wao waliobakia na hivyo wanakiri hawatakuwa na kikosi imara kitakachowafanya wawe na timu itakayotoa ushindani katika michuano hiyo.

"Kwa muktadha huo, ni ngumu kwetu kushiriki michuano hii kwa sababu hatutakuwa na kikosi imara ambacho kinaweza kutoa ushindani wa kweli," alisema Ten.

Aliongeza kuwa, Yanga inawashukuru Cecafa kwa kuwapa mwaliko huo, na inaahidi kuendelea kushirikiana nao kushiriki mashindano hayo katika misimu ijayo.

Mbali na Yanga, timu nyingine zilizoalikwa kushiriki mashindano hayo ya mwaka huu ni AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Zesco United kutoka Zambia.

Simba yenyewe kupitia Ofisa Mtendaji Mkuu wake, Crescentius Magori, ilisema kuwa imebanwa na kalenda yake, na inahitaji muda wa kwenda kufanya maandalizi ya msimu ujao, huku ikipanga kwenda kuweka kambi Marekani.

## Ndoa ya Ozil yazua hisia kali Ujerumani

**INSTANBUL, Uturuki**

RAIS Recep Tayyip Erdogan alikubali kuwa mpambe ['Best Man'] wa mchezaji wa Arsenal, Mesut Ozil wakati akifunga ndoa na mpenzi wake jijini Istanbul nchini Uturuki na kuibua hisia kali kwa nchi yake ya sasa ya Ujerumani.

Ozil, ambaye chimbuko lake ni Uturuki, alizua hisia kali alipopiga picha na Rais wa Uturuki, Erdogan kabla ya Kombe la Dunia mwaka uliopita.

Baadaye alistaafu soka la kimataifa, akidai ubaguzi wa rangi na kutoheshimiwa baada ya picha hizo kusambaa nchini Ujerumani.

Kiungo huyo wa Arsenal alimuoa mpenzi wake malkia wa urembo wa Uturuki, Amine Gulse, katika hoteli moja ya kifahari karibu na kingo za mto Bosphorus.

INAENDELEA UK 29

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >